

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tatu – Tarehe 4 Novemba, 2021

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali. Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swalii lake.

Na. 31

Ujenzi wa Daraja la Gunyoda - Mbulu

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Daraja la Gunyoda ambalo linaunganisha Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu hususani Tarafa ya Mang'ola kwenye mashamba ya vitunguu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishachukua hatua za kufanya upembuzi wa awali kwenye Korongo la Gunyoda lililoko katika Barabara ya Waama-Masieda, Kata ya Gunyoda katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ambako ndiko daraja hilo litajengwa. Korongo hilo lina urefu wa mita 70.4 na kina cha mita 5.0. Kutokana na ukubwa wa korongo hilo, upembuzi ulibainisha kuwa, ili kujenga Daraja la Gunyoda zinahitajika shilingi bilioni 1.2. Fedha hizi ni zaidi ya ukomo wa bajeti ya Halmashauri katika Fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kuona umuhimu wa daraja la Gunyoda ikizingatiwa daraja hilo linaunganisha Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha daraja hilo linajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali kuitia Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; nini kauli ya Serikali kwa kuwa Daraja la Gunyoda limepoteza maisha ya wakazi wa Jimbo la Mbulu Mji hasa nyakati za masika? Kwa kuwa daraja hilo ni kubwa na linaunganisha halmashauri mbili imekuwa kikazo kikubwa sana kwa huduma za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa tatizo la kuongezeka kwa makorongo katika nchi yetu limekuwa kubwa na tatizo hili linachochewa na mabadiliko ya tabianchi. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutuma

Watalaan wa Wizara, Mkoa na Halmashauri zote nchini ili wafanye mapitio upya katika maeneo haya ili waandae mpango wa kuzuia kuongezeka kwa makorongo, lakini pia na ujenzi wa maeneo ambayo yatapewa kipaumbele katika bajeti za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza anataka kauli ya Serikali juu ya hilo korongo ambalo linatakiwa kujengwa daraja. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi Serikali ya Awamu ya Sita, moja ya kazi yake kubwa ambayo tumekubaliana kuifanya sasa hivi ni kuunganisha maeneo yote kwa kujenga madaraja hususani katika maeneo korofi. Kwa hiyo na daraja hili katika mpango wa fedha wa mwaka unaofuatia tutaliweka katika vipaumbele vyetu kuhakikisha daraja hili na lenyewe linapatiwa fedha ili liweze kujengwa kwa umuhimu ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema hapa kwamba daraja hili linaunganisha halmashauri mbili kwa maana ya Mbulu Mji na Halmashauri ya Mbulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, lilihusu maongezeko ya makorongo, akawa anataka Serikali tufanye tathimini upya kwa kutuma watalaan ili tuweze kuzuia uendelezaji huu. Moja; nipokee kama ushauri kwamba sisi kama Serikali tumepokea, lakini la pili; ni kwamba kwa hivi karibuni tulishawatuma wahandisi wetu nchi nzima kukagua na kuanisha maeneo yote korofi hususani madaraja ili tuweze kuyatengea bajeti na yaweze kuitishwa. Kwa hiyo na hili ni

sehemu ya mapendekezo ambayo ameyatoa na sisi tunaendelea kuyapokea. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia korongo liliopo katika Wilaya ya Mbulu Mji ambalo linaenda mpaka Wilaya ya Karatu na katika Tarafa ya Yasi ambako kuna wakulima wa vitunguu katika maeneo hayo. Sasa je, Serikali haionti ipo haja ya kikutanisha *TANROADS* Mkoa wa Arusha kwa maana ya Wilaya ya Karatu na *TANROADS* Mkoa wa Manyara ili kwa pamoja kuwe na nguvu ya kuhakikisha haya madaraja ambayo yanaathiri wilaya mbili yanapatiwa ufumbuzi ili wananchi waweze kufanya shughuli zao kama inavyotakiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubali na nipokee ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Serikali ni moja na tunafanya kazi kama wamoja, basi kwa kutumia hadhara hii niahidi tu kwamba tutakaa pamoja na watu wa ujenzi kuhakikisha, hao *TANROAD* Arusha na Manyara wanakutana na kufanya tathmini katika maeneo hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha. Kwa hiyo tumepokea ushauri wake na tutaufanyia kazi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massay.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo. Jimbo

la Mji Korongo hili la Gunyoda linalosemwa lipo kwenye barabara moja hiyo hiyo kuja Jimbo la Mbulu Vijijini, lipo korongo la Hudaya ambalo lina thamani kubwa ya 1,200,000,000.

Je, Serikali ipo tayari sasa na hii ya Hudaya kuweka kwenye mpango kwa sababu ukiweka hili la Gonyoda la Hudaya utakuwa hujaweka kwenye mpango wa kujengwa barabara hiyo itakuwa haitumiki kabisa.

Je, Waziri yupo tayari na hili ili barabara itumike?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swalii dogo la nyongeza Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa sababu na hili ni ombi jipya na bahati nzuri lilishafanyiwa tathmini na gharama ya fedha na jukumu letu sisi kama Serikali ni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa hayo madaraja. Kwa hiyo na lenyewe nilipokee tutaenda kushauriana na wataalam ili na lenyewe tuliiingize katika mpango wa awamu inayofuatia. Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnavyopewa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza nenda moja kwa moja kwenye swalii. Mheshimiwa Joseph Kiswaga, swalii la nyongeza.

MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kuuliza swalii la nyongeza moja. Rais aliyepita, Mheshimiwa Magufuli alituahidi kutujengea daraja kutoka Kata ya Ifunda kwenda Kata ya Lumuli sasa napenda kujua, je, tumefikia hatua gani kutekeleza hiyo ahadi? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swalii la dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba Serikali ya Awamu ya Sita, moja ya mpango wetu ni kwamba ahadi zote za Viongozi Wakuu na Viongozi wetu Wastaafu na ile ambayo ilitolewa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, zote zipo katika mipango ya utekelezaji wa Serikali. Kwa hiyo, aondoe shaka zipo pale na Serikali inachosuburi tu ni namna ya kuzitekeleza. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kasekenya.

MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la *X-ray* ni tatizo ambalo tupo nalo katika vituo vyetu vya afya vya Kisolya, Kasaunga na Kasuguti.

Je, ni lini Serikali itapeleka *X-ray* katika vituo hivyo vya afya?

NAIBU SPIKA: Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde utamtafutia majibu Mheshimiwa Mbunge, ukishirikiana na Naibu Waziri anayeshughulikia Afya, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene.

Na. 32

**Hitaji la Wodi za Kulaza Wagonjwa na Mashine ya
X-Ray Kituo cha Afya Itobo**

MHE. SELEMANI J. ZEDI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo la Wodi za kulaza Wagonjwa pamoja na kupeleka mashine ya X-raykatika Kituo cha Afya Itobo kilichopo Jimbo la Bukene?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imepeleka shillingi milioni 250 katika Kata ya Itobo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kituo hicho ili kiweze kuwa na uwezo wa kutoa huduma za upasuaji. Ujenzi wa majengo hayo umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo 30 Aprili, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa vituo hivi vyatya afya unafanyika kwa awamu. Hivyo, baada ya awamu hii ya kwanza ya ujenzi kukamilika, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo mengine ikiwemo wodi katika Kituo cha Afya cha Itobo. Aidha, mashine za X-ray zitaendelea kununuliwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, swali la nyongeza.

MHE. SELEMAN J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kupeleka milioni 250 katika Kituo cha Afya cha Itobo ili kuboresha miundombinu ya pale, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vituo vyatya afya vyatya zamani kama Kituo cha Afya cha Itobo na Kituo cha Afya

cha Bukene vinaitwa vituo vya afya, lakini kimsingi havina ile miundombinu mizuri ambayo inafaa kuitwa kituo cha afya. Unakuta kinaitwa kituo cha afya, lakini hakina maabara, hakina wodi, hakina *theater*, hakina *X-ray*. Kwa hiyo, swali langu ni kwamba je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari baada ya Bunge hili na kabla ya Bunge la Februari kwenda Jimboni Bukene atembelee hivi vituo vya afya vya zamani ambavyo ni tofauti kabisa na vituo vya afya vya sasa, japo tunahesabiwa kwamba tuna vituo vya afya, lakini kimsingi haviendani kabisa na hali halisi inayopaswa kuwepo kama kituo cha afya? (*Makofij*)

NAIBU WAZIRI: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suleiman Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipokee pongezi zake kwa kazi hii kubwa ambayo imeendelea kufanywa na Serikali Awamu ya Sita, chini ya Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha tunajenga vituo vya afya ikiwemo katika Kata ya Itobo. Hata hivyo, nimhakikishie kwamba Serikali tunatambua vyema kwamba ni kweli vituo vyetu hivi bado vina upungufu wa miundombinu na ujenzi huu kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi ni wa awamu. Kwa hiyo, tuko awamu hii ya kwanza ya ujenzi wa majengo ya kuanzia, lakini awamu ya pili tutakwenda kujenga majengo mengine yakiwemo wodi, lakini na majengo mengine ya vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwahidi Mheshimiwa Zedi kwamba niko tayari, tutakubaliana baada ya Bunge hili, tupange ratiba ya kwenda kule Bukene, tupitie Vituo vya Afya vya Itobo na Bukene, tuweze kufanya tathmini na kuona mpango wa kuendeleza ili viweze kuwa na hadhi ya vituo vya afya. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Changamoto iliyopo Bukene ni sawasawa na changamoto iliyopo Makete katika Kituo cha Afya cha Matamba ambacho kinahudumia zaidi watu 25,000, lakini hakina jengo la mama na mtoto, hakina X-ray. Kwa hiyo, naomba Serikali iniambie ni lini italeta fedha pale Matamba ili wananchi wangu waweze kupata huduma? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Matamba Makete ni kituo ambacho kinategemewa na wananchi wengi zaidi ya 25,000, lakini ni kweli kwamba kina upungufu wa miundombinu ya majengo likiwemo jengo la mama na mtoto.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imechukua changamoto hiyo tunatafuta fedha ili twende kujenga majengo hayo mengine kuhakikisha wananchi wa Matamba wanapata huduma za kituo cha afya kilichokamilika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Itigi ambacho kinahudumia watu wengi katika Mji wa Itigi kama hospitali, je, Serikali ni lini itapeleka X-ray katika kituo hiki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa vituo hivi vya afya unaendana na uwekaji wa vifaa tiba zikiwemo mashine hizi za X-ray na ununuzi wa mashine hizi unakwenda kwa awamu kwa kadri ya bajeti zetu. kwa hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua kwamba Kituo cha Afya cha Itigi kina uhitaji mkubwa wa X-ray na kinahudumia wananchi wengi, hivyo tutaendelea kutafuta fedha ili tupate mashine ya X-ray kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika Kituo cha Afya cha Itigi. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Simon Lusengekile, swali la nyongeza.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hospitali ya Halmashauri ya Busega inahudumia takribani wakazi 300,000 na hatuna kabisa X-ray inabidi wananchi wale kwenda kutafuta huduma za X-ray kwenye wilaya nyingine kama Bariadi, Bunda na Magu. Je, ni lini Serikali itaipatia X-ray Hospitali ya Halmashauri ya Busega ili iweze kuhudumia wananchi wake? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Hospitali hii ya Wilaya ya Busega haina mashine ya *X-ray* na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika vipaumbele vya kipeleka mashine za *X-ray*, kipaumbele cha kwanza ni kipeleka katika hospitali za halmashauri.

Kwa hiyo, kadri ambavyo tunaendelea kuweka mipango yetu tutahakikisha hospitali zote za halmashauri zinakwenda kupata *X-ray* na ushahidi tumeona katika fedha hizi za UVIKO tunakwenda kununua *digital X-ray* zaidi ya 75 kwa ajili ya hospitali zetu za wilaya ambazo hazina, lakini pia vituo vya afya ambavyo vina idadi kubwa ya wananchi. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba tutaipa kipaumbele Hospitali ya Wilaya ya Busega. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 33

Idadi ya Mabilionea Tanzania

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Tanzania ina idadi ya watu takribani milioni hamsini na tano wenye madaraja tofauti ya uchumi:-

Je, katika idadi hiyo Tanzania ina mabilionea wangapi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba, majibu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia utafiti uliofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenye mwaka wa fedha 2014/2015 na baadaye kurejewa mwaka 2019/2020, unaonesha kuwa idadi ya mabilionea duniani inakadirisha kufikia watu milioni kumi na nne. Kwa mujibu wa Ripoti ya Capgemini and *RBC Wealth Management, July 2019*. Bara la Afrika pekee lina mabilionea 140,000 sawa na asilimia moja ya mabilionea wote wa dunia nzima. Kati ya idadi ya mabilionea waliopo Barani Afrika, mabilionea 5,740 wanatoka Tanzania ambao wanamiliki asilimia 4.2 ya utajiri katika kundi la mabilionea wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha mionganoni mwa mabilionea 5,740 waliopo Tanzania, mabilionea 115 sawa na asilimia mbili ya utajiri wa zaidi ya dola milioni 30 wanaomiliki zaidi ya asilimia 28 ya utajiri wote wa mabilionea wanaotoka Tanzania. Kati ya hawa mabilionea waliopo Tanzania wengi wamesajiliwa na Mamlaka ya Mapato yaani *TRA* na wanalipa kodi zao katika Idara ya Walipa kodi Wakubwa na wamewekeza katika Sekta za Viwanda, Nishati na Madini ikiwemo pia Sekta ya Fedha, Mawasiliano pamoja na Uchukuzi, Utalii na Makazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu haya ya Serikali ambayo kwa kweli yanaonyesha bado tuko nyuma sana, maana kati ya 140,000 kwa Afrika sisi tuna 5,000 sawa na asilimia 4.2: Sasa ni upi mkakati wa Serikali katika kuhuisha sera na sheria ambazo wakati mwingine ndiyo zinazokua kikwako katika ukuaji wa mitaji wa kibashara na uwekezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Mheshimiwa Waziri ametaja sekta mbalimbali ambazo mabilionea hawa aliotatajwa wanatoka, lakini kwa masikitiko makubwa hakuna hata mmoja anayetokana na Sekta ya Kilimo na Mifugo na Uvuvi. Haoni kwamba kwa stahili hiyo wakulima, wafugaji na

wavuvi wataendelea kuwa wasindikizaji katika eneo zima hili la kiuwekezaji wa mitaji? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, majibu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Shangazi kwa swali lake nzuri. Nampongeza kwa jana niliambiwa alikuwa anashabikia moja ya timu iliyoshinda kwa mbinde sana. Taarifa alizonipa Mkuchika anasema, basi timu yake isingeshinda, mpaka sasa mpira ule ungekuwa bado unaendelea kuchezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mabilionea hawa tuliotaja, tumewataja tu kwa mfano. Tumetoa tu mifano ya baadhi ya sekta ambazo tumeweza kuzainisha, lakini haina maana kwamba kwenye Sekta ya Kilimo na Mifugo hakuna mabilionea. Hata Sekta ya Mifugo na Sekta ya Kilimo wapo mabilionea na takribani kila mkoa kwenye sekta hiyo ya kilimo mabilionea wapo kuanzia ngazi zote; kuanzia kwenye kulima kwenyewe wapo ambao wako ngazi ya *processing* ambazo ziko ngazi ya viwanda, lakini wapo pia wa ngazi ya *export*. Kwa hiyo, hii tulitolea tu mifano ya baadhi ya maeneo ambayo yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta nyingine zipo ambazo hatujazitaja kwa kiwango kikubwa na zenyewe zina mabilionea ambao wako. Kwa mfano, King Musukuma pamoja na wengine ambao na wenyewe wapo katika makundi yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba tuna sera gani? Serikali ina sera na moja ya maeneo ambayo tumeyapa uzito mkubwa ni kutengeneza mazingira bora kabisa ya ufanyaji biashara ambapo tunahamisha watu kutoka kundi moja la kipato kwenda kipato kingine na mkakati huo unaanza na biashara kuanzia zile zilizo ndogo kwenda biashara zilizo kubwa na zilizo kubwa kwenda kwenye ngazi ya mabilionea ili Tanzania iweze kuwa na mabilionea wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tamko lilitolewa siku siyo nydingi sana, hata Wabunge wanakaribishwa waungane na King Musukuma kwenye kundi ille la mabilionea ili waendelee kuongozwa kwa mfano kwa wananchi hao wanaowaongoza. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Kwanza tunashukuru kwamba umeanza kututajia mabilionea walioko humu ndani, wakiongozwa na huyo uliyemsema.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, ninalo tangazo moja hapa la kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa taarifa kwamba ye ye hatakuwepo Dodoma kwa ajili ya majukumu yake ya kikazi. Kwa muktadha huo, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, atakuwa anakaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kwa hiyo, mumpe ushirikiano wote na mnaona amekaa sehemu inayohusika kabisa pale. Kwa hiyo, hamna wasiwasi, Serikali iko vizuri Bungeni.

Mheshimiwa Halima James Mdee, swalii la nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, ili mtu aweze kuwa bilionea, wengi wanaanza katika biashara ndogo ndogo. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, unaanza na biashara ndogo ndogo, unafika kati na hatimaye unakuwa mkubwa ukiacha wale ambao wanarithi. Sasa imekuwa ni utamaduni wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwafukuza Wamachinga ambao wanatumia kipato chao kidogo kwenye maeneo yao ya biashara na kuwapeleka pembezoni na maeneo ambayo hayajaandaliwa na mazingira ambayo siyo wezeshi kufanya biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuthibitisha kwamba Serikali haijali kundi hili la wafanyabiashara wadogo wadogo, hapa kwenye mpango ambao Waziri ameusoma jana, hakuna maeneo ambayo anazungumza atawapanga vipi hawa vijana wetu? (*Makofi*)

Sasa nataka Waziri aniambie, kwa kuwa anatambua ili uweze kuwa milionea na hatimaye bilionea, lazima uanzie chini; na kwa kuwa anatambua...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja, ninakuja. Serikali...

NAIBU SPIKA: Aah, uliza swali, kwa sababu umepewa nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina uwezo wa kuajiri asilimia mbili tu: Je, sasa ana mpango gani rasmi wa kuingiza eneo hili muhimu katika Mpango wetu ambaao tutakuja kuufanya kazi Januari, kwa kundi hili kubwa la vijana ambalo sasa hivi wanahangaika mtaani?

NAIBU SPIKA: Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Halima kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali inayowajali sana wafanyabiashara wadogo. Mfano na uthibitisho mmoja ni kwamba mabilionea wote walioko katika nchi hii, ni zao la Chama cha Mapinduzi kwa sababu hakuna chama kingine kimewahi kuongoza. Kwa hiyo, mabilionea wote unaowaona katika nchi hii na wengine wame-spill over mpaka nchi za SADC na nchi nyingine kwa ukombozi wa Chama cha Mapinduzi. Ni zao la Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hawa ambaao wako hapa, amesema Mpango haujasema watapangwa vipi? Mpango wa nani akae wapi, ni suala la kisekta ambalo litafanywa na Serikali za Mitaa. Kwa upande wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Rais ana mpango mzuri sana na kundi hili ambalo Mheshimiwa Halima amelisema la wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa sababu ndiyo kwanza bado tunaendelea kuchambua huu Mpango,

tutawapa undani wake Waheshimiwa Wabunge, ni kwa sababu tu hatukusema kwa kuwa bado tuko kwenye mazungumzo ya awali. Hata hivi tunavyoongea, tunaendelea kuongea na wenzetu wa Benki ya Dunia, lakini pia tunaendelea kuongea ndani ya Serikali kutengeneza utaratibu ambalo lengo lake kubwa hasa ni kuwafanya hawa ambao tumewataja kwa jina la Wamachinga waweze *ku-graduate*, wapige hatua kwenda kwenye hatua nyingine inayofuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema hii mtaiona katika Mpango huu na mtaona katika bajeti hii inayokuja na wenyewe Wamachinga watakuwa mashahidi kwamba kumbe kweli huu Mpango ulikuwa ni mwema ambapo umetufanya *tu-graduate*. Kwa sababu katika hali ya kawaida, hakuna Mmachinga anayetaka aendelee kuwa Machinga katika malsha yake yote. Hata wao wanataka siku moja wawe kama GSM wafanye mambo ya kweli na yanayoonekana katika nchi hii. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa sasa aulize swalie lake.

Na. 34

**Serikali Kuingia Makubaliano na Chuo cha Ufundi
cha Lugarawa - Njombe**

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA aliuliza: -

Je, ni kwa nini Serikali isiingie makubaliano na Chuo cha Ufundi Lugarawa kinachomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Njombe kwa kupeleka Walimu, vifaa na fedha za ruzuku ili Wanaludewa na Wanajombe wapate mafunzo wakati ujenzi wa Chuo cha VETA Shaurimoyo ukisubiriwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Eilimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa haina utaratibu wa kushirikiana katika kutoa mafunzo kwa pamoja na taasisi binafsi. Hata hivyo, Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi, zikiwemo taasisi za dini katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini. Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha taasisi zake za elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga vyuo katika ngazi za Wilaya na Mkoa na kuvipatia vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa lengo la kuhakikisha kwamba watananzia wanapata elimu bora ya ufundi karibu na maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Njombe, Serikali inamiliki Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Makete chenye uwezo wa kudahili wanafunzi 160 kwa mwaka. Kwa sasa Serikali inaendelea kupanua Chuo hicho kwa kuongeza madarasa matano yenye uwezo wa kubeba wanafunzi 100 kwa wakati mmoja, mabweni mawili yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 72 kwa kila moja na nyumba mbili za watumishi, kila moja ikiwa na uwezo wa kubeba familia mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inaendelea na matayarisho kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Njombe kitakachojengwa katika Wilaya ya Ludewa kuititia fedha za *IMF*. Aidha, ujenzi wa chuo hicho unatarajiwa kuanza mwezi huu wa Novemba, 2021. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swalii la nyongeza.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali

mawili ya nyongeza. Moja, namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kutupa Mpango wa Serikali: Ni kwa muda gani chuo hiki kitakuwa kimekamilika na kuanza kutoa mafunzo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili: Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Ludewa kwa umoja wao wamechangia fedha na nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya wanafunzi watakaokuwa na ufaulu mkubwa wa Darasa la Saba.

Je, ni lini Serikali katika kutambua jitihada za wananchi na kuunga mkono juhudii zao? Ni lini Wizara itatuma watalaamu kwa ajili ya kwenda kusajili shule ile ili watoto waweze kuanza kusoma pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; naomba sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kamonga Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Kamonga pamoja na wananchi wa Ludewa na vilevile Watanzania wengine walioko kwenye Mikoa ya Rukwa, Geita pamoja na Simiyu, kwa sababu katika maeneo ambayo vyuo vya mikoa vinaenda kujengwa ni pamoja na maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la muda, tunatarajia ndani ya miezi minane kutoka leo vyuo hivi vinakwenda kukamilika kwa sababu fedha hizi zina muda maalumu wa utekelezaji kuhakikisha kwamba miradi hii inafanyiwa kazi sawa sawa. Kwa hiyo, niwahakikishie tu, Mheshimiwa Rais ametoa fedha hizi kwa kuhakikisha katika kipindi hiki kifupi huduma hizi zinaweza kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili, anazungumzia Shule ya Sekondari; nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Ludewa kwamba taratibu za kufuata zipo wakati wa kufanya ukaguzi na kusajili shule hizi. Namshauri Mheshimiwa Mbunge kupitia Mkurugenzi wa Halmashauri kuweza kuandika barua kupeleka kwenye idara yetu ya Udhibiti Ubora iliyokuwepo katika Wilaya ile ya Ludewa na wataalamu wetu wale wakishapata tu barua na maombi hayo, mara moja wanatakiwa kwenda kwa ajili ya kufanya ukaguzi ili kutengeneza ithibati iwapo viwango vile vimethibitika kuwepo, basi usajili huo utapatikana. Ila kwa vile amelizungumza suala hili hapa Bungeni, tutakwenda kulifanyia kazi kuhakikisha kwamba wiki ijayo wataalamu hao waweze kwenda kwenye eneo hilo la shule ili kuweza kupata usajili ili vijana wetu kama Januari shule hii inaweza kufunguliwa, iweze kufunguliwa na wanafunzi waweze kupata huduma. Ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ningependa tu kujua ni lini Serikali sasa itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Kilolo ambayo tayari ina ongezeko la vijana na chuo kinahitajika ili nao waweze kuijendeleza kama ilivyo kwenye maeneo mengine? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba sasa kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Serikali inaendelea na ukamilishaji wa vyuo vile vya VETA katika wilaya 29 ambazo sasa zinakwenda kukamilisha, lakini siyo tu kukamilisha na kuhakikisha vile vile vifaa kwa ajili ya

mafunzo vinaweza kupatikana. Kwa hiyo katika mwaka huu wa fedha, juhudhi za Serikali tunajikita kwenye eneo hilo, kukamilisha vyuo hivi vya wilaya 29, lakini na vile vya mikoa vinne. Kwa hiyo, nimhakikishie, baada ya ukamilishaji wa vyuo hivi, Serikali sasa tunajipanga vizuri kutafuta fedha ili kuweza kufikia wilaya zote kama sera yetu inavyosema kwamba kila wilaya ni lazima iwe na Chuo cha Ufundı cha *VETA*. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii. Matatizo ya Ludewa yanafanana sana na matatizo ya Wilaya ya Muleba. Wilaya ya Muleba ni kubwa yenye watoto wengi wanaohitimu darasa la saba, *form four* na kidato cha sita.

Je, ni lini Serikali itatujengea Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Muleba? (*Makofı*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba sasa kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kikoyo, Mbunge wa Muleba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwa upande wa Kilolo, Serikali inaendelea kutafuta fedha baada ya ukamilishaji wa vyuo hivi 29 katika wilaya 29 ambayo tumeanza kwa awamu ya kwanza kuweza kuzifikia wilaya nyingine ikiwemo na Wilaya ya Muleba. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Kikoyo katika muda mfupi ujao baada ya Serikali kupata fedha tutahakikisha kwamba kila wilaya tunaifikia ikiwemo na wilaya ya Muleba. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mtemvu swali la nyongeza.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam lina idadi kubwa ya watu zaidi ya milioni sita na tunategemea Chuo cha VETA kimoja tu maarufu cha Chang'ombe na Wilaya ya Ubungo sasa ipo pembezoni na idadi kubwa ya watu na eneo tunalo:-

Je, ni lini sasa Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Ubungo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kutoa jibu dogo kwa Mheshimiwa Mtemvu Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye maeneo mengine, nitoe rai na wito kwa Mheshimiwa Mtemvu, kwa sababu Ubungo ni Jiji na ni eneo kubwa na mapato yake ni makubwa, kwa hiyo, aone umuhimu nalo wa jambo hili. Basi angalau kwenye mapato ya ndani pale kama wanaweza wakatoa kasma kidogo wakaanza mchakato huu wa ujenzi, pindi pale Serikali itakapopata fedha kwa ajili ya vyuo hivi vyta wilaya, basi tutakwenda kuongezea nguvu na kukamilisha chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri naona Wabunge wengi wanaauliza vyuo vya VETA huko kwenye maeneo yao, hebu tuambia kwa ujumla mpango wa Serikali kuhusu ujenzi wa vyuo vya VETA. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mpango uliokuwepo hivi sasa kwa mwaka huu wa fedha, bado tunaendelea na ukamilishaji wa vyuo vile 29 na vile vile kununua vifaa. Kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha vyuo hivi siyo tunajenga tu majengo, bali vile vile kuhakikisha kwamba tunapeleka

pamoja na vifaa ili viweze kufanya kazi na kutoa elimu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mwaka ujao wa fedha, jukumu la Serikali ni kuhakikisha kwamba sasa tunaweza kutenga bajeti kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa vyuo vingine vya wilaya. Huo ndiyo mpango uliopo mpaka hivi sasa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 35

Serikali Kugharamia Matengenezo ya Reli ya TAZARA

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kugharamia matengenezo ya Reli ya *TAZARA* ambayo miundombinu yake imechakaa na ni muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania na hata nchi jirani za *SADC*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (*TAZARA*) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya *TAZARA* Na. 23 ya mwaka 1975 iliyorekebishwa kwa Sheria ya *TAZARA* Na. 4 ya mwaka 1995. Reli hiyo inamiliikiwa kwa uwiano wa hisa hamsini kwa hamsini baina ya Serikali ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania inatambua umuhimu wa kugharamia matengenezo ya reli ya *TAZARA* na ndiyo maana inaendelea na jitihada za kukamilisha marekebisho ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1995 ambayo kukamilika kwake kutaondoa changamoto zinazoathiri uwekezaji katika reli hiyo kwani uwekezaji unaofanyika sasa hauongezi thamani ya hisa za nchi inayowekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa changamoto hiyo, Serikali ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa *TAZARA* inaendelea kutoa huduma wakati jitihada za marekebisho ya sheria zikiendelea. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Serikali ya Tanzania iliipatia *TAZARA* jumla ya shilingi bilioni Kumi kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya kutengenezea vichwa saba vya treni na vifaa vya kuongeza uwezo mgodi wa mawe na kiwanda cha kutengenezea mataruma ya zege vilivyopo Kongolo Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipuri na mashine hizo vimeshanunuliwa na matengenezo ya injini yamekamilika mwaka 2020 na hivi sasa zinafanya kazi. Mashine kwa ajili ya Kongolo zinafanya kazi pia. Aidha, Serikali ya Tanzania inaendelea kulipa mishahara ya wafanyakazi wa *TAZARA* upande wa Tanzania ambapo katika Bajeti ya mwaka 2021/2022 zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 14.98.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Serikali kuwa mchakato wa kurekebisha Sheria ya *TAZARA* utaisha hivi karibuni baada ya Serikali ya Zambia kukamilisha zoezi linaloendelea la uteuzi wa viongozi katika ngazi mbalimbali na kuwa tayari kwa kikao cha pande zote mbili kwa ngazi ya Makatibu Wakuu na hatimaye Mawaziri ili kuridhia mapendekezo ya marekebisho ya Sheria tunayoyasubiri. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hali ya madaraja ya *TAZARA*, hasa kwa upande wa mataruma ya mbao, yana hali mbaya sana kiasi cha kuhatarisha maisha ya wasafiri pamoja na usalama wa mizigo. Je, Serikali ina mkakati gani na mpango wa haraka kupeleka fedha ili hayo madaraja yaweze kukarabatiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; *TAZARA* ni muhimu sana katika ushindani wa Bandari yetu ya Dar es Salaam, huu ushindani wa kikanda unaifanya bandari yetu kuwa katika *pressure* kubwa sana. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga pesa ya kutosha kupitia *TPA* Shirika letu la Bandari ili liweze kushiriki katika kujenga na kuboresha miundombinu ya *TAZARA*? Nashukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, anatoa taarifa ya hali mbaya ya Reli yetu ya *TAZARA*. Ninaomba nimuelekeze Mtendaji wetu wa *TAZARA* atembelee maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, afanye tathmini ya haraka ili tuone kama hali ni mbaya kiasi hicho Mheshimiwa alivyozungumza basi ufanyike utaratibu wa kawaida kufanya marekebisho ili kuepuka madhara kwa mizigo na abiria ambaa wanatumia eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, Mheshimiwa Mbunge anauliza kama kuna uwezekano wa *TPA* kuwekeza katika eneo hili. Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Kamati tumekutana kule *TPA* Dar es Salaam, wazo hili alilitoa ni wazo jema. Tumewapa maelekezo watu wa *TPA* waangalie uwezekano wa kuwekeza katika eneo hili kwa sababu wanaihitaji *TAZARA* katika kusafirisha mizigo, walifanyie kazi, wafanye tathmini, tukijiridhisha basi wazo la Mheshimiwa Mbunge tutalifanyia kazi. Lengo ni kuweza kutoa huduma kwa watu wetu, hasa upande wa Tanzania. Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swalii la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa njia pekee ya kuisadia *TAZARA* ni kubadilisha hiyo sheria iliyoanzisha *TAZARA*, Serikali inatoa tamko gani la haraka kuhakikisha sheria hiyo inabadilishwa ili Tanzania iwekeze zaidi kuliko wenzetu wa Zambia wanaosuasua? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spik, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sheria hii imekuwa ni kikwazo kwa upande wa Tanzania kuwekeza katika reli hii kwa sababu kama nilivyosema, hisa ni asilimia 50 kwa 50. Kila ukiwekeza upande wa Tanzania haiongezi hisa katika upande wetu, lakini nia ya Serikali ni kwamba ingewezezana hata leo sheria hii ingeweza kubadilishwa

tuwekeze katika upande wetu kuweza kutoa huduma kwa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba sheria hii hatuwezi kuibadilisha upande wa Tanzania mpaka tukutane na watu wa Zambia. Wenzetu walikuwa na uchaguzi wameshamaliza, wamefanya uteuzi wa viongozi mbalimbali, tumeshawaandikia barua tunasubiri wakijibu tukutana jambo hili nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge litafanyiwa kazi haraka sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei, swali la nyongeza.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuuliza kuhusu hii reli kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi na Arusha ilifufuliwa, sasa imekufa, ni kitu gani kimeiu? Naomba Waziri hebu tueleze. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kimei kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hii reli haijafa ila zipo changamoto ambazo tunaendelea kuzifanyia kazi, kuongeza vitendeakazi pamoja na wafanyakazi katika eneo hili. Mheshimiwa Mbunge avute subira tunalifanyia kazi, reli hii itaendelea kufanya kazi ambavyo imekusudia Serikali, ndiyo maana ikaanzishwa baada ya muda mrefu sana. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri inabidi mtusaidie kwa sababu inakuwa ngumu sana kuwaambia

wananchi kwamba tunasubiria watu wa Zambia ili sisi tufanye marekebisho kwa upande wetu. Nadhani angalieni namna ya kulifanya hilo kwa sababu wanaosafiri wengi katika kipande hiki cha Dar es Salaam mpaka hapo ambapo wanaanza Zambia kwa maana ya Tunduma hapo, wanaosafiri ni Watanzania wengi hapo. Sasa kama madhara yatatokea ni kwa Watanzania, sio kwa wenzetu ambao wao pengine wana changamoto zao huko.

Nadhani tuangalie namna ya kufanya ile ambayo tunaweza kufanya upande wetu kama ambavyo tunalipa mishahara, basi na haya mengine tuendelee kuyafanya Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 36

Kuanzisha Benki ya Uvuvi Nchini

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Benki ya Wavuvi nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB*) tayari ipo kwa ajili ya kutoa huduma za kifedha kwa

wadau wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi. Benki hii ilianzishwa mnamo mwezi Septemba, 2012 chini ya Sheria ya Makampuni (Sura ya 212).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha Benki hiyo ili kusaidia kuongoza mageuzi ya kuleta maendeleo kwenye sekta ya kilimo sambamba na kujenga uwezo wa wadau kutekeleza programu mbalimbali za kuongeza thamani mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Benki hii inatoa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa watu binafsi na vikundi vinavyojishughulisha na sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge awahamasishe wavuvi kuchangamkia fursa mbalimbali za mikopo na huduma nyinginezo za kifedha zinazotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, swali la nyongeza.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri yanayotia moyo. Lakini katika sentensi yake tu ya kwanza amesema ile ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo na mimi nazungumzia wavuvi.

Sasa ninataka kujua, je, ni vigezo gani vinavyotumika ili hao wavuvi waweze kupata mikopo katika hiyo Benki ya Kilimo?

Swali la pili; ninataka kujua, kwa kuwa wavuvi wengi bado hawajapata elimu kuhusiana na mikopo hiyo; Je, Serikali ina mpango gani wa kuzungukia wavuvi hao ili wapate elimu waweze kunufaika na mikopo hiyo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swalilake la kwanza kuhusu ni vigezo gani. Kwanza ni kuomba ama kama nilivyooleza katika jibu la msingi, mtu mmoja ama kikundi, waombe kwa watoaji wa mkopo kwa maana ya benki. Tunashauri vikundi, hasa vyaya ushirika kwa kuwa ni rahisi zaidi kulingana na sera yetu kupata mkopo kisha benki watakapokuwa wameombwa wataeleza nini kimepungua na nini kinachohitajika ili mwombaji aweze kukamilisha utaratibu. Kwa hiyo namshauri Mheshimiwa Malembeka na wavuvi wote kutembelea katika mabenki mbalimbali na wanaweza kupata msaada wa kuelezwa ni nini hasa vile vigezo vinavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili la utoaji wa elimu ni endelevu na limekuwa likiendelea kufanya wakati wote, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Malembeka ya kwamba tutaendelea kufanya kazi hii ya kutoa elimu kwa wavuvi wetu juu ya uvubi endelevu katika Taifa letu na wenye manufaa. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, sasa aulize swalilake.

Na. 37

**Wenyeviti wa Halmashauri na Wabunge kuwa
kwenye Kamati za Uvunaji Mali za Misitu**

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza: -

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuwajumuisha Wenyeviti wa Halmashauri na Wabunge kwenye Kamati za

kujadili na kuitisha maombi ya wavunaji wa mali za misitu kwenye Wilaya zetu nchini?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, uwakilishi wa wananchi upo katika ngazi mbili. Ngazi ya kwanza ni ambapo Wenye viti na Watendaji wa Vijiji vinavyovuna hushiriki kwenye vikao vya Kamati, ngazi ya pili ni ambapo Waheshimiwa Madiwani na Wabunge katika vikao vya Baraza la Madiwani hupata wasaa wa kujadili na kutoa ushauri juu ya taarifa za Kamati zinazohusu maombi yote ya uvunaji wa miti na tathmini ya mwenendo wa uvunaji katika Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugawaji wa malighafi ya miti ya kuvunwa katika misitu ya asili ya Serikali unasimamiwa na Kamati ya Usimamizi ya Uvunaji katika kila Wilaya. Jukumu la kwanza la Kamati hii ni kujadili na kutoa maamuzi ya maombi ya uvunaji wa miti Wilayani katika misitu ya asili inayovunwa kwa ajili ya magogo, mbao, nguzo, fito, kuni na mkaa. Mazao hayo ni yale tu yatakayovunwa kwa ajili ya biashara. Jukumu la pili ni kufuatilia utekelezaji wa mpango wa uvunaji katika msitu husika na kutoa ushauri katika ngazi za Wilaya na Wizara pamoja na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa upandaji miti katika eneo la msitu unaovunwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru Serikali kwa majibu mazuri, na nimpongeze Naibu Waziri kwamba naye ameshafika Liwale kwa hiyo ninachokizungumza anakifahamu. Lakini hii sehemu ya pili anayosema kwamba Madiwani na Wabunge wanahuksika, kwamba wanapata hizi taarifa, mimi nimekaa Liwale miaka sita, sijawahi kupata hii taarifa zikiletwa kwenye Baraza letu la Madiwani. Kwa hiyo jambo hili labda leo aagize hili jambo lifanyike lakini hili jambo halifanyiki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, kwamba Kamati hii ya Uvunaji anayeingia mwanakijji ni Mwenyekiti wa Kijiji peke yake, sasa wanaovuna hesabu zinakuja pale wanaambiwa *cubic meters* yule mwanakijji *cubic meters* hajui, magogo mangapi yanaondoka hajui, matokeo yake kuna magogo yale makubwa ambayo yana mashimoshimo wanayaacha, kwa hiyo uharibifu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kufahamu, ni lini Serikali italeta fedha za upandaji miti kwenye vile vijiji ambavyo vina uvunaji huo ambao mimi nausema kwamba ni uvunaji wa holela?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili.

NAIBU SPIKA: Ulishauliza, mwanzo umesema atoe tamko, atoe agizo, na sasa umeuliza swali la pili.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema labda atoe tamko...

NAIBU SPIKA: Hapana, sasa hayo maelezo ya mwanzo ndiyo yaliyoashiria kwamba umeshauliza maswali mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kuchauka Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Kamati hii ni Kamati ambayo inaundwa katika *level/ya Wilaya*, lakini washiriki wa Kamati hii ni pamoja na Wenyeviti wa Vijiji na Watendaji wa Vijiji, pia inajumuisha Meneja wa Misitu ambaye anatoka Makao Makuu *TFS* lakini yuko pale Wilayani, kuna Afisa Misitu ambaye anakuwa ni mjumbe, vilevile kuna Afisa Tawala wa Wilaya ni mjumbe pia kuna Afisa Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaitamka hii Kamati ili afahamu Wajumbe wanaoingia mule ambaao sasa ndiyo wanapeleka taarifa kwenye Baraza la Madiwani kama taarifa ya wale wote tu waliopitishwa kwenye orodha ya uvunaji wa mazao ya misitu na anayekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ni Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Katibu ni Meneja wa Misitu anayetoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inapokuwa imekamilika inapelekwa kwenye Baraza la Madiwani. Baraza la Madiwani Wabunge ni Madiwani, wanashiriki pia Mwenyekiti wa Halmashauri ni Diwani na hawa Wenyeviti na Watendaji wa Vijiji wanapopeleka maombi yao kwenye hii Kamati ya Wilaya tayari wanaonekana ni wajumbe ambaao watapeleka tena kwenye *WDC* kama taarifa. Kwa hiyo taarifa hizi kuanzia *level/ya kijiji* kwenda *WDC* na mpaka kufika kwenye Halmashauri, Mbunge na Mwenyekiti anakuwa ameipata kupitia Mabaraza yanayofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niwaombe tu, kwa kuwa huyu Mjumbe ambaye ni Afisa Ardhi wa Wilaya anaingia kwenye hii Kamati na kama hafanyi hivyo basi anafanya makosa ni kwamba hii taarifa baada ya kukamilika inatakiwa ikasomwe kwenye Baraza la Madiwani ili

Waheshimiwa Wabunge wafahamu lakini pia na Mwenyekiti wa Halmashauri afahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya Mwenyekiti wa Halmashauri ama Mbunge, wale ni wasimamizi, hawawezi kuingia kwenye mchakato kama ilivyo maelekezo na miongozo ya uvunaji wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili ameongelea kuhusu fedha, ni kweli kulikuwa kuna changamoto ya fedha, tukipeleka kwenye Halmashauri, halmashauri zilikuwa hazifikishi kwenye maeneo husika ambayo kunatakiwa kuanzishwa vitalu na kupandwa hii miti ili kuziba yale maeneo ambayo yamekwisha vunwa. Kwa sasa tutapeleka hizo fedha lakini tutaleta mwongozo mahsusii wa kuhakikisha fedha hizi zinawafikia wale tu ambao wanahusika na fedha hizi na siyo Halmashauri kuelekeza kwenye matumizi mengine. Naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwatumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 38

Mpango wa Kukarabati Kituo cha Polisi Makunduchi

MHE. MWANTUMU DAU HAJI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali imepanga kuanza kukarabati majengo ya Kituo cha Polisi Makunduchi.?.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swalii la

Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uchakavu wa Kituo cha Polisi Makunduchi pamoja na nyumba za makazi ya Askari ambayo ni jengo la ghorofa moja linaloishi familia nne na mahanga mawili ya familia kumi na sita. Tathmini kwa ajili ya ukarabati imeshafanyika na jumla ya Shilingi 110,093,400 zinahitajika. Ukarabati huo ni wa kubadilisha paa, dari, mfumo wa maji safi na taka pamoja na kupaka rangi. Jeshi la Polisi linatafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo ikiwa ni pamoja na majengo mengine ya vituo na makazi ya askari yaliyokwisha fanyiwa tathmini. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza. Kwanza, nishukuru Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mama Samia Suluhu Hassan jinsi anavyo chapa kazi mwanamama, kweli kinamama tunaweza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri na Serikali yake inatambua uchakavu huu wa majengo ya polisi ya Makunduchi pamoja na makazi na wametenga jumla ya shilingi milioni kumi na moja na tisini na tatu mia nne, ambazo fedha hizi zinatakiwa ziende zikafanye ukarabati katika majengo haya na vituo vya polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo hivi vimechakaa sana, binafsi ukizingatia Makunduchi ni sehemu ya utalii hususan kila mwaka tunakwenda kule kukoga mwaka na viongozi wetu wakubwa wakubwa wanakwenda kule Makunduchi.

Kwa hiyo, je, Serikali lini itakwenda kuyatengeza majengo haya ili tuondoe kadhia hii ya majengo haya machakavu?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakinii suala langu la pili, namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri tena nasema tena, Mheshimiwa Naibu Waziri aende mwenye Makunduchi akayaone jinsi yale majengo pamoja na zile nyumba zilivyo chakaa. Tuoneeni huruma jamani, tunaona vibaya? Ahsante sana naomba kuwasilisha. (*Makofij*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NAMBO YA NDANIYA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kujibu masuala mawili mazuri sana ya nyongeza yaliyoulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Uguja, Mwantumu Dau Haji nayajibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja mionganoni mwa azma kubwa ya Serikali hasa kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kupitia Jeshi la Polisi ni kuhakikisha kwamba inaboresha na inatengeneza vituo vyote vya polisi vilivyopo nchini pamoja na nyumba za makaazi za maafisa hawa wa polisi na familia zao. Kwa hiyo, kubwa ni mwambie tu Kituo cha Makunduchi ni moja mionganoni mwa kituo ambacho tumeshakipanga na tayari fedha hizi tumo mbioni kuzitafuta na kupitia mwaka wa fedha ujao tutahakikisha kwamba kituo hiki tunakipa kipa umbele ili kijengwe na shughuli za kitalii na mambo mengine yaweze kuendelea vizuri na shughuli za ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo pia, nipo tayari kwenda Makunduchi kwenda kuona hilo eneo ili kuona namna ambavyo tunaweza tukashauri na tukaweza kupata fedha kwa ajili ya kukarabati hicho kituo. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika swali la nyongeza.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Njombe mpaka miaka michache

iliyopita ulionekana kama ni mkoa mpya. Katika maeneo yaliyosahaulika kwa Mkoa wa Njombe ni Vituo vya Polisi. Je, Serikali ni lini sasa itaanza kukarabati Kituo cha Polisi cha Mkoa wa Njombe ili kiendane na hadhi ya Mkoa wa Njombe? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo ameliuliza, linalozungumzia suala la ukarabati wa Kituo cha Polisi Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba azma yetu ni kuhakikisha kwamba vituo vyote vinajengwa ipo pale pale. Lakini kikubwa nimwambie tu kwamba tutajitahidi pia katika mwaka wa fedha ujao tuhakikishe kwamba kituo hiki nacho tunakijenga kikawa katika hadhi ile ya kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kupata huduma hizi za ulinzi na usalama. Nakushukuru pia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, jengo la Kituo cha Polisi katika Mji Mdogo wa Mlowo ambapo mpaka sasa hivi tayari kimeishawekewa alama ya X kwa sababu kimejengwa kwenye hifadhi ya barabara.

Nilikuwa naomba kufahamu nini mkakati wa Serikali wa kutujengea Kituo kipyaa cha Polisi pale Mlowo na ikizingatiwa kwamba tayari tunalo eneo ambalo limetengwa pale *Forest* maalum kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shonza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli moja mionganini mwa changamoto ambazo tuko nazo ni kwamba vituo vingi viro maeneo ya barabara na wakati Serikali inataka kutanua ama kupanua miundombinu ya barabara inabidi lazima kuna vituo viritishwe doza kwa ajili ya kuvunjwa ili sasa barabara itengenezwe. Sasa nimwambie tu Mheshimiwa kwamba kwa kuwa eneo lipo, basi tutajitahidi tutenge fedha kwa ajili ya kujenga kituo hicho ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata huduma za ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru pia.

NAIBU SPIKA: Kutokea Msekwa Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuku kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ningependa kujua kituo cha polisi Mgeta ambacho niliahidiwa kujengwa na niliambiwa nilete tathmini ya ujenzi wa kituo hicho ambacho wananchi wamejenga, tumefikia kwenye boma. Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Naibu mwenye waliniyahidi kwamba ikifika mwezi Agosti, 2021 kitakuwa kimeshamalizika kujengwa. Ni lini sasa watakwenda kumaliza hiyo ahadi yao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Getere nalo nalijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tulifika wakati tukaona kwamba tunaweza tukapata fedha haraka kwa ajili ya ujenzi wa kituo kile, lakini mambo yaliingiliana kwa sababu tuna nyumba za maaskari, tuna vituo vyaa polisi, tuna

mambo mengi ambayo polisi tunahitaji tuimarishe ili wananchi waweze kupata huduma hizo. Kubwa nimwambie tu kwamba katika mwaka wa fedha ujao tutajitahidi kituo kile tukiangalie, tutakipa kipaumbele ili wananchi waweze kupata huduma za ulinzi na usalama. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wa Kishapu na wadau wa maendeleo katika Wilaya ya Kishapu wameanzisha jengo kwa maana ya Ofisi ya *OCD* ya Wilaya ya Kishapu na jumla ya shilingi milioni 60 zimetumika na jengo hilo lipo hatua ya *renter*. Sasa je, Seikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba ina-*support* nguvu za wananchi na wadau ili mradi huduma za kipolisi ziweze kwenda sawasawa katika Wilaya ya Kishapu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniface nalo naomba nilijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze sana kwa kuwa ni moja ya mionganini mwa watu ambaao wanahamasisha sana wananchi ili kuweza kuanza ile miradi halafu Serikali kwa kuititia wafadhili tuje tuone namna ambavyo tunaweza tukamalizia. Kikubwa nimwambie kwanza, tutajitahidi baada ya Bunge hili tuje tuone hatua hiyo ambayo imefikia hicho kituo ili sasa tuone na sisi tathmini ya kuweza kujenga.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumwambie kwamba sasa tunakwenda kutafuta fedha, popote zilipo ili tuhakikishe

kwamba kituo hiki tunakimaliza na wananchi waweze kupata hizo huduma katika maeneo hayo. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, swali la nyongeza.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, hii habari ya vituo hayo yote tisa lakini kumi kuna Kituo Chukwani kimejengwa kwa nguvu za wananchi na kisha pauliwa tayari. Sasa ni ipi *commitment* ya Serikali ili kuja kumaliza kituo kile ambacho kinahitaji milioni 30 tu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ali Hassan King, Mbunge na Mtumishi wa wananchi wa Jimbo la Jang'ombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli ni kwamba kituo hiki tunakifahamu na binafsi nimeshakwenda kufanya ziara kwenye kituo hiki na hiyo *amount* ya fedha iliyotajwa tunakifahamu, kikubwa tulimwambia Mheshimiwa Mbunge ambaye alitupeleka katika eneo lile, ilikuwa ni Mheshimiwa Shah. Mheshimiwa Ahmada Shah tulikwenda kuona, kikubwa tulichomwambia kwamba sasa tunakwenda kutafuta fedha kwa sababu kama unavyojua siyo jambo la kusema kwamba tunachukua tu kesho tunakwenda kujenga. Ni jambo ambalo linahitaji taratibu za upatikanaji wa fedha kwa hiyo kikubwa nimwambie tu kwamba kituo hicho tunakifahamu na sasa tunakwenda kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa majibu kwa maswali ya Wabunge tumefika mwisho wa kipindi cha maswali. Nilita matangazo kabla hatujaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Kwanza, ni

wageni waliopo Bungeni mchana huu, wapo wageni ambao wamekaa jukwaa la Mheshimiwa Spika, wapo wageni 25 wa Mheshimiwa Spika ambao Wajumbe wa Bodi ya Biashara, Viwanda na Kilimo kwa maana ya *TCCIA* wakiongozwa na viongozi wa Bodi hiyo na hawa ni:-

Ndugu Pauli Koyi ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi na Rais wa Chembba hii, karibu sana, karibu sana mwenyekiti wa Bodi. Lakini pia yupo ndugu Dkt Meshark Kulwa ambaye ni Makamu wa Rais anayeangalia eneo la biashara, karibu sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Ndugu Clement Bocco ambaye ni Makamu wa Rais upande wa Viwanda, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Swallah Swallah ambaye ni Makamu wa Rais upande wa Kilimo, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Nebart Mwapwele ambaye ni Makamu Mkurugenzi Mtendaji Mkuu, karibu sana. (*Makofii*)

Sijui kama makamu au kaimu, nadhani ni kaimu sijui kama Mkurugenzi anaweza kuwa na Makamu. Karibuni sana sana viongozi wetu kutoka *TCCIA* Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge wageni hawa pamoja na mambo mengine siku ya leo Mheshimiwa Spika alipewa fursa ya kwenda kufungua ofisi yao ndogo hapa Makao Makuu Dodoma. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge huduma zote zinapatikana hapa, wafanyabiashara waliopo kwenye maeneo yenu, wenye viwanda waliopo kwenye maeneo yenu lakini pia wakulima kutoka kwenye maeneo yenu sasa *TCCIA* ina ofisi hapa Dodoma. Mnakaribishwa wote kwenda kutembelea hapo na kuwaelekeza watu wenu wakapate huduma hapo.

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni wa wanne wa kwangu kutoka Arusha ambao ni Waandaaji wa Shindano la *Miss Jungle International* na hawa ni:-

Ndugu Samwel Malugu ambaye ni Rais wa *Miss Jungle International*, karibu sana. Yupo pia, Ndugu Judith

James ambaye ni mshindi wa *Miss Jungle Tanzania* atakayeiwakilisha Tanzania kwenye Shindano la Dunia. Karibu sana. (*Makofii*)

Tunaye pia Ndugu Prisca Ephater ambaye ni Mkurugenzi wa Iyanna Foundation na Mjumbe wa katika Kamati ya *Miss Jungle International* karibu sana. Yupo pia Ndugu Simon Mollel ambaye ni Katibu wa Kamati ya *Miss Jungle*. Karibuni sana sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lao mahsusि litakuja wakati utakapowadia lakini *Miss Jungle International* itafanyika hapa Dodoma mwezi Desemba, siku ya tarehe 10, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana sana kushirikiana na vijana wetu hawa ambao wamebuni wazo zuri na sasa Ma-*Miss Jungle* kutoka Nchi zingine wote watakuja hapa Dodoma kwa ajili ya kushindana lakini pia itatusaidia sisi katika kutangaza utalii wetu. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, nafikiri mtawapa ushirikiano wa kutosha vijana hawa ili shindano hili litusaidie kutangaza utalii wa Nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na hawa ni wageni 3 wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Kellan Nkya, nadhani hawajapata fursa ya kuingia humu ndani lakini popote pale walipo wanakaribishwa sana.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Maafisa wa Idara ya Uhamiaji wapo hapa Bungeni katika Jengo la Utawala Ukumbi Na. 9, ghoroga ya chini kuanzia tarehe 02 - 12 Novemba, 2021. Maafisa hao wanatoa huduma ya hati za kusafiria zenye hadhi ya kidiplomasia za ki-electronic kwa Waheshimiwa Wabunge ambao bado wanamiliki hati za kusafiria za zamani.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wanaomiliki hati za zamani wanatakiwa kujaza fomu za maombi na kuambatanisha nakala ya hati ya zamani, barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Bunge na nakala ya Kitambulisho cha Mbunge. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaambiwa barua za utambulisho zipo tayari kwa hiyo mtu ambaye hana hati ya kusafiria ya ki-electronic ambayo pia ina hadhi ya kidiplomasia aende chumba Na. 301, ghorofa ya tatu Jengo la Utawala atakuta barua hapo ili aweze kwenda kuonana na hao Maafisa kutoka Uhamiaji.

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine ambalo linazungumzia huduma ambayo inatolewa ya upimaji wa afya kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi katika Kituo chetu cha Afya kilichopo hapa Bungeni, Jengo la Utawala Annex. Zoezi hili limeanza tarehe 2 na litaisha tarehe 12 Novemba, 2021 na watoaji wa huduma hili ni Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Sasa Waheshimiwa Wabunge tusikilizane vizuri hapa kuna watu ambao wanaweza kwenda pale kwa ajili ya kupata huduma kati ya hizi zinazotajwa hapa. Kwanza kuna upimaji wa magonjwa ya moyo, magonjwa ya ndani, saratani, ngozi, figo, njia ya mkojo au kibofu na uzazi na magonjwa ya wanawake.

Waheshimiwa Wabunge magonjwa haya yametajwa hapa lakini ukienda pale utapata ushauri wa mambo mengi kabisa na hii inaonesha namna ambavyo wenzetu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wanatujali Waheshimiwa Wabunge kama wawakilishi lakini twende tukapime afya zetu tuwe tunajifahamu jamani. Kwa hiyo, inasaidia sana katika namna ya kuendesha maisha yetu lakini pia kuwawakilisha walio tuchagua vizuri.

Hayo ndio matangazo yaliyoko hapa mezani tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Kamati ya Mipango.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Mipango.

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na mwongozo wa kuandaa mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mapendekezo yalisomwa jana na leo tunaanza michango ya Wabunge mbalimbali ambao mmeusikiliza Mpango na Mapendekezo ya Mpango mmesoma na sasa ni kipindi kizuri kwa Wabunge kushiriki zoezi hili kwa kuchangia mawazo yao wapi ambapo wanaona Serikali iliposema hivi, ingeboresha hapa, ingeongeza hili na ingepunguza nini.

Tutaanza na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mheshimiwa Oran Manase Njeza ajiandae.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ambaye ni Naibu Spika wetu; naomba awali ya yote kabisa nianze kwa niaba ya wananchi wa Sikunge kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan ambaye ameendelea kuenzi maana halisi ya majina yake, maana Samia maana yake ni Msikivu, Suluhu maana yake ni Mpatanishi na Hassan maana yake ni Mzuri au mtu mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana, ndio maana mwezi uliopita kwa makusudi kabisa akaamua kuwaongeza Watanzania kwenye bajeti yao, zaidi ya Shilingi

trilioni 1.3 ili zikapeleke rekodi ya maendeleo ambayo haijawahi kupatikana katika miaka ya hivi karibuni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena kwa kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango ambao Mheshimiwa Waziri aliuwasilisha kwa weledi mkubwa sana. Nimpongeze Waziri na timu yake yote kwamba, wameweza kuwasilisha kwa weledi mzuri sana Mapendekezo ya Mpango. Pia simsahau Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Daniel Sillo aliposimama kuwasilisha maoni ya Kamati aliwasilisha kwa ueledi mkubwa sana. Hongera sana Mheshimiwa Daniel Sillo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Spika Job Ndugai, siku ya Jumanne alitoa maelekezo muhimu sana kwa Serikali akiwa kwenye kiti kile pale. Akailagiza Serikali kwamba, fanyieni kazi suala la upandaji wa bei ya mbolea kwa haraka iwezekanavyo. Hiyo kweli nampongeza sana Mheshimiwa Ndugai, kwa sababu, ni jukumu ambalo ni muhimu sana kwa Serikali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni katika maeneo manne tu. Eneo la kwanza, naomba sana katika hatua hii ya mapendekezo ya Mpango naomba Serikali ikasisitize, Mpango utakaletwa na bajeti yake itakayopendekezwa, ni muhimu sana Serikali itenye bajeti maalum kwa ajili ya vitu viwili; ruzuku ya pembejeo za wakulima na hii ni kwa nchi nzima. Pili, kupanga fedha za *buffer stock* kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima pale ambapo uzalishaji utakuwa mkubwa ukazidi soko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kupendekeza katika maoni yangu, Mfuko wa Jimbo ni wa Sheria ya Mwaka 2009. Kwa sasa hivi una umri wa miaka 12, vigezo ni vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati Waziri atakapoleta Mpango azingatie vile vile, Serikali ilete marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo ili kuboresha zaidi malengo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nilikuwa naangalia upandaji wa bidhaa muhimu nchini, hasa hasa bidhaa za ujenzi na nimeona kwamba kuna tatizo ambalo Serikali inabidi iweke mkakati maalum. Afrika Kusini mwaka uliopita 2019/2020, kwa sababu ya UVIKO walifunga viwanda 2,000. Mwaka jana na mwaka huu 2020/2021, wamefunga viwanda 1,000 kwa sababu ya mambo ya *lock down*. Sasa hii imesababisha *demand* ya bidhaa zinazotengenezwa Tanzania ivuke mipaka ya nchi kwa kasi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna *demand* kubwa ya bati, kuna *demand* kubwa ya *cement*, kuna *demand* kubwa ya bidhaa za chuma ikiwemo nondo katika nchi hizo za Kusini mwa Afrika - *SADC* kwa ujumla. Kwa hiyo, lazima Serikali itengeneze utaratibu/mkakati maalum wa namna ya kukabiliana na hiyo hali ya hiyo *demand*. Matokeo yake, uzalishaji wa Tanzania sasa umekuwa ni wa *export* zaidi, kwa hiyo *demand* ya ndani ya nchi nayo imeathirika matokeo yake bei zimepanda sana. Kwa hiyo, naomba Serikali ije na mkakati maalum wa namna ya kudhibiti hali hiyo ya biashara kuanzia sasa, sio kusubiri mwakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nitatumia muda kidogo hapa, kwa miaka mingi kumekuwa na udhaifu kwenye eneo la ufuatiliaji na tathmini na ndio maana akienda Mkuu wa Mkoa, anagundua matatizo, akienda Mkuu wa Wilaya kwenye miradi, anagundua matatizo, akienda mkimbiza Mwenge wa Kitaifa, anagundua matatizo, akienda *CAG*, ndio kabisa. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kuimarisha ufuatiliaji na tathmini (*monitoring and evaluation*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana Kamati imekuwa inasisitiza mara kwa mara na Serikali imekiri Bungeni humu kwamba, upo umuhimu sasa wa Serikali kuja na sera na sheria maalum *itakayo-guide M&E* nchini. Nikisema hivi watu wengine watasema mbona sheria zipo tunazo, sawasawa ni kweli. Tuna Sheria 10 zinazo-*guide M&E* nchini na nitazitaja kwa kifupi kabisa. Sheria ya Fedha za Umma ya

mwaka 2001, inayo-guide utunzaji wa nyaraka, matumizi na ukaguzi wa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ni Sheria ya Ununuzi wa Umma *ina-guide M&E* za mikataba, kukagua miradi na utunzaji wa nyaraka; Sheria ya Tawala za Mikoa, Sheria za Serikali za Mitaa, Sheria ya *PCCB*kuhusu masuala ya kudhibiti ubadhirifu, Sheria ya Polisi - *Police Force Ordinance* kuhusu ukaguzi wa sheria zote, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sheria ya Utumishi wa Umma kuhusu *Strategic Plan* na *OPRAS*, Sheria Kuu ya Jinai (*Penal Code*) kuhusu wajibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Sheria ya Kodi ya Mapato kuhusu kufuatilia ajira, biashara na uwekezaji. Halafu kuna Sheria nne kuhusu tathmini; Sheria ya Ukaguzi wa Umma ambayo anaitumia *CAG*; kuna Sheria ya Bajeti, halafu kuna Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana za Serikali ambao kwenye *Financing Agreement* inaweza ikatoa *M&E framework*, kwa ajili ya miradi na *program* fulani fulani. Halafu ya mwisho ni Sheria ya *NBS – National Bureau of Statistics* hii Sheria nayo *in-a-guide* kuhusu *evaluation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna Sheria 14 sasa kuna hapa na pale, kuna mambo fulani fulani ambayo inaonyesha kabisa kwamba hii *M&E* haipo *streamlined*. Kwa hiyo, ombi langu, Serikali mwaka ujao itunge Sera ya *M&E* halafu vile vile, ifuatiwe na Sheria ya *M&E* ambayo sasa hiyo ndio itatumia...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kufuatilia na *ku-evaluate* mambo ya Serikali yote kwa ujumla. Ahsante sana. Kuna taarifa hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome, naomba mchangiaji ameshasema ahsante sana. Umemaliza Mheshimiwa Kakunda?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Bado hajamaliza.

MWENYEKITI: Sawa, endelea Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Kakunda kwamba, tulishaleta mapendekezo ya kuunda sera ya *monitoring and evaluation* na Serikali ilishapokea na ikasema inaenda kulifanyia kazi. Kwa hiyo, labda tuombe Serikali walete kwenye *commitment* ya Mpango huu, sera hiyo, lakini tulishawapelekea. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salome, unasema tulishaleta wewe na nani?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *tuna-Caucus Maalum* ya *Monitoring and Evaluation*, tulileta na Kamati ya Bajeti walileta lile pendektezo na walitoa Azimio la Bunge.

MWENYEKITI: Ngoja kwanza ngoja. Ukitsema tulileta, maana yake ulileta kwa Spika, la sivyo useme tulipelekea Serikali. Kama ukitsema tulileta maana yake ulileta kwa Spika, ndio maana nakuuliza wewe na nani mlileta?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho Kiswahili chako hicho hicho ndio nachukua na mimi na-*adopt*, lakini *point* yangu ni kwamba suala hili Serikali ilishalipokea na ni Azimio rasmi la Bunge. Kwa hiyo, *commitment* ya Serikali wataleta lini sera hiyo ndio nafikiri alichotaka kukitsema Mheshimiwa Kakunda. (*Makofi/ Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakunda unaipokea taarifa hiyo?

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge Wakereketwa wa ufuatiliaji na tathmini na naipokea taarifa ya Mheshimiwa

ya Salome Makamba. Ndio maana mimi sikutaka kuisema hiyo, kwa sababu, ile ilipelekwa katika utaratibu ambao sio wa Bunge kwa maana kwamba, Kamati yetu sisi ya Wakereketwa mambo yetu humu Bungeni yanaletwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yalishaletwa humu na Waziri mwaka jana alisema kwamba suala hilo ni muhimu. Kwa hiyo, kama Serikali ilishakiri kwamba suala hilo ni muhimu ndio maana tunasisitiza kwamba, kwenye Mpango ujao walete sasa mchakato maalum ambao utatunga Sera ya *M&E* halafu itahitimishwa na utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie mchango wangu sasa kwamba lengo la pendekizo hili sio kuzifuta Sheria zile 14 nilizotaja, hapana. Lengo ni kunyoosha utaratibu wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini katika nchi yetu, illi uwe wa Kimataifa na kuhakikisha kwamba tunapunguza *observations* zile ambazo *CAG* ndio huwa anasubiri akienda anazikuta au mkimbiza mwenge akienda anazikuta, au Mkuu wa Mkoo akienda anazikuta, au Waziri au Waziri Mkuu au Rais akienda anazikuta yapunguzwe hayo kwa kufuatilia. Kuna maeneo 35 ya kufuatilia kwenye mchakato wote wa mradi. Maeneo hayo yakifuatilia vizuri, hizo *observations* za *CAG* na Wakaguzi wengine zitapungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kakunda. Mheshimiwa Dkt. Charles Steven Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, ajiandae.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Nikupongeze kwa namna ambayo unaendesha Bunge hili kwa weledi. Pia nijiunge na wenzangu kutoa pongezi na shukurani nydingi, kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa jinsi ambavyo anaendeleza kazi hii kwa kasi na kusema kweli anatekeleza kwa mafanikio. Sio mafanikio tu,

Iakini huku akizingatia kile ambacho watu wengi wanakisahau; Katiba, Sheria, Sera na Kanuni. Jambo hili limeanza kuvutia sana wawekezaji kutoka nje na hapa ndani na watu kujisikia wako nyumbani. Naamini hiki kitachangia sana katika ukuaji wa pato letu katika miaka inayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake yote kwa yote ambayo walifanya. Wameleta mapendekezo ya Mpango ambayo yanakubalika. Nimpongeze pia Mheshimiwa Daniel Silo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, kwa namna ambavyo aliwasilisha ushauri na maelekezo fulani fulani ambayo, yametoka kwenye Kamati yake kuhusiana na mapendekezo haya ya Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajikita kwenye lile ambalo nataka nizungumzie zaidi ambalo ni la mambo ya sera ya fedha, niseme kwamba licha ya mipango mingi na mikakati mingi ambayo inatekelezwa kwa sasa hivi, ikiwepo ile ambayo inaendana na mpango wa kupambana na athari za *COVID-19*. Utaona kwamba bado Mpango huu umekuja na maoteo ya ongezeko la pato la Taifa ambalo nafikiri ni chini sana asilimia 5.2. Ni ongezeko kidogo sana ukizingatia kwamba mambo mengi yanatokea na yanatokea kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hivyo, naamini kwamba, sisi hatutoki kwenye uchumi ambao ulikuwa kwa hasi, uchumi wetu umekuja chanya, kwa hiyo tuna kila sababu ya kutegemea kwamba, kile kinachotokea kwenye *ground* na ukweli ni kwamba maoteo ya ukuaji wa chumi zilizoendelea ni asilimia sita kwa mwaka 2020/2021 na mwaka unaokuja unaoteara wakue kwa asilimia 4.9, yote hii itachochaea ukuaji wa uchumi wetu. Kwa hiyo, ni lazima pengine tuangalie vizuri kwamba tusiwe-*conservative* sana bali, tujaribu kuangalia ni namna gani tutachukua hatua na nafikiri kwamba, hatua zitakazochukuliwa zilete matokeo ni hizi ambazo nazungumza sasa hivi ndio hizo zitawenza na ndio kitu kimekuwa kikwazo kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba ukuaji wa pato la Taifa unatokana zaidi na sekta zile ambazo zinanufaika na uwekezaji wa Serikali. Miundombinu, ujenzi ndio utaona hizo sekta ndio zinanufaika na zinakua kwa kasi mpaka asilimia 13 mpaka 14, lakini sekta nyingine hizi za watu binafsi binafsi za kilimo na kadhalika, zinakua kwa kiwango ambacho naamini bado kiko chini. Ukuaji huu mdogo kwenye sekta hizi naamini unatokana zaidi na kile ambacho hakijafikiwa licha ya kwamba tuna uchumi ambao tunasema ni uchumi tulivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi tulivu maana yake ni uchumi ambao *una-low inflation* (mfumuko mdogo wa bei). Hata hivyo, utakuta kwamba, mahitaji kwa uchumi kukua kwa kasi sio tu kwamba uwe na mfumuko mdogo wa bei, wanasesma *necessary but not sufficient conditions* ziko tatu. Moja ni hiyo mfumuko wa bei mdogo; lakini huu mfumuko wa bei mdogo lazima uweze kutupelekea kupata riba zilizo chini. Cha kwanza, riba ziwe chini na tulivu na maana ya riba kuwa chini na tulivu ni riba ziwe chini kwa maana ya kwenye tarakimu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwamba, thamani ya sarafu yetu iwe nayo tulivu; *exchange rate stability*. Kwa hiyo, *the three ni necessary but not sufficient conditions za rating growth*. Sasa niseme hivi, tutaona kwamba uchumi wetu kwa miaka mingi umekuwa na *inflation* ambayo ni chini ya asilimia 10. Imekua kwenye zaidi ya miaka 10 iliyopita, tuna *inflation* ambayo iko kati ya tatu sasa na sita au saba, lakini utakuta kwamba bahati mbaya licha ya kuwa na hiyo, bado kuna matatizo ya sera ya fedha haijaweza kutuletea riba ambazo ziko chini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ni kwamba tujiulize ni kwa nini sera hizo haziji chini? Benki Kuu imefanya mambo mazuri, imeweza kupunguza ile riba ambayo wanatoza mabenki wanakwenda kukopa kwao. Imepunguza fedha ambayo mabenki wanalazimika kuweka kwenye Benki Kuu ambayo haipati riba. Zote hizi zimejaza mabenki ukwasi wa kutosha. Hata hivyo, bahati mbaya hatua hizi zilizochukuliwa

siku za karibuni zimesaidia yale mabenki kutengeneza faida kubwa kwa manufaa ya wana hisa wao tu, hazijaenda kwa walengwa, yaani hizi hatua zimguse yule mzalishaji wa sekta binafsi ambaye ili yeze aweze kuongeza uzalishaji au awekeze kwenye uzalishaji mpya, ni lazima apate mkopo ambao ni *acceptable* kwa riba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo haijatokea. Nafikiria kwamba, siku itakapotokea kwamba riba zishuke ziwe kwenye tarakimu moja, ndio utaanza kuona kwamba mahitaji ya mikopo yataanza kuongezeka. Kwa sababu, unajua kwamba unaenda kuzalisha, lakini huhatarishi ile dhamana yako, hawaji kuiuza kwa sababu utaweza kulipa ule mkopo na *u-service*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa hizi riba za asilimia 16 mkopo unaji-*multiply* mara mbili baada ya miaka mitano. Hebu niambie ni kitu gani duniani hapa utawekeza halafu *kiji-multiply* mara mbili kwa miaka mitano. Hata nyumba yako wewe mwenyewe miaka 20, 30 ndio unarudisha fedha yako. Kwa hiyo, nasema hiyo haitawezekana mpaka wafanye hivyo. Sasa napenda kutoa hoja kwamba, kitu kinachopelekea mabenki wasishushe riba sio kana kwamba hawana ukwasi, ni kwamba kuna riba ambayo ni *bench mark*, kigezo ambacho wao ndio wanaangalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika wao wanaangalia kwamba kwenye soko la dhamana za Serikali, je, riba inayopatikana pale ni kiasi gani? Wakishapata pale wanasema *ok*, hii ni *risk free rate* kwa hiyo ile ndio kigezo chetu. Hatuwezi kushuka chini na ukweli ni kwamba fedha hizi zilizopatikana zote kwenye huu mlegezo uliotolewa na Benki Kuu, nydingi zimekwenda kwenye dhamana za Serikali, hazikwenda kwenye sekta binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme hivi, ukweli ni kwamba hata deni la Taifa linachochewa zaidi na riba hizi za dhamana za Serikali za muda mrefu ambazo ni asilimia 15, 16. Kwa hiyo, tunaposema deni la Taifa tatizo sio tu

kwamba eti wanakopa sana, hapana. *Rate service burden* inakuwa kubwa kwa sababu riba hizo ziko hivyo. Ukiangalia miaka ya nyuma riba kwa dhamana za Serikali hazikuwa hivi. Kwa hiyo, nasema ule mfumo wa *ku-auction* dhamana za Taifa, *una-auction* kwa kutaja bei, kwamba, nauza dhamana za bilioni 400 kwa asilimia 16 nani atashusha bei? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni soko au *una-dictate*? Nakuapia hazitakaa zishuke hizo riba ilimradi namna ya kuendesha hiyo minada ni hiyo hiyo. Kuna mwanaume anaitwa *Dutch Auction* natumai wajaribu kuangalia namna gani ya kufanya au waanze kushusha waseme *tuta-auction* kwa asilimia 10, tuone kama hawatanunua. Mabenki yatakimbia hata mimi nitanunua kwa sababu asilimia 10 *it is a big real interest rate*. *Real* kwa sababu ukitoa hii asilimia tatu, nne ya *inflation* bado nina *real benefit* ya *six, seven percent*.

Kwa hiyo, kuna kila haja tumwombe Waziri atekeleze kwa sababu, hiyo itasaidia kwenye kupunguza *burden* kwa kila mtu na kuanza kuona tena hali inarudi kikawaida, watu kuchukua mikopo, biashara kukua na sisi wote tukafaidi na utakuta hata kwenye kilimo watu watapata mikopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, nafikiria hilo ni la msingi na tuseme kwamba pamoja na kwamba mfumuko wa bei umetufaidisha kuhakikisha kwamba *exchange rate* bado imekuwa *stable*, lakini bado haujatufikisha pale ambapo, *that is the most critical issue* ni riba na niseme hivi nazungumza riba kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya fedha sio kitu kingine isipokuwa riba, basi ukienda nje huko duniani kwenye masoko yaliyoendelea, nenda US, nenda wapi kitu cha maana wanaangalia *bank rate*, *that is all*, mambo mengine yanaji-set yenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambiwa muda umeisha. (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, utafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, ajiandae.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie maboresho ya Mpango wetu. Kwanza nianze kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali. Katika hii ripoti, imeonesha kabisa kuwa utekelezaji wa bajeti zillizopita ullkuwa ni mzuri sana. Pia ni hivi juzi tu Mheshimiwa Rais ametupelekea zaidi ya shilingi trillioni 1.3 kwenye Halmashauri zetu. Hizo zimeleta mabadiliko makubwa sana kwa nchi yetu na hayo mabadiliko nafikiri yatakuwa endelevu kwa jinsi ninavyoyaona mambo yanakwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ya juzi, alipokuwa kwenye mkutano. Ile hotuba imeniwezesha hata mimi kujaribu kuuangalia huu Mpango vizuri zaidi, na nikagundua kuwa huu Mpango wetu umeacha kipengele ambacho ni muhimu sana. Kilimo hakijawekwa kama ni kipaombele katika huu Mpango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoongelea suala la tabia ya nchi, kilimo kinabeba kwa kiasi kikubwa hayo madhara ya tabia nchi. Dhima ya Mpango wetu tulionao ni kujenga uchumi shindani. Uchumi shindani unashindana na nani? Sasa ukiangalia huu Mpango wetu haujatuonesha kuwa huo ushindani wetu sisi tunashindana na nani? Nina imani ya kwamba sisi kama nchi, kama Tanzania, unapoengenya uchumi shindani, unajilinganisha na wengine ambao tupo

kwenye ukanda mmoja, kama *East Africa*, SADC au Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hilo kwa sababu, nchi za wenzetu, kilimo wamekipa kipaombele sana. Uzalishaji kwenye kilimo ukiangalia nchi kama wenzetu Zambia, uzalishaji wa mahindi ni magunia 30 mpaka 40 kwa eka, ukilinganisha na sisi ni magunia ambayo hayazidi 10. Sasa unaona ni kiasi gani sisi hatujajijengea kilimo kikawa ushindani kwenye ukanda wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia mapato yanayotokana na zao la kahawa kwa wenzetu Waganda. Kwa mwaka 2020, wenzetu *foreign exchange* ya kahawa wamepata dola karibu milioni 515 ambayo ni karibu shilingi trilion 1.2; wakati sisi tulichopata hakizidi shilingi milioni 135, ambayo ni asilimia 30 au theluthi tu ya ile ya wenzetu wa Uganda. Sasa ukiangalia ungetegemea wapi tupate mapato mengi ya kigeni yanayotokana na kilimo cha kahawa? Kwa imani yangu, nafikiri sisi tungepata nyingi zaidi inawezekana hata mara mbili ya hizo. Ni kwa nini wenzetu wamepata fedha nyingi hizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huhitaji hata elimu kubwa. Wanachokifanya wezetu, kwanza wamejenga ile *chain* ya uzalishaji. Kwenye *production* wamehakikisha kuwa wakulima wanapewa ruzuku (*subsidy*) kwenye mbolea na wakulima wanapewa malengo. Sasa hapa kwetu hiyo haipo. Naangalia hata kwa nchi ya Rwanda, nayo wameweke hivyo hivyo; kwenye kilimo kuna ruzuku kwenye mbolea, na wanzetu ruzuku yao ni zaidi ya nusu; asilimia mpaka 60, lakini sisi ruzuku hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitengeneza hesabu kwenye kilimo cha Watanzania, hakuna mkulima hata mmoja anayeweza kwenda na jembe shambani, kwa sababu hutakuwa na nguvu hiyo, hata kwa bei hizo zilizokuwepo. Mkulima wa kwetu, uwekezaji kwenye eka moja ya mbolea, atakachopata hata akawauzia *NFRA*, ni nusu tu ya ile gharama ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba tunapoiangalia nchi kama Tanzania ambapo tegemeo kubwa ni kilimo, *seriously* kwenye mipango yetu tuangalie kilimo tutakisaidia namna gani ili tufanye kilimo cha kisasa, na huku ndiyo kutakuwa na mabilionea ambaao Mheshimiwa Shangazi alikuwa anawaulizia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu, kwa mwaka huu hivi sasa Serikali iagangalie namna gani itawapatia wakulima ruzuku ya mbolea na isisubiri Mpango. Leo hii kilimo kimeanza, lakini hakuna maandalizi yoyote ya kilimo. Pamoja na hali ya hewa kuwa mbaya, lakini wakulima wanaogopa kuandaa mashamba kwa sababu ya bei ya mbolea ambayo hakuna mtu atakayeweza kuimudu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu, kwa hesabu ya haraka haraka, nilikuwa naona Serikali ikitenga (sijui itazipata wapi, nina imani itazipata), kama shilingi bilioni 200 mpaka 250 zinaweza kusaidia zikaiokoa nchi yetu ili janga la njaa litakalotokana na ukame mwakani tuweze kuzalisha kwa tija. Kwa hiyo, naomba pamoja na mwendelezo wa hii ruzuku, lakini tunganezia sasa hivi na uharaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa lile agizo aliloipa Serikali. Nafikiri lile ni agizo muhimu, naiomba Serikali iangalie kwa haraka sana ni namna gani iweze kuwasaidia wakulima. Hilo tamko lisichelewe, kwa sababu kwa ukanda kama ule ninaotoka mimi, sasa hivi watu ndio wanatafuta mbolea ya kupandia, na kwa bahati mbaya hata mbolea za kukuzia leo wanaoagiza mbolea nina imani ni pungufu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipojaribu kuuliza wakasema, wazalishaji wote sasa hivi hawawezi kuzalisha kwa sababu *order zilizopo* kwenye wazalishaji nje ya nchi, labda mwezi *March* au *April next year, 2022*. Sasa hiyo inaweza kutusababishia sisi, kama tulikuwa hatujajiandaa kwa hilo, hata hiyo mbolea ambayo tunaitegemea isiwepo. Hata hizi mbolea za kupandia nazo hazipo. Sasa hii yote inatokana

na sababu kwamba katika mipango yetu kilimo hakijawekwa katika kipaumbele. Kwa hiyo, naomba Serikali katika huu Mpango, iweke kipaumbele cha kilimo ikiwezekana namba moja, ili tuweze kusaidia jamii yetu ya Watanzania ambao ni zaidi ya asilimia 60 wanaotegemea kilimo. (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mheshimiwa Jonas William Mbunda ajiandae.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Nami nijumuike na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya. Tulimwona alipokuwa kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, tumemwona alipokuwa kwenye Mkutano wa Mazingira wa Mabadiliko ya Tabianchi huko Duniani na hotuba alizozitoa ambazo kwa kweli zilikuwa na mvuto mkubwa na msisimko mkubwa. Hakika analitenda haki Taifa lake na aendelee kuchapa kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii kama ingekuwa tunafika mahali tunaweza tu kuwa kwenye mipango muda wote; na hata yale tunayoyazungumza wakati mwingine yasipate muda wa kufanyiwa kazi; tulizungumza mengi sana wakati tunapitisha bajeti ya mwaka huu. Nami naamini kama yale tuliyoyazungumza wakati huo kama kuishauri Serikali yanzezingatiwa kwenye huu Mpango tuliosasilishiwa, leo hii tusingekee na maneno mengi hivi ya kusema. Hayo tuliyoyazungumza na ushauri wote tuliousema, hatuyaoni kwenye Mpango, sasa tutashauri mpaka lini ili tuweze kusikilizwa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri mengi sana kuhusu ajira za vijana wetu, zinapatikanaje? Tulishauri mengi sana kuhusu sekta binafsi, kuhusu mapato ya Serikali na kuhusu kuumaliza umasikini Tanzania. Vile vile ukipitia Mpango huoni ni wapi sasa ambapo maoni yetu yamezingatiwa. Nami nianze moja kwa moja na hili eneo la ugharamiaji wa Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Hotuba ya Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti uliowasilishwa na Waziri, sehemu kubwa inazungumzia tu matumizi, lakini ni namna gani haya mapato tutayapata kwa ajili ya kugharamia Mpango wenyewe? Huoni wapi yameelezwa. Unaona jitihada tu zilizozungumzwa, tutahamasisha matumizi ya Tehama, tutahamasisha hiki, tutahamasisha hiki. Ni mambo ambayo yamekuwa yakirudiwa kila mwaka na ni ya ku-copy na ku-paste.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo changamoto kubwa sana kwenye ukusanyaji wa mapato ambazo zingeweza kufanyiwa utaratibu na tukatoka hapa tulipo. Kwa mfano, hivi ni utafiti gani tunaoufanya? Kila mwaka huwa tunafanya utafiti kweli?

Kwa nini huu Mpango usituambie tunafanya utafiti gani kufikia ukusanyaji wa mapato yetu? Vyando vyetu vyaa mapato tunavifanyia utafiti? Hao *TRA* wanapofanya ukusanyaji wa mapato, tunawachunguza namna gani uwezo wao wa kuweza kukusanya mapato yetu na tunachukua hatua gani? Sasa unakuta mwisho wa siku mnaingia kwenye bajeti mnasema tu, hili limesamehewa, hiki kimetozwa, hii tozo tumeongeza; na mfano upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2020 hapa kwa sababu ya sisi wenyewe kutokuwa na utafiti wa kutosha katika mapato yetu, tumekuwa tukiingia kwenye mgogoro mkubwa sana. Tumeingia kwenye mgogoro mkubwa kwenye tozo za simu. Tumebishana hapa, tukatoka tulivyotoka, tumefika mahali tumerekebisha wenyewe viwango vyaa tozo vyaa miamala ya simu vilivyokuwa vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda na *withholding tax* tukawaambia watu kwamba tunataka kuweka *withholding tax* kwenye mazao ya 2%, halafu tukaenda kusamehe wanywa bia kwamba wasilipe kodi ili zao la shayiri liweze kuzaishwa. Wakati huo unamsamehe mywa bia ili kilimo kiongezeke, halafu unaenda kumtoza anayelima shayiri yenye. Sasa unaenda kutoza *withholding tax* 2% huku ukijua kuna *Service Levy* 3%. Huyo mkulima atalimaje? Matokeo yake najua, watakuja kufanya marekebisho hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda kwenye mafuta, nako hivyo hivyo, tulisema yanaweza kua-*attract inflation*, hata kama tuna nia hiyo njema, Serikali imefanya marekebisho katikati ya safari. Hii yote ni uthibitisho kwamba tunaibuka na mabadiliko ya kodi bila ya kufanya utafiri wowote. Kwa nini hatufanyi utafiti? Kwa nini hatuwekezi? Kwa nini suala hili la mapato limekuwa la siri siri tu, halafu linakuja kuibuka hivi, hakuna mafanikio ambayo tunaweza kufika nayo popote? Hata hivyo Mpango hauzungumzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema hapa Wabunge, tunazo shilingi triliioni 360 zimeshikiliwa na Mahakama, uamuzi haujatoka. Nilitegemea kwenye Mpango hapa isemwe kwamba hizo shilingi triliioni zetu 360 ziko wapi? Leo hapa Bunge zima linapiga makofi kwa shilingi triliioni 1.3 tulizopewa na IMF. Fedha ndogo shilingi triliioni 1.3 tunapiga makofi mpaka mikono inauma; na kwa kweli tunashukuru kwa hilo, lakini tuna shilingi bilioni 360 za kwetu, hata kama ni asilimia 10 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 10 ya shilingi triliioni 360 ni shilingi triliioni 3.6. Bado hilo kwetu halijatuma, Bunge halijaumia, Serikali haijaumia. Fedha zimeshikiliwa tu kwa maamuzi tu ya Mahakama. Kama tatizo ni hizo bodi zetu za rufaa za kodi zina shida na wataalamu, si tuajiri wataalamu hata wa kutoka mpaka nje kama ni wataalamu? Ni nini kinachosababisha? Mpango haujazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *transfer pricing* nalo tulilisema. Tunayo makampuni 504 yenye miamala zaidi ya shilingi triliuni 105 kwa mwaka. Uwezo wa *TRA* kuyakagua makampuni haya ni asilimia moja. Hawana wataalamu, hawana fedha na hawawezi kukagua na hivyo hatuwezi kupata kodi katika maeneo hayo. Fedha nydingi za Watanzania zinapotea, matrillioni ya fedha. Makampuni 504 unakagua asilimia moja kwa mwaka, unapata nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote kwetu sisi, mipango yetu hatuoni kama ni shida, lakini tukiletewa hata shilingi bilioni tano hapa tunafurahi kweli kweli, lakini fedha zetu zimeshikiliwa na watu, hatupati hasira katika hili. Nilitegemea hata mikataba mibovu ya akina *SICPA* na *TRA* ingezungumzwa humu kwamba tunaenda kuifuta mara moja. Mikataba ya kinyonyaji ambayo inanyonya fedha za Watanzania tungeweza kuifuta tukapata mapato mengi tu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye *TR*, anasimamia Mashirika ya Umma 237, makampuni haya yamekuwa mzigo mkubwa kwa Serikali, yanategemea ruzuku kutoka kwa Serikalini. Tumeshindwa kuyawezesha kuyapa fedha, hayana mtaji, yapo tu, hayatekelezi majukumu yake sawa sawa. Kwa nini Mpango hauzungumzi juu ya Mashirika yetu ya Umma, kuyapatia mtaji yaweze kufanya biashara tuweze kupata gawio kubwa la Serikali na hela tunazozipeleka kwa ajili ya ruzuku zifanye mambo mengine? Ila kwetu sisi tunaona hii ni sawa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu *TR* leo, Msajili wetu wa Hazina ana uwezo wa kuyasimamia makampuni haya kwa asilimia 13 tu. Hana fedha, hana wataalamu, lakini kwetu sisi tunaona kukaa na kupanga tu ni sawa, lakini upembuzi wa matatizo haya yanayotukabili hatuyafanyii kazi. Tatizo letu lipo wapi?

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

TAARIFA

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwa mchango wake mzuri kwamba, ni kweli Serikali mbali ya kutoa ruzuku, inashindwa kutoa mtaji kwa mashirika yake ili yaweze kufanya vizuri. Mfano Shirika la *TTCL*, linahitaji mtaji wa shilingi bilion 300 ili liweze ku-compete na *Voda* na *Airtel*, lakini mpaka sasa hivi wameshindwa na shirika haliko kwenye hali nzuri kama ilivyo mwanzo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, unapokea taarifa hiyo?

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea sana taarifa ya dada yangu na ninamkubali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna maeneo mengi, kuna utoroshaji mkubwa tu wa fedha, utoroshaji mkubwa sana. Ukienda mipakani mle madini yetu bado yanatoroshwa, mazao yetu ya uvuvi bado yanatoroshwa, mifugo yetu bado inatoroshwa, misitu na hata wanyamapori bado wanatoroshwa. Mpango unatueleza nini? Unaenda kudhibiti namna gani maeneo haya ili tuweze kupata mapato? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuangalia hapa sasa hivi, tunazungumza kwenye Mpango huu, kwa mwaka unaokuja wa fedha, mapato yetu tunayotegemea kuongezeka ni shilingi trillioni 1.16 peke yake. Ila ukiangalia hiyo shilingi trillioni 1.1 wanaipata wapi? Hilo ongezeko wanalipata wapi? Wanaserma mapato yataongezeka kwa asilimia 7.6, lakini 7.6 wameipataje wakati uchumi utakua kwa 5.2%, mfumuko wa bei utaifikia kwenye 4%, tayari ni 9.2%, bado kuna kuongezeka kwa tozo, tunakuja na kodi mpya ambayo ni walau 1%, tunapata 10.2%, bado kuna uthibiti wa upotevu

wa mapato kama huu atunaouzungumza. Kukishaweka mikakati kama hiyo, nayo kuna asilimia kama moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaweza ukakuta mapato yetu yakaweza kukua hata kwa 12%, kama tungekuwa tunafanya utafiti wa kutosha kuhusu mapato yetu; lakini hapa tunafika tu tunasema mapato yataongezeka kwa shilingi trilioni 1.2, halafu yanatokana na nini? Kwa hiyo, wakusanyaji nao wanaenda kiuzembe kukusanya, wanashindwa hata kushughulikia fedha hizi ambazo zipo, ni za kuchukua tu kwa sababu sisi Bunge tumewaidhinishia makadirio madogo. Sasa tutabaki hapa mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu ushiriki wa sekta binafsi. Hatuwezi kukua kama ushiriki wa sekta binafsi tunaenda nao namna hii na kama sekta binafsi itaendelea kudhulumiwa namna hii. Sekta binafasi, kwa mfano taarifa zetu za madeni, watu wa sekta binafasi walikuwa wanatudai shilingi trilioni 3.8 tulipoanza uhakiki mwaka 2015/2016, lakini ikaja kugundulika kwamba shilingi trilioni 1.16 ni malipo ambayo siyo halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu ushiriki wa sekta binafsi. Hatuwezi kukua kama ushiriki wa sekta binafsi tunaenda nao namna hii, kama sekta binafsi itaendelea kudhulumiwa namna hii. Sekta binafsi ambapo kwa mfano taarifa zetu za madeni, watu wa sekta binafsi walikuwa wanatudai trilioni 3.8 tulipoanza uhakiki mwaka 2015/2016, ikaja kugundulika kwamba trillions 1.16 ni malipo ambayo siyo halali. Kwa hiyo, karibia asilimia 30 ya malipo hayo siyo halali. Inayosema siyo halali ni Serikali siyo wananchi waliokopwa. Hii ni dhuluma kwa sababu wewe unakuja kuhakiki huku deni langu nilishakupa *service*, ukapata *service* hiyo halafu unakuja kusema hili deni asilimia 30 walioingia madeni hao ni akina nani, waliruhusiwa na nani na wamechukuliwa hatua gani waliodanganya hilo? Mnaenda kuwaadhibu hawa wananchi ambaa ni haki yao, kumdhulumu mtu kwa fedha au kwa mali ulioichukua ni sawasawa na ujambazi mwingine tu. Kwanini, Serikali ijihusishe kwenye ujambazi wa namna hiyo? (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mpina. Nilikuwa nimekuacha umalizie hoja yako, kengele ya pili imeshagonga. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mheshimiwa Juma Hamad Omar ajiandae.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia uzima na mimi kuweza kuchangia mpango siku ya leo. Niwapongeze Kamati kwa kazi kubwa ambayo wameifanya Kamati ya Bajeti, wamefanya kazi kubwa sana kwa uzalendo kwa ajili ya Taifa letu, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na matumizi bora ya rasilimali za nchi tulizonazo, nitaanza na Ziwa Viktoria na Ziwa Tanganyika. Maziwa yote mawili tuna-sharezaidi ya nchi moja. Pamoja na kwamba ndani ya ziwa kuna vitu vingi ikiwemo maji, ikiwemo samaki, dagaa na vitu vingine vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na mfano wa Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika pamoja na kwamba leo kwenye mpango tunazungumzia upatikanaji wa maji mjini malengo ambayo hayajafikiwa toka tulipoanza kutengeneza mipango yetu, lakini kwenye mpango nilitegemea kuona ni namna gani Serikali imejipanga kutumia maji hayo tuliyonayo kwenda kutatua changamoto za maji kwenye Taifa letu, sijaona kwenye mpango, mmezungumza kidogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo fedha inatumika vibaya ni maeneo ambayo watu wanakwenda kwa ajili ya kufanya *surveyya* kutafuta maji. Zinatumika fedha nyingi wanaacha mashimo tu kule, lakini kuna vyanzo vya uhakika ambavyo ni Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Hatujaona mpango ukionesha hasa kwamba wamewekeza fedha kule ili kufikia malengo ya kupunguza changamoto ya maji Vijijini na Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha suala la maji tu kuna suala la uvuvi, kama wanaweza wakatumia Congo, Zambia, Burundi, tunapozungumza namna ya kuongeza Pato la Taifa ni lazima tuwawezeshe wavuvi wetu waweze kuvua kisasa, pamoja na kuwawezesha, lakini bado lazima tuondoe sheria kandamizi zinazowakandamiza wavuvi wetu

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea tunapozungumza kuongezeka kwa pato tutengeneze mazingira rafiki ya watu ambao wanatakiwa kuongeza Pato la Taifa. Leo pamoja na kwamba nia njema ya Serikali ya kuondoa uvuvi unaoitwa uvuvi haramu, tukachoma vile vifaa lakini lengo ni kuongeza pato, tukawachomea vile vifaa walivyokuwa navyo ambavyo walikuwa wanaongeza pato kupidia hivyo vifaa vinavyoitwa haramu lakini tukawaacha bila hivyo vifaa, mkumbuke wale samaki na dagaa hawajui kwamba hapa ni Tanzania au hapa ni Congo. Kwa hiyo, badala ya kuwasaidia wavuvi tumewatia umaskini. Nilitegemea kwenye mpango tuseme tumejipanga namna gani kwenda kuwaondoa wale wavuvi ambao waliondolewa vile vifaa ambavyo vilikuwa vinaitwa haramu, kuwapa vifaa halali ambavyo ni vya kisasa ili tukaingie kwenye *competition* na nchi hizo nyingine ambazo tuna-share Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwenye mpango huu kwa kuwa tunajua kuna fedha zinapatikana kwenye uvuvi, tutafute namna bora, kwanza zikiwemo meli za kisasa kwa kuwa tunashindana, tuko kwenye ushindani. Lazima tutengeneze mazingira rafiki tukiamini kwamba kweli malengo ambayo tunatarajia tumeonesha kwa mifano kuwasaidia wavuvi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya ziwa ukiangalia Ziwa Tanganyika ukiacha maji na uvuvi kuna suala la mafuta. Kwenye Mpango hapa nilitegemea nione mmejipanga namna gani kuvuna yale mafuta ya Ziwa Tanganyika ambayo yangesaidia kuongeza Pato la Taifa letu. Tumezungumza kidogo tu na kuna mambo ambayo hatuwezi kuwa na vyanzo vilevile. Kuna rasilimali ambazo tunazo lakini hatujazitumia kama inavyotakiwa. Mungu ametujaalia

maziwa kama hayo yapo, lakini hakuna mipango ambayo inaonesha kweli namna gani tumejipanga kutumia rasilimali hizo kuweza kusaidia Taifa letu ikiwemo suala la Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Nimezungumza mara nyngi na leo nitaendelea kusema bado hatujatumia inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndani ya hayo maziwa mawili bado kuna suala la mipaka. Wavuvi wanapoingia ili wakachukue mazao yao yaliyopo mle ndani kwa maana ya samaki, wanaambiwa kuna sehemu ambazo ni za hifadhi. Ukiangalia kwenye mpango hakuna sehemu wamesema wanaweka kiasi gani kwenda kuweka mipaka kwa kuwa hakuna alama yoyote inayoonesha kwamba hapa ni mpaka. Lakini, toka wameanza kusema hayo maeneo ni hifadhi, hatujawahi kuambiwa kwenye hifadhi hiyo, hao samaki wamefika wangapi zaidi ya wananchi kukamatwa na kupewa adhabu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwenye jambo jingine kwa sababu ya muda kuhusu matumizi bora ya ardhi, kabla sijafika huko, tunatambua nia njema ya wale Mawaziri, Tume iliyoundwa kwenda huko kupitia mipaka. Kuna maeneo ambayo leo kwa sababu kwenye mpango hapa Mheshimiwa Waziri ametuambia idadi ya watu inavyoongezeka na kwa neema ya pekee wanawake wanaongezeka kwa asilimia 51 alivyotusomea hapa, lakini ukiangalia kama idadi inaongezeka tulitegemea kwenye mpango watuambie kwa sababu ardhi iko pale pale na idadi ya watu inaongezeka kuwe na Mpango maalum kwa ajili ya kuongeza maeneo ya uzalishaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo yamewekwa hayana faida yoyote, hakuna hata mdudu unaweza ukatembea mchana, asubuhi ukakutana nae lakini wananchi wangeozewa hayo maeneo wangeongeza uzalishaji. Kwa hiyo, kuna haja ya Serikali kuwa na mpango maalum wa kupitia angalau kila mwaka kuangalia maeneo ambayo hayana sababu ya kuwa pori tengefu warudishiwe wananchi ili waendelee kuzalisha na waongeze Pato la Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza kuna maeneo ambayo yamekuwa na migogoro mara nyingi, hifadhi na wananchi. Pamoja na kuwa hifadhi, lazima tujue hivi wanyama wale wako wangapi, wanaingiza kiasi gani na kama tungeweza kuwapa wananchi wangeingiza kiasi gani kwenye Pato la Taifa. Leo hatuwezi tukawa tunazungumzia mipango ambayo tunathamini pekee wanyama halafu tukaacha wananchi na tunajua kweli idadi inaongezeka na aridhi iko pale pale. Kama kweli tunategemea matokeo chanya ni lazima tuwe na utaratibu maalum wa kuongeza maeneo kwa ajili ya uzalishaji wa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye matumizi bora ya ardhi, hapo lazima tuzungumze tumepima eneo kiasi gani kwa ajili ya kilimo. Tumezungumza kwamba hapa inasaidia Pato la Taifa asilimia 26 lakini tulitegemea kwenye mpango hapa mtuambie mmetenga kiasi gani kwa ajili ya kwenda kuongeza kwenye Vyuo vya Utafiti, hatujaona hapa! Kwa hiyo, hakuna suala lolote ambalo linaonesha kilimo ni kipaumbele. Ni lazima tuone kwenye mpango hapa kwa sababu huwezi kuboresha kilimo wakati hujaweka fedha kwenye utafiti. Lazima tutafiti tujue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimaliza kwenye utafiti ni lazima fedha itengwe kwa ajili ya kupima udongo. Leo mnatuambia kuna mazao ambayo soko lake ni gumu lakini mnapokuja na mazao mbadala lazima ardhi iwe imepimwa kwamba udongo huu unafaa kwa ajili ya zao hili. Kama hatujapeleka fedha kwa ajili ya kupima udongo hakuna kilimo hapo na lazima mjue kwamba hivi tunaposema kilimo tunazungumza kitu gani. Kuna suala la kupima udongo, kuna suala la pembejeo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru tu kwamba kuna fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya kujenga madarasa, ni jambo jema sana, mionganoni mwa maeneo ambayo watu wake wameathirika ni pamoja na wakulima wa nchi hii kwa sababu nchi ambazo zilikuwa zinazalisha mbolea na wao walikumbwa na janga hili kwa hiyo, bei imekuwa kubwa ya mbolea. Tulitegemea kipaumbele cha kwanza mngepeleka

kuweka ruzuku kwenye pembejeo ili Watanzania na wao waone! Mheshimiwa Waziri huwezi kumpeleka mtoto darasani wakati hajala, lazima ale chakula ashibe ndiyo aende huko darasani. Kwa hiyo, tunategemea kwenye mpango hapa mtuambia mpango wa Serikali pamoja na *slogan* ya Awamu ya Tano ya Serikali ya Viwanda, lakini viwanda vingekuwepo hapa vingezalisha mbolea. Mbolea ingezalishwa Tanzania bei ingekuwa nafuu na ingeweza kumsaidia mkulima wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira yote haya tunaomba busara ile iliyotumika kwenda kwenye madarasa ni jambo jema na mimi nakubali lakini turudi kwa hawa wakulima ambao hiyo asilimia 26 nikueleze tu ni wakulima wa mkono na kama nia ni njema ya kwenda kumsaidia mtu huyu ni lazima tuoneshe hiyo nia njema ya kumsaidia mkulima wa kawalda kabisa. Ruzuku ni lazima na mimi ni semetu, Serikali iliyopewa dhamana ni lazima muangalie namna ya kuwasaidia hawa wakulima. Hii siyo *favor*, lazima tujue kwamba tuna dhamana ya kuwasaidia wakulima wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujue athari ya hili jambo, huu ni mwezi Novemba na kama ni Novemba, wakulima wa Nyanda za Juu Kusini zaidi ya Mikoa Saba huu ndiyo mwezi wa kupanda, mbolea haipo! Tutakuja kuingia gharama mara mbili ya kuagiza mazao nje ya nchi badala ya leo kuweka ruzuku kwenye mbolea iweze kuwasaidia Watanzania. Lazima tuchukulie jambo hili kwamba ni jambo muhimu sana na lazima tuone kwamba Watanzania hawa ambaeo leo tunaamini zaidi ya asilimia 60 tunawapeleka wapi. Wakati nazungumzia hiyo mbolea lazima mjue pia kuna *competition* ya masoko hao wenzetu na wao hawajalala. Hawa majirani zetu Zambia mfuko wa mbolea ni 65,000 wao wanatoa wapi? Tanzania tunasubiri nini? Lazima tuone yale mambo mazuri ambayo wenzetu wanafanya siyo vibaya kuiga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Jonas William Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mheshimiwa Tabasamu Hamis Mwagao ajandae.

MHE. JONAS W. MBUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango ulioletwa mbele yetu. Vilevile naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza kwa kutoa bilioni 50 kwa ajili ya kunusuru soko la mahindi kwa wakulima wetu, limesaidia sana ingawa wakulima wale bado wanahitaji soko la kuuzia mahindi yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza kwa kutoa shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo itasaidia kuongeza sana uhitaji na kuboresha maisha ya wananchi katika maeneo yetu. Naomba naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Sillo kwa kuwasilisha taarifa nzuri pia niwapongeze wanakamati wenzangu kwa kuchambua hii taarifa na kuileta mbele ya Kamati yako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuandaa taarifa pamoja na timu yake yote ya Wizara ya Fedha na Mipango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kuchangia *draft* ya mpango ulioletwa mbele yetu kwa ajili ya kujadili na kutoa maoni, kabla sijaanza kuchangia naomba nitoe masikitiko niliyonayo kwamba tunajadili mambo mengi, tumekaa karibu miezi minne kujadii bajeti ambayo iliisha tarehe 30 mwezi wa Sita lakini kulikuwana mipango mingi sana ambayo tulipanga na kujadili ukifanya tathmini ya utekelezaji wa kipindi cha robo mwaka katika taarifa ambayo tumeletewa sasa hivi ukurasa wa 16 kwenye utekelezaji wa robo mwaka ya bajeti inaonesha kwamba kwenye utekelezaji, bajeti ya maendeleo ya mwaka 2021/22 hakuna

fedha zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo kwenye upande wa kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *slogan* yetu tunasema kwamba kilimo ni uti wa mgongo kwa Watanzania. Sasa unajiuliza kilimo cha Tanzania sehemu kubwa tunalima kwa kipindi kwamba tunategema mvua na ni sehemu chache sana ambazo anafanya umwagilaji. Sasa unajiuliza sasa hivi ni mwezi wa 11 na wananchi wanajiandaa kuingia kwenye kilimo hawana mbolea ya kupandia, hawana mipango yoyote wakati huo tunategemea kwamba ni kilimo ni uti wa mgongo katika uchumi wetu. Sasa najiuliza huu uti wa mgongo utakuwa ni uti wa mgongo salama au hauna msaada katika maisha yetu Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo vilevile tumepata changamoto kubwa sana huko nyuma sasa nilitaka nione, kwa mfano nimepitia mpango ukiangalia kuna changamoto ambayo ilijitezea inayohusiana na sumukuvu. Mpango wa Serikali na mikakati ni kujenga maghala na kuhakikisha kwamba tunaondoa hili tatizo la sumukuvu lakini kumbe sumukuvu inatakiwa katika mpango wetu tuangalie uwezekano wa kusaidia kuanzia kwa wazalishaji ili ku-*trace* ile sumukuvu ni sehemu gani ambayo unatakiwa uisimamie. Kwa sababu ninachofahamu kwa uzoefu wangu sumukuvu wakati mwingine inatokana na ubichi au wakulima wanavuna mazao mabichi na kuyaweka kwenye maghala matokeo yake yanababisha sumukuvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mpango wetu naomba uboreshwe, uwekwe mkakati ambao utasaidia kuondoa sumukuvu kuanzia kwa wakulima.

Vilevile nilipopitia mpango sijaona mkakati ambao umewekwa wa dharura kuhakikisha kwamba wakulima hawa wanasaidiwa kwenye suala la pembejeo. Suala la pembejeo ni kizungumkuti. Sasa hivi hatuna taarifa yoyote ile ya mbolea na hatuna taarifa ya kwamba mbolea hizi hata kama zitapatikana zitauzwa bei gani kwa wakulima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekazo yangu ni kwamba mpango utakapokuja uboreshwe, uoneshe kwamba bei za mbolea pamoja na pembejeo zingine ziwe zimeshuka kwa kiwango kikubwa ikiwezekana iwe sawa na bei ambayo wakulima wetu walinunua mwaka jana ili iweze kuwasaidia katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa kilimo utakuta mpango wetu haujaonesha muunganiko uliopo kuanzia kwenye uzalishaji, kwenye masoko na viwanda. Kwa mfano, sasa hivi tunaweka mikakati mingi sana ya kuhamasisha uzalishaji wa michikichi lakini mpango haujaonesha kwamba sasa hii *flow* ya uzalishaji, masoko pamoja na suala la viwanda kwa ajili ya kuchakata hiyo michikichi ambayoo tunaiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize sana kwenye upande wa Serikali kuhakikisha kwamba tunawekeza kwa kiasi kikubwa sana kwenye upande wa kilimo ili kuwasaidia wakulima wetu kuondokana na mazingira magumu ambayo yapo ili kuhakikisha kwamba tunaongeza uzalishaji. Kwa hiyo, kwenye hilo nategemea kwamba mpango utakapokuja kama walivyoshauri wenzangu tuhakikishe kwamba Serikali inaweka *subsidies* kwenye pembejeo pamoja na mbolea za aina mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mikakati yetu tuliweka hoja ya kuhakikisha kwamba Serikali inapima udongo. Kwenye upimaji wa udongo nilikuwa nashauri mpango uangalie uwezekano wa kuweka maabara za upimaji wa udongo kwenye kila Mkoa ili tuweze kuwasaidia hawa wananchi kuweza kupima udongo na kupata mbolea ambazo zitakwenda sambamba na udongo uliopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumeweka mikakati mingi sana na mipango mingi ya maendeleo lakini tumeangalia kwenye masuala ya maji, masuala ya kilimo, ufugaji na miundombinu mbalimbali lakini nilikuwa naomba mpango unapokuja baada ya kuboresha uangalie ni namna gani tunaweka mikakati ya kusimamia kwenye suala la

mazizngira ili kuhakikisha kwamba hii miradi yetu ambayo tunaitekeleza kwa kutumia fedha nyngi za Serikali iweze kuwa himiliwu kwa kipindi kirefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitoe mchango wangu kwenye suala la madeni. Kwenye mpango tumeonesha kwamba kuna madeni mbalimbali ambayo Serikali inadaiwa lakini nataka njikite kwenye suala la madeni ya ndani. Madeni ya ndani kuna madeni ya wafanyabiashara na kuna madeni ya wakandarasi, kuna kipindi Serikali ilikuwa inafanya uhakiki wa madeni ya wafanyabiashara ambao walisambaza mbolea na pembejeo mbalimbali kwa wakulima wetu. Takribani sasa ni zaidi ya miaka mitano wafanyabiashara wale hawajalipwa chochote, kila siku wakiuliza wanaambiwa kwamba uhakiki bado unaendelea na ninaona kwamba wale wafanyabiashara wameingia kwenye matatizo magumu na wana hali ngumu kwa sababu wana madeni mengi ya kwenye benki mbalimbali na wanashindwa kulipa yale madeni kwa sababu madeni yao bado hayajahakikiwa.

Kwa hiyo, naomba sana kwenye mpango utakaokuja uhakikishe kwamba unsimamia na unaweka mikakati ya kuhakikisha kwamba tunawalipa wale wadau mbalimbali ili kuondoa adha ambayo inawakabili. Nakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma Hamad Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu kuwa ni mmoja wa wachangiaji wa jioni ya leo. Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Spika nyote mmekuwa mkitulea vizuri sana katika Bunge hili mpaka kufikia kiasi cha kusema Mheshimiwa Spika anataka Bunge hili lifanye mageuzi katika kilimo. Nasema hilo ni jambo zuri kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wewe umekuwa mlezi wetu mkubwa sana kwa maana ya kujadili kwa mujibu wa kanuni na sheria tulizojiwekea. Siku zote huwa ninakuita *dictionary* wa kanuni kwa hiyo, nakupongezeni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Suluhu Hassan. Kwa kweli, kama kuna Rais ambaye ametu-*encourage*, ametunyanya nchi hii, yeye ni mmojawapo. Na ninasema hivi kwa sababu, bado amebaki na adhma au na dhima ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Na hivi karibuni ameonesha kwamba, kweli anajali, amefanya mambo mengi ambayo nitayataja *as I go through my speech*, kwa hiyo, kwa kweli, tunampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Mcemba mmoja katika Waziri ambao kwa kweli, nimebahatika kufanya kazi na Mawaziri wa Fedha muda mwingi sana nikiwa kama Naibu wao, lakini kama kuna Waziri wa Fedha aliyekuwa msikivu, hayuko *adamant*, yuko *dactyl* naweza ukampa mawazo na akayakubali, sisemi atakubali yote asilimia 100, lakini ni mwepesi wa kukubali yuko *dactyl* nakupongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati, Daniel Sillo, kwa kweli, ni Mwenyekiti mzuri sana. Kamati hii imeuchambua mwongozo huu wa mpango na imekuja na mapendekezo mazuri. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha utayachukua mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo nataka niseme hivi, Kamati yetu ya Bajeti, nikiwa ni mmoja katika Wajumbe, imechunguza hali ya uchumi katika kipindi *pre-covid* na katika kipindi *post-covid* na tumeona mengi sana na tumependekeza mengi. Mmoja katika wachangaiji hapa, Dkt. Kimei amesema kwamba, Sera ya Riba ambayo

inakuwa *determined* na *Bank of Tanzania* ni moja katika kigezo kikubwa cha kukuza uchumi au cha kufufua uchumi, nasema ni sawa kabisa ametueleza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijikite katika suala la ujazi wa fedha, *money in circulation* ambayo inakwenda sambamba na hii sera ya, au hii *tune* dhana ya kuchochea uchumi kwa maana ya riba aliyoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *over some time now* ujazi wa fedha umekuwa ukipungua, *money in circulation*. Na kwa tafsiri pana wale wataalam wanasema *M3* na ni kweli, ukienda mwaka 2019/2020 ujazi wa fedha ulikuwa kwa asilimia 10, lakini unakwenda mwaka 2020/2021 lengo lilikuwa asilimia 10, lakini ujazi wa fedha umekuwa kwa 7.6. Hii ni dhahiri kwamba, *money in circulation*, pesa ile inayozunguka imepungua, lakini unajuliza kwa nini? Nadhani hilo ndio la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kwamba, *private sector* ni *engine* ya uchumi, *engine* ya kuchochea uchumi. *Private sector* hawana fedha za kuzungusha na kwa nini hawana fedha, nitakuja. Lakini sababu kubwa zilizotolewa ni tatu kwa nini *money in circulation* inapungua; moja ni shughuli za uchumi hasa katika sekta ya biashara, katika sekta ya utalii na katika uwekezaji katika *private sector* zimepungua. Na kwa nini zimepungua? Nadhani nakujahapo, kuna hizo sababu tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kimsingi ni kwamba, *private sector* ambayo ndio *engine* ya kufufua uchumi haina *access* kubwa na na mikopo. Wengi hawa wanashindwa kwenda kwenye *commercial banks* wakakopa, wanashindwa kwa sababu *interest* ambazo zilikuwa zinatolewa na *commercial banks despite the fact* kwamba, *BOT* na Mama Samia hapa amefanya mambo mengi. Hawa *commercial banks* wengi hawafikiki katika kutoa. Sisi Wabunge ni mashahidi, sisi Wabunge tunajulikana *address* zetu zinajulikana, lakini tunachukua mikopo yetu *at an interest*

rate of 15%, 16%. Hawa private sector wanapewa zaidi ya hapo, nasema hilo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa ujazi wa fedha unapungua hilo ni tatizo maana ili fedha izunguke yule tajiri anataka awe na fedha nyingi na masikini basi humohumo anauza mazao yake naye atapata fedha, lakini kama haizunguki, kama fedha haizunguki tutauwa na matatizo tu. Kwa hivyo, nasema pamoja na kwamba, Mama yetu Rais ametusaidia sana, kwa mfano hivi karibuni katoa *1.1 billion* kawapa Benki Kuu ya Tanzania. Kama hiyo haitoshi, juzi katusaidia amepata *1.3 trillion* zote hizo zitatiwa ziende zikapunguze suala la ujazi wa fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nasema pamoja na mambo mazuri anayotufanyia Mheshimiwa Rais wetu, lakini bado *money in circulation* ujazi wa fedha umekuwa ni tatizo. Kwa hiyo, ninapendekeza yafuatayo, ili kukabiliana na suala hili la ujazi wa fedha:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tu-*encourage PPP (Public Private Partnership)*. Hivi tujilize tokea sheria hii ipite ya *PPP* ni miradi mingapi ambayo imefanywa kwa njia ya ubia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama sikosei ni Daraja la Kigamboni basi, Daraja la Kigamboni. Na Kigamboni pale ni *private*, lakini kwa maana ya shirika letu la hifadhi NSSF, lakini hakuna jitihada ambazo zimeelekezwa ku-*encode PPP*. Sasa hilo ni tatizo na ninadhani *PPP* katika ulimwengu huu ina *play part* kubwa, hasa katika miradi ambayo ni *capital intensive*; mradi kama wa *SGR*, mradi kama wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, mradi kama wa njia nne kutoka Kibaha mpaka Chalinze. Mradi kama ule wangepata *private sector* tukafanya *partnership* nao nadhani kwa kiasi kikubwa Serikali isingekuwa na haja ya kuwekeza fedha kama hizo kwa hiyo, nadhani hiyo ni njia moja tu-*encourage PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, *BoT*, Benki Kuu ya Tanzania, lazima pamoja na kwamba, kuna kitu Dkt. Kimei

amekitaja kinaitwa *Statutory Minimum Reserve Requirement*, pamoja na kwamba, Benki Kuu ya Tanzania imepunguza hii *Statutory Minimum Reserve Requirement*, lakini hii haisaidii. Inasaidia kuhakikisha benki zetu endapo zitapata matatizo zinaweza kurejesha fedha za watu kwa sababu benki haina fedha zake, benki inakusanya amana na kuna benki nyingi kwa mfano *Greenland Bank* kuna wakati ilifilisika kwa hivyo, Benki Kuu ikatakiwa irejeshe amana pale ikarejesha. Kwa hivyo, hii haimsaidii mtu binafsi wala haiwasaidii watu wa *private sector*, zaidi inasaidia kuhakikisha kwamba, benki zetu ziko *liquid at a given time*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu ninalopendekeza ni kwamba, lazima tukataka tusitake, *private sector* iende ikafanye kazi hasa katika miradi ile kwa *PPP* kama tulivyosema, lakini kuna kuna miradi kwa mfano, nitawapa mfano; mradi wa Mchuchuma na Liganga, mradi wa Liganga, chuma cha Liganga na makaa ya Mchuchuma. Hii miradi kama sisahau mradi wa Liganga umekuweko tokea miaka ya *1990s*, mimi niko Bungeni wakati huo, Mheshimiwa Kihauli, *If I can remember very well* alikuwa anauzungumzia mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *so far* mradi huu huwezi kuamini, *so far* mradi huu nafikiri umetumia *only* shilingi 5.7 *billion* huu ni *LNG*, Mchuchuma nafikiri umetumia kidogo zaidi...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Juma. Mda wako umekwisha.

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya. Kwa sababu muda hauniruhusu naomba kuunga mkono hoja zote hizi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kwamba, naomba nichangie mpango wa bajeti yetu ya 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuandaa jambo hili, lakini pia namshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake, lakini kuna vitu ambavyo tunaomba sisi kidogo kama Waheshimiwa Wabunge tujaribu kushauri katika jambo hili. Ni kwamba, mpango wowote utakaokuwa umeandaliwa halafu mpango ule ukawa unakinzana na ilani yetu ya uchaguzi, sisi Wabunge tunaanza kupata hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, tulizungumza hapa katika suala la sheria zetu za nishati na madini kule tuliruhusu maduka ya kuuza dhahabu. Leo maduka haya ya kuuza dhahabu yamekwenda kuzingirwa tena kwa ajili ya kuanza kudaiwa kodi kubwa ambazo hazikuweko katika sheria. Sasa leo utoroshaji wa dhahabu umeanza upya mara 20 zaidi ya ulivyokuwa mwanzo hapo. Sasa tunajiuliza nchi gani hii leo inakuwa hivi kesho inageuka hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri na Kamati ya Bajeti hebu nendeni kwenye haya masoko uya dhahabu mkaangalie matatizo waliyonayo. Mambo mengi yamebadilika sasa huku kwenye madini tunataka kuleta tabu nydingine ambayo ilikuwa haipo; hawa wanunuaji wa dhahabu kule kwa wachimbaji hawa wengi ni ma-*middle man* japo wana leseni wenye pesa zao wako kule ghuba, wako Dubai, wako Madina, wako wapi, wale ndio wenye hizi pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu analetewa bilioni tatu watu wanataka labda kilo 20, kule ndani katika kilo 20 ana faida ya shilingi laki tatu-tatu tu, kilo 20 anapata milioni sita yake na anaweza akakaa miezi mitatu hajapata ile kilo 20 anakuja kudaiwa kodi ambazo haziwezekaniki kulipika. Kwa hiyo, badala ya kuitisha pesa katika mifumo yetu ya kibenki sasa pesa zinaanza kuletwa kwenye magunia kwenye magari. Hii Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana uangalie

katika mpango huu namna gani mtakavyoweza kuweka jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la biashara ya mafuta na gesi. Katika mpango wako hatujaona hiki kitu kwa sababu, lazima tukaziangalie hizi sheria, juzi tumetoa tozo, tumefanyaje, sasa huku tukaangalie. Tuangalie sera zetu za mafuta na sheria ambazo zinaonekana kwamba, kwenye gesi tunachelewa namna gani, kuna mpango wa bomba la gesi kutoka kwa wenzetu kule MtWARA na Lindi, hii biashara sasa hivi inaonekana kama sio biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye suala la mafuta tunashukuru mpaka sasa hivi ni kwamba, Wizara ya nishati imechukua nafasi ya kutafuta mpango mpya kwa ajili ya kushusha hizi bei za mafuta. Lakini biashara ya mafuta ile iweze kuchangia katika uchumi wetu. Hili Mheshimiwa Waziri katika mpango liingizwe tuone namna gani ambavyo tunaweza tukaenda katika mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jingine suala ambalo tunalionia sisi kwamba ni matatizo ni kilimo cha pamba. Kwenye kilimo cha pamba kwenye ilani yetu tumesema tunataka kuzalisha tani milioni 10, leo mwaka unaisha tunakuja katika mpango mwingine tena wa 2022/2023 hatuoni jitihada za pamba tupate tani milioni 10. Tulikuwa tumezungumza kwenye mpango wa 2021/2025 katika ilani na katika mpango huu juzi tumeujadili, huku na kwenyewe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni kwamba, tunakuomba uangalie katika pamba. Tulisema mbegu zitazalishwa Igunga, kwenye mpango wako hapa hatujaona kiwanda kinachotengenezwa Igunga kwa ajili ya kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mbegu hakuna kwa wakulima. Mbegu zinazwa mpaka 1,500; 1,200. Juzi tumemuuliza sisi Waziri, Naibu Waziri wa Kilimo, suala la kuuza mbegu limetoka wapi? Leo mbegu imekwenda kuanza kuuzwa wakati mbegu ilikuwa inagawiwa kwa wakulima halafu badaye wanakuja kukatwa? Hii mnaanza kutengeneza vita katika sisi Wabunge tunaotoka kwenye

zao la pamba; tutapataje hiyo ajira milioni 10 kwa sababu wakulima wa pamba ni wengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na huko kwenye pamba tunapata pamba kwa ajili ya nguo, tunapata mbegu kwa ajili ya mafuta, tunapata mashudu kwa ajili ya mifugo yetu, hatukuona kwenye mpango wako. Sasa hili halikubaliki Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine Mheshimiwa Waziri katika hili suala lako la mpango ni suala la, tulikuwa tuna shirika letu sisi hapa la mbolea *TFC*, leo watu wanaanza kuzungumza tena ruzuku? Nani wa kupewa ruzuku kama sio Shirika la Mbolea? Tunatakiwa *TFC* tunayo, jambo lolote ambalo lilianzishwa na Mheshimiwa Hayati Baba yetu wa Taifa Mwalimu Nyerere, jamani, leo tunaanza kutoa ruzuku tena kwa mabepari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aah! Hii inauma sana kwa wastani. *TFC*, tunaiacha *TFC* leo tunakuja kununua mbolea, mbolea inaanza kulalamikiwa wakati hii mbolea tumeishauri sisi kwenye mpango kwamba, mbolea inunuliwe wakati ambaio sio wa *season*. Sasa leo mnakuja kuagiza mbolea kwenye *high season*, inakubalika wapi? Wakati mngeiimarisha *TFC* mkapeleka kule mtaji mkubwa katika *TFC*, kwanza mkisema ruzuku kule ndio mahali penyewe sasa; Mheshimiwa Waziri hili suala la mbolea liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ambalo nataka kuzungumza ni hili suala ambalo limekuja katika nchi yetu. Sijui tumeenda kulipata wapi, suala la ujenzi wa *Force Account*, nchi inakoelekea Mungu ndiye anayejua. Wenzetu Wakenya miaka 10 walikataa *Force Account*, leo watumishi wa Serikali badala ya kuja kufanya kazi za Serikali tunawaona kwenye mitandao, unamuona mkuu wa wilaya, mkurugenzi, anachimba misingi, eeh! Hii nchi. Mipango gani hii tunayokwendanayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakwenda wataalamu wote wanahama ofisi za Serikali wananchi wanaacha

kuhudumiwa kwenye ofisi za Serikali unakwenda kuuliza unaambiwa watu wote wako vijiji. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wewe ni mchumi, makandarasi wapo, tunao makandarasi zaidi ya elfu 60, wapeni kazi tutengeneze uchumi katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sasa hivi imekuwa ni wizi, tunakwenda kuziimarisha ofisi zetu kule, watu wanakwenda kuiba hizi pesa zinapelekwa hazina ukaguzi. Kwenye mpango wako hatujaona hapa sisi suala la CAG unakwenda kumuimarisaje CAG? Hatujaona kwenye mpango wako na ndiye anayekwenda kukagua hizi pesa hizi trillioni 1.3 subiri balaa lake utakuja kuliona. Pamoja na vitisho mnayyovitoa sasa hivi ambavyo havina meno wataendelea kuiba hizi pesa kwa sababu, walioiba hawajapelekwa kotini mpaka sasa hivi. (Makof) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuambie CAG unakwenda kuongeza idadi ya watumishi CAG kwa kiwango gani kwa sababu ofisi hiyo iko kwako? Hawa wakaguzi wetu wa ndani ndio ni sehemu ya wezi wanaoiba kule katika halmashauri, hatujaona kwenye mpango wako unakuja kusemaje kuhusiana na suala la CAG?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili mimi bado napinga huu mpango. Kauandaeni vizuri muulete. Mtuambie namna gani watakavyopelekwa kortini jhawa wat una Mahakama kule za hawa watu mnaenda kuziongezea fedha kiasi gani ili tuwe tuna uhakika na jambo hili. Lakini suala la kuwaondoa makandarasi katika nchi hii tunabakiza wachina, tunabakiza waturuki, habari yake mtakuja kuiona mbele ya safari. Ahsante sana. (Makof)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kama niliviyokuwa nimesema mwanzo, Serikali haina mpango bado, ukiacha ule mpango wa miaka mitano haina mpango. Hiki kilicholetwa hapa ni

mapendekezo ya mwongozo wa kutayarisha huo mpango. Kwa hiyo, maoni yenu Waheshimiwa Wabunge yanachukuliwa na upande wa Serikali wataenda kuyachakata huko halafu ndio waweke sasa kwenye hicho watakacholeta ambacho na sisi ndio tutakuwa tumeshirikiananao katika kukiandaa. Kwa hiyo, hiki kilicholetwa hapa ni mapendekezo ya muongozo wa mpango, mpango bado kwa hiyo, tuendelee kuwapa mawazo yetu wakayafanyie kazi.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga. Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niwe mionganini mwa Wajumbe wanaochangia Mapendekezo ya Mpango ambao unaenda kuandaliwa na Serikali. Naomba nianze kipekee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehma kwa kunijaalia afya njema ili na mimi niwe mionganini mwa hao ambao wamejaaliwa kuchangia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wajumbe waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana ambayo anafanya katika kuleta maendeleo kwa ajili ya Watanzania. Nami ni mionganini mwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, nimepata fursa ya kuchangia na kwa kiasi kikubwa sana naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake mengi ambayo tulichangia wameyapokea na katika kuja na mpango hakika hata yale ambayo yalikuwa yamesahaulika naamini wataenda kuyaingiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitachangia katika maeneo machache. Eneo la kwanza litakuwa Bandari, Reli ya TAZARA, Reli ya Kati na SGR kwa ujumla wake na muunganiko wa kiuchumi. Kamati yetu tulipata fursa ya kutembelea Bandari ya Dar es Salaam maboresho makubwa sana yamefanyika, imefanyika kazi kubwa sana ya uwekezaji ambao baada ya muda mfupi tunatarajia kama Taifa tutaanza kupata matunda yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mahojiano ambayo tulifanya na Wachumi wakasema Tanzania kama tunataka kujihakikishia uchumi wa uhakika na biashara ya bandari iweze kufanya kazi ya uhakika ni mizigo ambayo inasafirishwa kwenda Kongo ya DRC na wala siyo Zambia na wala siyo Uganda, *effort* ambazo zinatumia kutafuta mzigzo wa kwenda Uganda nusu yake inatosha kuweza ku-explore na kupata mzigzo mkubwa wa kwenda Kongo DRC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi kubwa nzuri sana ambayo inafanywa katika ujenzi wa reli *Standard Gauge* kwa maana ya *SGR*. Ni matumaini yetu sisi Watanzania kwamba reli hii hatujengi kwa ajili ya kusafirisha abiria, siamini hilo. Ili reli hii iwe na manufaa makubwa ni pale ambapo tutasafirisha shehena kubwa ya mzigzo na mzigzo ambao tunatarajia kupata kwenda bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilimsikia Mheshimiwa Naibu Waziri akiongelea habari ya Reli ya *TAZARA* na ubovu wake na manufaa ambayo tunategemea kupata kama nchi. Naomba niileze Serikali na hili waliandike, kama tunatarajia kwamba mkataba huu utarekebishwa eti na Wazambia wana *interestjuu* ya ufanyaji kazi bora wa *TAZARA* tunapoteza wakati na hili wanalifanya kwa makusudi. Naomba niikumbushe Serikali, hivi karibuni kuna malori karibu 300 ya Watanzania ambayo yalizuiliwa Zambia takribani mwezi mmoja mpaka miezi mitatu, hii wanafanya kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niikumbushe Serikali ili katika mipango yao waweze kuweka mambo haya; mwaka juzi tulipata soko kama nchi wakati tulizalisha mahindi mengi sana kupeleka Kongo, lakini tulishindwa kupeleka kwa sababu ya kodi ambazo ziliwekwa na Wazambia, ikaonekana kwamba huwezi ukatoa gunia la mahindi Rukwa ukalifikisha Kongo likakulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najenga hoja hiyo, naomba niwaambie Serikali, ukitaka kufanya biashara ya uhakika kama Taifa na kuna matunda ambayo yako, hatuhitaji hata kutumia juhudhi kubwa ya *low-hanging fruits*

twende tukayachume haya matunda. Ukienda *border* ya Tunduma ambayo ndiyo *border* iliyo *busy* kuliko zote, mzigo ambao unatoka bandarini hauendi Kongo ya Moba wala Mlilo, unaenda Kongo ya Lubumbashi huko ndiko mizigo inakoenda. Kwa hiyo naomba katika mipango Serikali izingatie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *border* nne za kuweza kwenda Kongo; kuna Kongo kwa kupitia Kasesha *border* ambayo iko Jimboni kwangu, unapita Zambia kilometra 871 ndiyo unafika Kongo la Lubumbashi. Ukitaka kupita Kigoma, unaenda Moba kwenda mpaka Lubumbashi ni kilometra 750. Ukipita Tunduma ambayo ndiyo *route* ambayo inatumika zaidi ni kilometra 1,088.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa njia iliyokuwa fupi kuliko zote na naomba nilpongeze Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana katika kuboresha bandari ikiwa ni pamoja na Bandari ya Kasanga na kwa bahati nzuri sana, tunavyoongea leo hii lami imefika mpaka Bandari ya Kasanga na katika bandari ya ambazo ni *natural port* ni pamoja na Kasanga ndiyo maana Wajerumani waliitaka Bandari ya Kasanga iweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini ambacho kinatakiwa kifanyike? Unajua katika kazi kubwa ambayo tunafanya ya kujenga reli ambayo itaanza kubeba mizigo, si suala la muda mfupi, itachukua muda mrefu kwa sababu *heavy investment inatakiwa*. Niiombe Serikali ukivuka kutoka Kasanga kwenda upande wa pili ni kilometra 480 tu ushafika Lubumbashi. Kwa hiyo kwa wale ambao walisoma hesabu kwa *critical path analysis* ndiyo *shortest route*, niiombe Serikali upande wa kule barabara ipo ambayo inatoka Moba kwenda Lubumbashi, kuna vipande vichache sana ambavyo vinahitaji kumaliziwa ili tutumie njia hii, tutakuwa tunapeleka mizigo Kongo bila kupita Zambia bila kukutana na vipingamizi ambavyo tumekuwa tukivipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, tuna mahusiano mazuri sana na Serikali ya Kongo, hiki kipande

kifupi kwa sababu siyo kwamba kilometra 480 zote hazina barabara, barabara ipo ni maeneo machache sana haiwezi kuzidi kilometra 100. Tuanze kuvuna matunda haya ambayo hatuhitaji kutumia jitihada kubwa. Naamini kwa sababu Mheshimiwa Waziri anasikia, katika mpango ambao utakuja na bajeti ianze, kwanza ni bajeti ya maongezi tu, kinachotakiwa ni sisi tuwe na kivuko kutoka Kasanga kwenda upande wa pili ambacho kitaruhusu malori yapakiwe ndani. Ukipika kule ni barabara ya vumbi na kama kuna sehemu ambayo tutaweza kuwa na barabara ambayo *PPP*itafanya kazi ni kwa kipande hicho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuhitaji pesa nyingi, ni pesa ambayo ipo, hizi *barrier* zote ambazo tumekuwa tukikutana nazo za kiuchumi itakuwa ndiyo mwisho wake, tukitarajia kwamba eti tuna mahusiano mazuri na wenzetu wa Zambia wataturuhusu, tutachelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo na nimemwona Mheshimiwa Waziri akitikisa kichwa, naamini katika mpango ambao utakuja tutaliona hili likionekana vividly ili tuanze kuchukua hayo matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kabla mchangiaji aliyejikuwa ametajwa hajasimama Mheshimiwa Nicodemas Maganga, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, tunapoositaja nchi nyininge humu ndani, lazima tuzitaje kwa namna ya kujifunza ama kwa mfano halisi kabisa ni pale alipozungumza kuhusu biashara inayoweza kufanyika katika Tanzania na Kongo. Hata hivyo, katika katika mchango wake Mheshimiwa Kandege kaeleza kuhusu Zambia pia, kwa namna ile ambayo hatuwezi kuiweka hapa kama sehemu

ya mjadala kwa sababu inasemwa kwa namna ile ambayo haistahili kwa sababu si hoja iliyoko mbele yetu kujadili nchi nyngine.

Kwa hiyo nawakumbusha kwamba masharti yetu ya kuzizungumzia nchi zingine humu ndani, unaweza kuitaja nchi kwa maana ya kama inafanya jambo zuri ili Tanzania tuige kama inafanya jambo fulani haya kwa makusudi, kinyume na Tanzania na mambo kama hayo, hayo si sehemu ya mjadala kwa sababu itaonekana Bunge la nchi hii linaijadili Nchi ya Zambia ambayo si hoja iliyoko mbele yetu hakuna hoja ya kujadili Zambia mbele yetu. Nadhani kwa hilo nitakuwa nimeeleweka Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo tukumbuke hilo na tulizingatie, kwa sababu nchi zetu hizi zina mahusiano zaidi ya yale mambo ambayo tunaweza kuyazungumza humu ndani Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo ni muhimu sana kulikumbuka hilo.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mpango wa mwaka 2022/2023. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunifanya siku ya leo tena nipate nafasi hii adimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu waliotangulia wamesema mengi wamesema mazuri na naungana nao. Sasa nichangie Mpango wa Mwongozo wa Taifa. Nimeusoma wote, nimesoma sura ya pili pale inapoelezea kwamba deni la Serikali limekuwa. Jana wakati Waziri anasoma hapa nimepata meseji nyngi sana kwa Watanzania wanahoji ni kwa nini deni limekuwa kutoka bilioni 564 mpaka bilioni 644 ambayo ni sawa na asilimia 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu tuko kwenye kipindi kigumu, wakati huu Watanzania wanatupima, tuko kwenye utekelezaji. Nimpongeze Mheshimiwa Rais Mama

yetu Samia, kiukweli anapambana sana, kweli kabisa yaani bila unafiki mama anapambana, isipokuwa niseme tu wazi maana huwa napenda kusema ukweli, mama anacheza peke yake kwenye uwanja, wasaidizi hawafanyi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu nimeshuhudia hii trillioni 1.3 jinsi ilivyoshuka vijijiini kule kwenda kusaidia sekta mbalimbali kama vile afya pamoja na mambo mengine. Mwenzangu Mheshimiwa Tabasamu pale aliweka mfano wake, nami nataka nirudie tu maneno yake yale aliyoyasema, kuna hatari kubwa na hiki ni kipimo chetu cha kwanza sasa Wabunge kwenye maeneo yetu, hizi hela zinaenda kupigwa yaani inavyoonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza imeanza kuonekana mifano mingi mara *cement* imepanda, nondo zimepanda, yaani kila kitu kumekuwa na migogoro mingi, baada ya pesa kufika kwenye maeneo. Niiombe Serikali sasa iliangalia kwa macho manne, wananchi wanatupima, tukiangalia llani yetu yenye kurasa 303, wananchi walituamini kwa moyo mmoja kabisa na tuliahidi mambo mengi katika llani hii. Nashauri katika Mpango huu tuchukue vitu vichache tu ambavyo ni muhimu sana kwa wananchi wetu wale wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongelea suala la miundombinu za barabara mkoa hadi wilaya, bado hatujafanya lakini kwenye ilani humu wananchi tuliwaahidi. Ukiangalia kwenye mpango humu milolongo ni mingi, kuna ndege, *service*, mashirika yasiyo na mbele na nyuma, kwangu mimi naweza nikasema hivyo kwa uelewa wangu. Kwa wananchi wetu wale wapigakura waaminifu kuna vitu muhimu kama vitatu tu; miundombinu ya barabara, maji na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiboresha hayo maeneo tunaweza tukathaminiwa sana na tukaonwa kweli kuitishwa kwetu, hata kuja humu ndani tutaonekana tunaisaidia Serikali kulikoni kuelekeza matrillioni kwenye masuala ya watu

wachache, wanufaika wachache, hawa wengi ambao hawana uwezo wa kupanda hizi ndege wakaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu nazunguka sana kwenye nchi hii. Majimbo mengi nazunguka, ukiangalia pamoja na kwamba tumezungumza kwamba tumetekeleza, lakini kuna sehemu nyngi ambazo bado hazijafanyiwa marekebisho. Hii inasababishwa na mifumo yetu ya manunuvi, maana pesa kweli mwanzoni tu hapa ilitoka milioni 500, lakini ukiangalia mpaka sasa hivi hiso fedha hazijafanya kazi, bado sijui *process* za manunuvi, mifumo mara imekataa na sasa hivi mvua zinanyesha, ina maana wananchi wanaona kabisa haya ni maneno tunayaongea ambayo hayatekelezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namshauri Mheshimiwa Waziri, ye ye kweli ni mpambanaji na nimemwamini kuanzia kwenye tozo, pale alipokusanya bilioni 48 na akazisema hadharani na akazielekeza kwamba ziende zikajenge vituo vya afya nikamwamini kabisa kweli ana mapenzi mema, lakini kwa kuwa na ye ye ni binadamu naomba anisikilize ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu iliyopita nilishauri hapa kwamba, kuna wenzetu Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Vitongoji, hawa watu tumefanya nao kampeni kwenye uchaguzi, walikuwa wakitufungulia mikutano, tungewawekea hata kama ni shilingi 50,000 kwenye huu mpango na wao wajisikie vizuri, kuliko kuona deni linakua halafu wenzetu wanalala njaa, hawana hata shilingi 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine hapa, nimeona kwenye Mpango huu inazungumziwa kwamba maji yanatoka Ziwa Victoria kuja Dodoma. Nikiri tu wazi kwamba Kanda ya Ziwa bado tuna uhaba sana wa maji. Waziri wa Maji naomba hilo waliingize kwenye Mpango maana ni kelele kubwa ambapo mimi na Mheshimiwa Waziri tumewahi kupita Kanda ya Ziwa na kuwaaminisha watu kwamba litakuwepo hili

mwaka 2022 na 2023, lakini kwenye mpango humu halimo na wananchi wanahitaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la umeme, nimezunguka na aliyekuwa Waziri wa Nishati, tukawatangazia Watanzania kwamba umeme sasa unakuja tena tuliahidi mwezi huu ungekuwa umekamilika vijiji vyote, lakini mpaka sasa hivi bado sarakasi za kichina mpaka nazima simu kuonekana kwamba sina majibu ya kuwaeleza wananchi. Kwa hiyo Serikali ione umuhimu wa kupeleka umeme katika kila kijiji ambavyo vimebakia. Hii itaturahisishia sisi wanasiisa kuweza kuendelea kuwaongoza wananchi, maana tutakuwa tunatoa ahadi zile za kweli na zinafanikiwa kuliko kuwa tunapanga mipango elfu moja ambayo hatuiwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, kwa wachimbaji wadogo, nilshukuru Wizara ya Madini mwezi wa Nne ilinipa mkoa wa Kimadini na nimekusanya mpaka sasa hivi bilioni 6.49 kwenye Mkoa wangu wa Kimadini Mbogwe. Niwaombe tu wananchi wengine, Wabunge nimeona wamo wengi humu wawekezaji karibu kwenye Jimbo lile, tuje tushirikiane, lakini hii sekta inapaswa iangaliwe vizuri, maana kwenye Mpango huu haimo, haijawekewa kipaumbele kwamba Serikali itasaidiwa je kwenye huu mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wanaingiza pesa nydingi na hawajawezeshwa na Serikali. Ukiangalia kuna mashirika Serikali huwa inayapa bajeti na ukiangalia zile hesabu hata ripoti za CAG hayafanyi vizuri, hao wachimbaji ambao wanachimba kwa nguvu yao Serikali ione umuhimu ya kuweza kuwasaidia watu hawa. Kwa mfano mimi hapa kama nimeingiza bilioni sita ni miezi mitatu tu, unaweza ukaona kwamba jinsi gani watu hawa waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa wafanyabiashara; Taifa hili, na-*declare interest* nauza mafuta, ipo changamoto kubwa kwenye mafuta ya *petrol* na *diesel*. Mafuta yanapanda bei kila siku, Serikali ione sasa namna gani inaweza ikatenga bajeti ili kusudi mafuta yakishuka bei kila

mwananchi atapata unafuu kuitia hii bidhaa ya mafuta. Jana *EWURA* imetangaza tena kupandisha bei, wananchi wanalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia wakati tunakuja mara ya kwanza Bungeni humu mafuta yalikuwa yanauzwa shilingi 1,900, lakini mpaka sasa hivi mafuta yanaelekea shilingi 2,500, vijijini ambako hakuna vituo mpaka shilingi 4,000, lita moja ya mafuta. Hii inaonekana kabisa kwamba mambo yanaenda vibaya kwenye Taifa letu na sisi Wabunge tunakuwa kama vile hatuyaewi haya mambo wakati sisi naweza nikasema, ni maprofesa wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuiombe Serikali, ina bandari yetu na Waziri wa Nishati ameteuliwa juzi nimshukuru, nilimwona juzi sijui Norway, sijui wapi, alikuwa na mzungu, naomba apambane usiku na mchana, wananchi tunamtegemea ili tuweze kupata unafuu kwenye bidhaa ya mafuta. Mafuta yakipungua bei nauli zitashuka bei. Mafuta haya haya pia ndio yameshikilia uchumi wa nchi. Ukiangalia kwenye bandari yetu pale tunapoingizia mizigo, nahisi kuna michezo ambayo inafanyika pale ndio maana mafuta yanakuwa na bei juu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akidhibiti vizuri hapo tunaweza tukaishi vizuri sana na itaonekana kwamba tunamsaidia mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, niwaombe Wabunge wote, unajua sisi ni wasaidizi wa mama na anatusaidia kweli kwenye Majimbo yetu, lakini nashangaa Wabunge hatusemi mazuri yale ambayo mama anayafanya. Alijitokeza mchana kweupe akachanjwa, sisi Wabunge wengine tunachanja kimya kimya kwa kujificha. Mama ametupa pesa za barabara, mama anatupa kila pesa anayoipata na anaitangaza hadharani za shule, zahanati na kadhalika. Tunakuwa na ugumu gani kusema mazuri ya mama pale tunapokuwa kwenye mikutano yetu. Kwa kweli niseme kabisa, kuna Wabunge nawaangalia tu, maana hawajui walitendalo, hawasemi kama mama kawatumua amewapa zile fedha wananyamaza tu.

MBUNGE FULANI: Kweli.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Sijui wanategemea nini mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna kila sababu hata tutakopomaliza hili Bunge, Wabunge wenzangu, tukiwa tunaifuatilia hii trillioni 1.3 tukamseme mama, maana hata juzi tumemwona akihutubia mataifa na kiukweli mama ni mpambanaji, siwezi nikalinganisha sijui ni mchezaji nani ambaye nilikuwa namjua, labda Messi, ila kila akipiga pasi hivi, wengine wanazubaa tu. Niwaombe Baraza la Mawaziri, kila Waziri ajitathimini kwamba ni kwa nini umepewa kiti hicho na ufikirie hapa Tanzania unafanya nini? Umepewa nafasi utembelee kwenye V8 au umsikilize Mama au ukamshauri na ulete mawazo mbadala ya kuweza kulibadilisha Taifa. Tofauti na hapo hizi nafasi tutaziomba na sisil, tunaziweza kabisa tena tunazona ni kazi rahisi tu kuliko hata vitu vingine. (*Makofi/Kicheko*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Maganga, kengele ya pili imegonga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, ajiandae.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia hii nafasi.

Vilevile namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, ambaye ametujalia kuwa na afya njema na kupata faraja, tunafurahi kama wenzetu wanavyozungumza humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wangu wote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama mpambanaji ambaye ameamua kutupeleka mbele katika mapambano ya kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawashukuru watendaji wote akiwemo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika, Naibu Spika na Waziri wangu ambaye ni Mjumbe katika Kamati yetu ya Bajeti, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Huyu mimi namwita mpambanaji. Ninaamini kwa haya anayoyasikia humu ndani atayafanya kazi ili utekelezaji wake uwe mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ni Balozi wa Watu Wenyewe Ulemavu; anawapenda wale mavu na ninapenda kumpelekea salamu zake kama wale mavu wanasesma wanakupenda, tena karibu sana, uwe nao karibu. Nao wana imani kuwa katika Mpango wako hautawaacha nyuma wale mavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia upande wa kilimo. Kilimo kinachangia uchumi wa shilingi trilioni 44, sawa na asilimia 26.9 ya pato kubwa la Taifa ambalo ni shilingi trilioni 163, lakini ukuaji wake ni 3%. Tujitafakari na tulitathmini, kwa kundi kubwa la asimilia 66 ya Watanzania, wanapata ajira na mapato yao kupitia kilimo. Katika ukuaji huu wa 3% mpaka 4% bado tuna changamoto kubwa katika eneo hili. Maeneo mengine ni ya watu wachache, lakini unapozungumza kilimo, unamzungumzia mkulima aliye kijijiini, ambaye anategemea Bunge hili limkomboe na limtoe katika umasikini kumpeleka mbele. Kama uchumi tuna asilimia tatu, tunahitaji nguvu ya ziada katika eneo la kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote humu ni mashahidi, tunakwenda kukutana na changamoto za wanavijiji wakiwa katika hali ngumu na wanahitaji msaada wa kukombolewa. Niliongea katika Kamati ya Bajeti, tumepata pesa za *Covid*, lakini mkulima hayumo. Kama mkulima hayumo, ina maana siyo *priority*, lakini kwa vile ni mpango tunataka kuutekeleza hela nyingine zote zilizobakia

tuzifanyie mpango tuone tunafanya nini ili kuingiza pesa katika bajeti ya kilimo ili iweze kumkomboa mwananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaizungumzia leo Novemba na Novemba tayari tunategemea mvua za vuli zinaingia na hatuna mbolea. Mbegu hakuna. Tusimame kwa Pamoja, hakuna haja ya kumwambia yule amekosea, amekosea, hapana. Watanzania twende kwa umoja wetu, tujue changamoto hii ya mbolea, ya pembejeo na mbegu tunalifanyia kazi. Tutume haraka kabisa, maana yake tukisema tunangojea muda fulani, suala hili linatakiwa maamuzi yake yawe ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika Mkutano Mkubwa wa Mabadiliko ya Tabia ya Nchi Duniani, mnaiyona kama ni rahisi sana. Tunazungumzia uchumi wa dunia unaozungumzwa katika nchi za Umoja wa Mataifa. Nimeangalia katika baadhi ya magazeti, nimeyasoma na *ma-bulletin* zimetolewa *grant* nyingi sana za kilimo. Kilimo wamekitangaza, *small grant* kwa ajili ya wakulima. Je, sisi Watanzania tuliokaa humu ndani, hatuna ripoti ye yeyote tunazopata kwa wenzetu wanapokwenda katika mikutao mikubwa kama hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kutoka sasa hivi, wale wanaokwenda kutuwakilisha katika mkutano mkubwa wa *Climate Change* waje watupe mabadiliko ya tabia ya nchi na nini inabidi tufanye kwa Tanzania katika masuala ya kilimo, masuala ya afya na masuala mengineyo ambayo yanahitaji kubadilisha uchumi wetu kutoka hasi kwenda katika maeneo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata nafasi ya kutembelea bandari. Nilikuja na hoja ya Bandari ya Mtwara na Bandari ya Tanga. Tuipe kipaumbele. Nikupe taarifa, ninaona njia nyeupe ya kuleta mabadiliko ya bandari hizo mbili na pengine na bandari nyinginezo. Bandari ya Mtwara ni bandari ambayo ina uchumi mkubwa kama itasimamiwa wa nchi za jirani ikiwemo Zambia, Malawi na Congo na ndiyo

maana ilianzishwa Mtwara *Corrido* kwa ajili ya kuhakikisha mazao yote katika Mtwara *Corridor* yanapelekwa Bandari ya Mtwara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza, Bandari ya Mtwara haina makasha. Hivyo watu wanatamani mzigo yao waipeleke Mtwara, makasha yako wapi? Hakuna. Nilitemanu katika pesa ambazo zitaandaliwa, iwemo bajeti ya kupata makasha ili Bandari ya Mtwara ianzu kufanya kazi. Tumekubaliana na Waziri Mkuu alitoa azimio kuwa korosho zote za Mtwara, Ruvuma (maana yake sasa hivi korosho mpaka Njombe kote wanalima, mpaka Mbeya wanalima) zipelekwe Mtwara. Imeshindikana, Mtwara hakuna makasha. Bado tunampa mkulima mzigo wa kuondoa mzigo wa Korosho kutoka Lindi au Mtwara kuupeleka Dar es Salaam.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kwanza ni kwamba, badala ya ile tozo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lulida kengele imeshagonga.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Aaah! Naunga mkono hoja na ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce John Kamamba na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Awali ya yote, nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kupata uhai na uzima wa kuhudhuria Bunge lako hili Tukufu, leo tunajadili Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/2023 ambao utakwenda kuwa bajeti huko mbele kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kitu kimoja; chanda chema huviswa pete. Chanda chema huviswa pete. Nakusudia kwamba anayefanya mazuri, basi ni lazima asifiwe kwa mazuri na ndiyo maana ya chanda chema huviswa pete. Maana yake pete huwa kama ni tunza. Sasa kwa nini tunasitasita kuyasema yale mazuri ambayo yamefanywa na hii Serikali ya Awamu ya Sita? Kwa nini tunasita? Pete ambayo tutamvisha mama, tunasema mama mitano tena 2025 – 2030. Hiyo ni pete. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa haya mazuri ambayo ameyafanya. Nafikiri kwa Majimbo ya Tanzania Bara katika masuala ya TARURA, walipata kila Jimbo shilingi bilioni 1.5, katika shilingi trilioni 1.3 zimekwenda kwenye madarasa. Wengine wana madarasa 270 na wengine wana madarasa 300. Sasa haya ni maendeleo ambayo ndiyo tunayotarajia. Ndiyo maana tukasema, chanda chema huviswa pete. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati, sisi Watanzania tuna kawaida ya kuwa na mawazo mgando. Mtu mwenye mawazo mgando kule kwetu sisi huwa tunamwita tozobi. Kwa hiyo, wapo matozobi ambao hawatambui lile jema ambalo linafanywa hata kama analiona. Sasa kwa kuwa akili yake imeganda, mtu kama huyu huwa anaitwa tozobi. Huyo hata awe na jina kubwa vipi, lakini huyo ni tozobi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuepukane na kuwafuata matozobi. Nasi wengine tukawa matozobi kwani huoni kinachofanyika? Huna macho? Au ndiyo bwegenazi? Macho matatu, lakini hakuna jicho hata moja linaloona!

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, amewasilisha vizuri sana. Waheshimiwa Wabunge. ripoti ya Kamati ya Bajeti ni ripoti ya Wabunge wote. Kama utakuwa unazo ziada zako, nawe unaweka pale *inputs* zako. Ripoti ya Kamati ya Bajeti ni ripoti ya Wabunge. Wewe kama ni Mbunge, ina maana hii ni ripoti yako, unaipingaje? Unaipingaje? Kama una yako, weka, lakini hii imefanyiwa kazi kitafiti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambieni Waheshimiwa Wabunge, hii ni ripoti yetu sote. Nina usemi mmoja, wanasema kwamba bubu hutaka kusema mambo yanapomzidia. Nami leo mambo yamenizidi, nataka niseme. Nataka kusema kwenye kilimo. Sijawahi kusemea kilimo, lakini leo naona nisemee kilimo. Nasema kwenye kilimo, namuunga mkono Mheshimiwa Spika Job Ndugai, alisema Bunge hili la Kumi na Mbili liwe ni Bunge la Kilimo. Kwa hiyo, naunga mkono mawazo yote ambayo yametolewa na Wajumbe au Wabunge wa Bunge hili kuhusiana na kilimo, yote waliyoyasema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naongeza kusema usemi ule ule unaosema kwamba mtemewa mate na wengi, hulowa. Mheshimiwa Waziri, uwekezaji katika Kilimo bado haujatosheleza. Kamati ya Bajeti imeshauri tutenge shilingi billioni 450 kwa sababu kilimo kinachangia kwenye pato la Taifa kwa asilimia 26.6, lakini hiki kilimo kimeajiri Watanzania asilimia 67. Ina maana kwamba kama tuta-*invest* zaidi kwenye kilimo, *impact* ya kukua kwa uchumi itaongezeka zaidi kwa Watanzania wengi na kila mahali tutapagusa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tukiwekeza kwenye kilimo, tukija tuki-set *inflation, rate* ambayo tunaitaka tutaipata kwa sababu tayari mazao ya kilimo yatapanda bei kubwa. Ina maana kwamba *inflation* itazidi kwa maana kwamba *tuki-control* tukiwa tume *base* kwenye kilimo, tutakuwa tuko vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida nyingine ukuaji wa uchumi, kwa kuwa inachangia asilimia 26.6, tuki-*invest* zaidi ina maana kwamba tutapata ukuaji wa uchumi mkubwa zaidi. Hapo hapo katika mauzo ya nje, kama tutakuwa tumeuza mauzo ya nje mengi katika *balance of payment* tutakuwa tume-*improve*. Kwa mauzo ya nje hayo hayo, *exchange rate* yetu itakuwa *stable*; katika mauzo hayo hayo ya nje pia kutatusaidia katika masuala mengi. Kwa kuwa *GDP* itaongezeka, hata kile kipimo cha uhimilivu wa deni la Taifa, kwa sababu itakuwa *GDP* imeongezeka kuwa kubwa zaidi

na deni la Taifa litakuwa halijakua sana, ina maana kwamba tutapata zaidi uhimilivu wa deni la Taifa na itakuwa rahisi kwetu sisi kupata mikopo kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, kiwango cha umasikini kitapungua kwa sababu asilimia hiyo ya kilimo itakayokuwa imeongezeka ni kubwa mno na Watanzania wengi watakuwa wamefaidika. Sasa mimi niseme jambo moja katika vihatarishi kwenye Mpango huu. Naomba hili, kwa kuwa haya ni mapendekezo ya Mpango, naomba hili Waziri alichukue. Kihatarishi tulishaambiwa, tutakuwa tuna mvua chini ya wastani. Kwa kuwa tutakuwa tunamvua chini ya wastani na sisi tulisema kwenye Bunge la Kumi na Moja wakati wa *Covid-19*, Rais alituhamasisha tulime, tukalima tukapata mavuno mengi. Sasa hivi tumelima huko mahindi mpaka yameshuka bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iongezee mtaji wa *NFRA* kwa ajili ya kuhifadhi vyakula hivi. Kuhifadhi vyakula hivi, tutanusurika na balaa ambalo linataka kuja, lakini tutapata na mbegu. Ukipita huu muda wa mvua hizi ambazo ziko finyu, ina maana kwamba tutalima tena. Kwa hiyo, ushauri wangu nauweka kwa Serikali kwamba; kwanza, kutoka shilingi billioni 234.1 tuweke shilingi bilioni 450, Mheshimiwa Waziri tunalisema hilo wazi. Kwa kuziweka hizo, zikafanye kazi gani? Hizi tukapate pembejeo za kutosha, pia muda sahihi na kwa bei nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kingine katika hicho kilimo, tukatengeneze mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji. Kingine, zile kodi na tozo kwenye mazao ambazo zinakera, tukiziondoa tutaweza kuweka kama ruzuku, kwa maana hiyo, hayo tutayafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashauri katika kihatarishi. Kwenye kihatarishi, sisi watu tuliosoma soma vitabu, Mashehe kama sisi, huwa tunajua Nabii Yusuf; Mfalme aliota ndoto akasema kwamba *raaitu sababa karatul simani yakul huna sabuna hijaf*. Nimeota ng'ombe saba walionona

wanawala saba waliokonda. Wasabu *sumbulat nhudhuri wa bukharu yabisat*. Na mashuke saba mabichi na mengine saba makavu. Kwa hiyo, Mfalme akataka *taawil*, apewe tafsiri ya ndoto. Nabii Yusuf alimjibu kwamba mtalima miaka saba, itakuwa ya neema, lakini itakuja miaka saba ya njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hifadhini chakula kwa ajili chakula na kingine kwa ajili ya mbegu kwa miaka ambayo mvua zitaanza kunyesha tena. Kwa hiyo, nami natoa ushauri huu kwamba kwa kuwa tumeshatabiriwa kwamba mvua zitakuwa finyu, tuweke chakula, tuhifadhi. Kuhifadhi ina maana kwamba, hifadhi ya chakula cha Tanzania ipewe mtaji kwa ajili ya kuhifadhi. Utakapokuja muda wa njaa, watu watatutegemea; na sasa hivi watu wanatutegemea, tulilizungumza hili mwakajana 2020. Tumelima kwenye *Covid*, tukapata mazao mengi, faida yake tuje tuipate hapa sasa hivi. Tumeshaambiwa mvua hazitakuwa sawa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda nichangie mchango huu wa kilimo katika nchi yangu hii na hilo ndiyo maana nikasema kwamba bubu hutaka kusema mambo yanapomzidia. Limenizidi mwenzenu, leo nasimama mbele yenu, kauli yangu kwenu kuitoa. Kwa hiyo, nami hii kauli kwangu ilikuwa siyo ya kawaida kuzungumzia kilimo, lakini leo imenipasa nzungumzie kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru sana. Tunaiomba Serikali, kwa kuwa haya ni mapendekezo, hebu ajaribu kutazama, *tuki-invest* kwenye kilimo, tutavuka. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, ajlandae.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi kuchangia kwenye Mapendekezo ya Mwongozo wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023. Kwa nafasi hii, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kwa fedha nyingi sana ambazo ametuletea sisi Wilaya ya Kakonko kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Tunamshukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kakonko kwa fedha ambazo tumeppata, zinakwenda kufungua na kujenga barabara maeneo mengine ambayo tangu dunia inaumbwa tulikuwa hatujawahi kupata barabara. Mheshimiwa Rais katupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Waziri wa Fedha kwa Mpango mzuri aliotuletea. Hii inakwenda sambamba na Kamati yenyewe, Kamati ya Bajeti. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitachangia katika maeneo machache, moja ni uandaaji na utengaji wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya kimkakati, ipo miradi ya kimkakati kama umeme, mpango wa bwawa la umeme maharufu kwa jina la Mwalimu Nyerere, reli ya kisasa *Standard Gauge* na miradi mingine kama hiyo. Muda mwiningi fedha ambazo zinapangwa katika maeneo hayo zimekuwa ni fedha kidogo naomba sana fedha ziandaliwe za kutosha ili miradi hiyo iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni miradi ambayo ni ahadi ya Viongozi wa Kitaifa, nimekuwa nikifuatilia muda mwiningi Waheshimiwa Wabunge wengi wanaauliza maswali kufuatia maeneo ambayo viongozi wa kitaifa waliahidi ujenzi wa miradi ya maji, ujenzi wa barabara na kadhalika. Niombe

pia fedha ziandaliwe za kutosheleza maeneo hayo ili kuondoa changamoto ambayo inajitokeza muda mwingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, napongeza sana kwamba fedha nyingi zimetolewa na zimepangwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa lakini haijaonyesha kwenye mpango huu fedha kwa ajili ya nyumba za walimu. Kujenga madarasa bila kujenga nyumba za walimu hakutapelekea ukamilifu wake hii ni kwa sababu fedha zimepelekwa kwenye maeneo mfano shule shikizi, ukifuatilia kwa ukaribu shule shikizi zimejengwa katika maeneo mapya, mengi ni maeneo ambayo ni ya wafugaji, mengi ni maeneo ambayo ni ya wakulima kwa hiyo ukijenga madarasa katika maeneo hayo bila kujenga nyumba za walimu katika maeneo hayo kwa ukaribu maana yake wanafunzi watakuwa wanasoma na madarasa yatakuwa yanaachwa wazi, maana yake hayatakuwa na uangalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba fedha zitengwe kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu na hii itapelekea walimu kukaa karibu na shule lakini hii pia itapelekea shule kuwa na ulinzi kwa maana kwamba walimu watakaa karibu na shule. Vilevile madarasa yale yataweza kutumika vizuri. Kwa hiyo hamuendi kama ambavyo tumeamua kupeleka fedha nyingi upande wa ujenzi wa madarasa basi tupeleke fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mabweni, mabweni ni muhimu sana kwa ajili ya watoto hasa watoto wa kike kwa upande wa shule za sekondari, kutokuwa na mabweni kunapelekea wanafunzi hawa kusafiri umbali mrefu, kutokuwa na mabweni kunapelekea wanafunzi hawa kukutana na vishawishi njiani. Niombe fedha za kutosho zipelekwe katika maeneo hayo tuwe na mabweni ya kutosheleza wanafunzi waishi maeneo hayo ili kuwa na uhakika kwamba watakuwa na muda mzuri wa kujisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa walimu tumefanikiwa vizuri kwenye mpango wa elimu bila malipo, wanafunzi wapo wengi wa kutosha na muda huu tunapeleka

madarasa ya kutosha lakini walimu bado hawajaonekana kwamba kuna mpango maalumu wa kuweza kuajiri. Ninaomba fedha ziandaliwe mpango uandaliwe mzuri ili walimu waajiriwe wa kutosha waweze kusaidia vijana wetu katika maeneo hayo, hii iende sambamba na ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu za sekondari sawa tunapeleka fedha tunajenga madarasa lakini ukamilishaji wa maabara, ninaomba fedha ziandaliwe za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa maabara. Ujenzi wa maabara unapelekea moja wanafunzi kupata nafasi ya kujifunza kwa vitendo, wakijifunza kwa vitendo inapelekea uelewa mkubwa zaidi niombe hii iende sambamba na ujenzi wa maktaba katika shule zetu za sekondari. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ni muhimu sana hasa miundombinu ya barabara, Mkoa wetu wa Kigoma haujaweza kuunganishwa kwenye Mikoa mingine kutoka Tabora kwenda Kigoma, Mpanda kwenda Kigoma, Kagera kwenda Kigoma. Ninaomba fedha ziweze kupelekwa katika maeneo hayo, barabara ziweze kukamilishwa na kuweza kupelekea huduma muhimu sana kwa wananchi wetu hasa kwa Mikoa ile ambayo hajaweza kuunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafatiwa na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mheshimiwa Stella Fiyao ajiandae.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia *draft* hii ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nianze kwa kuelekeza shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa mambo mengi ambayo anaendelea kuyafanya na kuhakikisha kwamba wananchi wetu

wanaendelea kunufaika. Nitoe shukrani za pekee baada ya wananchi kutoa kilio cha bei za mahindi na kupelekwa kwake alitoa shilingi bilioni 50 kwa ajili ya ununuzi wa mahindi na fedha hizo kwa kweli zilifanya kazi kubwa tu ya kuhakikisha kwamba mahindi yananunuliwa na niliona mwenyewe kwa sababu hata Jimboni kwangu fedha hizo zilifika. Tunatoa shukrani nyingi sana kwa niaba ya wananchi wote ambao walinufaika na angalau bei ikaweza kuwa *stable* kidogo kutoka pale ilipokuwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye mambo machache ambayo nimeona ni vizuri nikitoa ushauri kwa Serikali wakati wa kuandaa mpango ambao tutakuja kuupitia utakapokuwa umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naomba niweke nyongeza kidogo kwenye ukurasa wa 68 wa Mpango unaohusu zao la chai, naomba niikumbushe Serikali kwamba wametaja Njombe, wametaja Lushoto, Iakini Kilolo imesahaulika pale nafikiri ni makosa ya kiuchapishaji, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili basi akafanya marekebisho kwamba pia nako kule kuna mashamba makubwa yana zaidi ya miaka 30 na nimeshasema hapa kwa muda mrefu hilo ninafikiri litakuwa ni kosa la kiuchapishaji kwa sababu Kilolo isingweza kusahaulika kwa sababu hata Waziri wa Kilimo ameshatembelea tayari.

Kwa hiyo, nafahamu analijua, kwa hiyo utakaporudi mpango nitaiona kwa sababu ni kitu ambacho kinafahamika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kilimo hasa kwenye mahitaji ya mbolea, nchi yetu inahitaji mbolea kiasi cha kama tani laki saba na hivi tunavyozungumza ukisoma mpango hata kwenye utekelezaji pale haukusema mbolea iliyokwisha ingia ni mbolea kiasi gani. Mpango pia hauoneshi mipango ya kuingiza hii mbolea kiasi gani zaidi ya kusema kuna kiwanda hapa Dodoma, kuna mwekezaji kutoka Burundi atajenga, kwa hiyo tunatarajia kitakapokamilika na hatujui hicho kiwanda kitakamilika lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa na watabiri wa hali ya hewa kwamba mwaka huu tutapata mvua za wastani au chini ya wastani, maana yake ni kwamba mikoa michache sana itakayopata mvua na hiyo ndiyo inayotegemea ilishe nchi yetu. Kwa hiyo upo uwezekano mkubwa wa kutokuwepo na chakula cha kutosha au kuwa na mabaa mawili baa la kwanza linalotokana na asili ambalo ni baa la kukosa mvua, lakini baa la pili ni baa ambalo tunalitengeneza wenyele la kuto kutoa ruzuku kwenye mbolea na kusababisha mbolea hiyo iwe bei kubwa na kuwafanya wakulima wasinunue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo wale wakulima wanasubiri mvua kidogo inayonyesha, kwa mfano baadhi ya Mikoa mvua zimeanza hawajapa hilo punguze la hiyo mbolea wala ruzuku na wala Serikali mpaka sasa haijasema chochote kwa sababu ameshatoa maelekezo tunaamini kabla ya Bunge hili kuisha basi tutasikia. Pia kwenye mpango ili hii iwe endelevu ningependa kushauri kwenye mpango utakapokuja basi tujue ni mpango gani wa muda mrefu utakaofanya wakulima waweze kupata nafuu ya mbolea kama ilivyo kwenye nchi za jirani ambazo baadhi yake wengine wamezitaja walipokuwa wakitoa michango yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kutoa ushauri ni kuhusu mikopo kwa vijana, akina mama na wenyewe ulemavu na hasa mifumo inayotumika. Ningependekeza kwenye mpango unapokuja sasa mwanzoni ilikuwa vikundi viwe vikubwa baadaye ikawa watu watano pendelekezo langu ni kuwa, lengo la mikopo ile ni kuongeza ajira, mawazo ya kutengeneza mradi ili uweze kuleta ajira si lazima iwe watu watano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja anaweza akatengeneza mpango wa kukopesha watu na akaajiri zaidi ya watu ishirini wakati kikundi kinaweza kikawa cha watu watano na kikawa na mradi wa kufanya wao watano peke yao. Maana yake ni kwamba mpango uje na vigezo vinavyofanya hata kijana mmoja, hata mwanamke mmoja,

hata mlemavu mmoja kukopa ili mradi anazalisha ajira nyingi kwa vijana, wanawake na watu wengine na hiyo itasaidia sana kwa sababu inaonekana wasiwasi ni uwezekano wa kulipa, kwa hiyo kuna dhamana zinazoweza kutengenezwa na nyingine zilishawahidi kupendekezwa hata humu ndani, watu wapeleke vyeti ziwe dhamana wamemaliza *degree* zao au vitu vingine vyovoyote vinavyoweza kuwa dhamana, au basi vijiji na maeneo watu wanaofahamiana vidhamini, lakini hii mikopo lengo ni kuzalisha ajira mtu mmoja apewe kusiwe na hii kusema wangapi ili mradi anazalisha ajira kwa watu wengi zaidi kwa sababu lengo ni kukuza uchumi ni kuweka mzunguko wa kutosha. Kwa hiyo, kigezo cha vikundi kinaelekea kupitwa na wakati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite pia kwenye kitu kingine cha miundombinu hasa vijijini kuhusu suala la barabara. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais ametoa fedha...

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa nafikiri inatoka Msekwa. Taarifa kutoka Msekwa, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi nafikiri.

TAARIFA

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Nataka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia sasa Mheshimiwa Nyamoga kwamba kuhusu suala la mikopo kwa vikundi itshe tu kwamba Serikali inatoa pesa kwa ajili ya vikundi kwa maana ya asilimia 10 (4:4:2), lakini mikopo hii iwe yenye tija. Unakuta kikundi cha watu hamsini wanakopeshwa milioni mbili bado hiyo pesa haitaweza kuleta tija kwa watu hamsini shilingi milioni mbili. Kwa hiyo, ikiwezekana vikundi mbalimbali viwekewe pesa ya kutosha ili waweze kuanzisha hata viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Justin Nyamoga unaipokea taarifa hiyo.

MHE. JUSTIN L. NYAMOGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea. Nijielekeze kwenye mpango wa *TARURA*, tumefurahi sana tumepewa wengine Bilioni 1.5, wengine Bilioni Moja kwa ajili ya barabara na kwa kweli fedha hizi zimesaidia sana tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu sasa kwa sababu ukiangalia tulivyojadili mwaka jana tulikuwa tunasema kwenye mfuko wa barabara iwekwe sheria zigawanywe ielekee... mpaka sasa *TARURA* ilianzishwa lakini chanzo chake cha mapato hakijawa kile ambacho ni mfuko kama ilivyo mifuko mingine, mfuko wa maji, mfuko wa barabara na mifuko mingine. Kwa hiyo tunagemea Mheshimiwa Rais akitoa kama hivi na tunamshukuru anaendelea kutoa na mwakani labda itafanyika hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ingekuwa kwenye huu mpango kama hizi fedha zipo na zinaendelea kuwepo basi ianzishwe programu kama ilivyo programu nyingine ambazo zimekuwa zikianzishwa na zinapewa fedha, labda iitwe *Rural Road Maintenance Program* na iwe na mipango kabisa ili tusiwe tunaenda kwamba leo kuna fedha tujue mpango huu labda ni wa miaka mitatu, miaka minne na *tuta-cover* barabara ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *TARURA* ije wakati wakuja wana mpango, waje na mpango wa ukarabati wa barabara za vijijini unaoeleweka ambao utasababisha sasa fedha zinazopatikana zinapelekwa na zinaenda moja kwa moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ningependa kushauri kwenye mpango ikiwepo ni miradi ya kimkakati kwenye Halmashauri na nina uhakika kwa sababu hili suala ni la Wizara ya Fedha Mheshimiwa Waziri analifahamu. Vile vigezo vilivyopo vya kupewa miradi ya kimkakati tumekwisha kuvilalamikia sana kwamba

vinatengeneza ubaguzi katika kunufaisha Halmashauri hasa zile zenye vipato vidogo na zile zenye hati chafu na hati zenye mashaka. Kwa hiyo, tulikuwa tumependekeza kwamba vigezo hivyo vипитиве ili viweze kuwa rafiki kwa Halmashauri zote. Pendekezo langu ni kwamba mpango huo utakapokuja basi uwe unataja kwamba vile vigezo kwa sababu mara nyingine kwenye Kamati tulikuwa tumeambiwa unapitiwa basi tuambiwe kwamba vimepitiwa na vipo kwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Fiyao, Mheshimiwa Subira Khamis Mgatu, ajiandae.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa maoni yangu katika mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Arusha vilevile naomba niendelee kumpongeza Mama yetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutuongoza kwa weledi mkubwa na vilevile kwa kuendeleza diplomasia ya kimataifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuchangia kwenye sekta muhimu ya afya. Naipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha huduma hizi za afya pamoja na maboresho yote yaliyofanyika bado kuna changamoto nyingi sana kwa wananchi wetu kupata huduma bora za afya. Changamoto hizi ni pamoja na gharama kubwa za afya kwa wananchi wetu, ubora wa afya wanaopata wananchi wetu na vilevile kupata kwa huduma za afya kwa wakati. Changamoto zote hizi suluhisho lake ni moja tu ni kuwapatia wananchi wetu bima ya afya kwa wote. Taarifa za kutoka Wizara ya Afya mpaka leo hii ni asilimia 12

tu ya Watanzania ambao wananaufaika na huduma hizi za bima ya afya kwa wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati ilivyoshauri kwenye mapendekezo yake na mimi naomba niweke msisitizo kwa Serikali kutuletea Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa wote ili basi sheria hii iweze kwenda sambamba na Mpango wetu wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa na vilevile wananchi wetu waweze kunufaika na huduma bora za afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile niweze kuchangia katika mwenendo wa riba za mabenki. Jana tulimsikia Mheshimiwa Waziri hapa akisema moja ya mafanikio ya sekta hii ya mabenki ni kushuka kwa riba kutoka asilimia 16.8 hadi asilimia 16.6, punguzo la asilimia 0.2 tu. Sisi kama wawakilishi wa wananchi hatuwezi kwenda kusema kwamba punguzo la asilimia 0.2 tu ni mafanikio ya sekta hii ya kibenki. Wananchi wetu bado wanateseka na riba kubwa za mikopo ya kwenye mabenki nasi Wawakilishi wao inabidi tufanye jitihada za makusudi kuhakikisha riba hizi za mabenki zinashuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwenye hotuba zake nyakati tofauti akiagiza Benki Kuu ya Tanzania iweze kushusha riba hizi za mabenki hadi kufikia asilimia 10 au chini ya hapo. Asilimia 16.6 inayosemwa hapa hii ni wastani tu, bado kuna wananchi wengi wanakopa kwa riba ya zaidi asilimia 18. Natambua sana jitihada zinazofanywa na Serikali yetu kuhakikisha riba hizi za mabenki zinashuka, wamesema wenzangu hapo ikiwemo mojawapo ni kupunguza kiwango cha chini cha akiba ambazo mabenki haya yanawekeza *BOT* yaani *Statutory Minimum Reserve* hadi kufikia asilimia Nane, lakini bado tumeona hili siyo suluhisho la kushusha riba za mabenki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali yetu imetoea Shilingi Trillion Moja imewapa Benki Kuu ya Tanzania ili kuweza kushusha hizi riba za mabenki, lakini bado tumeona siyo

suluhisho pia ya kushusha riba hizi. Pamoja na hayo jitihada zote zilizofanywa bado tunaona ni punguzo la asilimia 0.2 tu ambayo bado sidhani kama tunaweza tukajisifia kuwa ni mafanikio ya sekta hii ya kibenki. Naamini Benki Kuu ya Tanzania pamoja na Wizara yetu ya Fedha inao wachumi wabobezi wengi na kwa pamoja wanaweza kushirikiana kuhakikisha riba hizi za mabenki zinashuka kwa asilimia kubwa. Ili uchumi wetu uweze kuwa uchumi shirikishi na jumuishi lazima wananchi wetu waweze kwenda kwenye mabenki mbalimbali na kuwa na uwezo wa kukopa kwa riba nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti tuliweza kukutana na Umoja wa Mabenki ya Tanzania (*TBA*) na walitupa changamoto zao nyngi ambazo zinachangia gharama kubwa za uendeshaji wa mabenki na hivyo wao wanalahizimika kuongeza riba katika mabenki yetu. Sababu nyngi walizotupa kati ya hizo kuna sababu mbili ambazo zipo ndani ya Wizara ya Fedha ambao wao wanaweza kuzitatua ili basi kuhakikisha riba hizi zinaweza kushuka kwa wanachi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu walizozitaja moja wanasema kupishana kwa sera kati ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania, zote hizi ni Taasisi za Serikali naamini Waziri wetu hapa anaweza kukaa na taasisi hizi na kusuluuhisha na kufanya riba za mabenki ziweze kushuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyngine waliyoitaja Umoja wa Mabenki, walisema vilevile ni kutokuwa na ushirikiano kati ya Mamlaka ya Serikali na mabenki ya biashara. Naamini pia hii sababu iko ndani ya Wizara ya Fedha, wanaweza kwa pamoja wakashirikiana na umoja wa mabenki haya ili basi watafute suluhisho la kushusha riba hizi za mabenki kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo pia namuomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hotuba yake aweze kutueleza hapa mikakati Serikali ilionayo

itakayofanya kwa ajili ya kushusha riba za mikopo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya ajiandae.

MHE. STELLA S. FIYAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika mpango huu. Na kwa umuhimu mkubwa nitachangia katika sekta ya kilimo, hasa kwa kutambua umuhimu wake mkubwa katika kuongeza Pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua umuhimu mkubwa wa sekta hii katika kukuza uchumi wa Taifa letu, na hasa tunapozungumzia sekta ya kilimo, ni sekta ambayo imetanuka kwa upana wake. Leo hii tumeketi katika Bunge hili ni kwa sababu tumekula chakula vizuri na ndiyo maana tumekusanyika hapa, yote hii ni sekta ya kilimo tunaigusa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini umesimamia kikao vizuri hapo kwa sababu umekula chakula kizuri. Leo hii tunamuona Waziri wa Fedha amekaa pale kwa kutulia, ni kwa sababu amekula chakula vizuri; yote hii tunaigusa sekta ya kilimo. Hata mgonjwa anapokuwa hospitali, *doctor* anapompa dawa anasisitiza kwamba ale chakula kwa kutambua umuhimu wa chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunapozungumzia viwanda, ili viwanda viende sawasawa ni lazima kwanza mtu awe amepata chakula, ameshiba na ndiyo maana atafanya kazi katika viwanda. Kwa hiyo hii ni sekta muhimu sana katika Taifa letu na tunatakiwa tuichukulie kwa uzito wa hali ya juu sana kwa ajili ya kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tuamini kwamba hakuna uchumi unaoweza kukua katika Taifa lolote kama sekta ya kilimo itawekwa nyuma kwanza. Ni lazima tuitangulize sekta ya kilimo mbele ndipo tunaweza kufanikiwa katika mambo mengi ya kukuza uchumi wa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema sekta ya kilimo ni muhimu sana; leo hii sekta ya kilimo inachangia kwa asilimia 26.7 katika kukuza uchumi wa Taifa letu, hivyo, tunapaswa kujua kwamba hii ni sekta muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la ajabu na la kusikitisha ni kuona kwamba sekta muhimu ya namna hii yenye kukuza uchumi wa Taifa letu inakua kwa asilimia 3 mpaka 4; hili ni kitu cha kushangaza sana kwenye Taifa letu. Na ninashukuru jana Mheshimiwa Rais Samia alipokuwa akihitubia aliweza kuigusia sekta ya kilimo, kwamba ni sekta muhimu katika kukuza pato letu la ndani. Hata Mheshimiwa Rais anatambua umuhimu wa sekta hii katika kukuza uchumi wa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaona kwamba kwa namna sekta hii inavyokuwa kwa kusuasua inaonesha kwamba siyo kipaumbele katika Serikali yetu. Ninaweza nikazungumzia hali halisi, hasa kwa mikoa yetu ambayo kwa asilimia kubwa wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wananchi wa Mkoa wa Songwe wamekaa kusikiliza kauli ya Serikali inasema nini kuhusu pembejeo za kilimo maana hali ni mbaya sana ambayo inasababisha wananchi wengi na wakulima asilimia kubwa kukata tamaa kutokana na bei ya pembejeo za kilimo kuwa mara mbili ya ilivyokuwa awali. Na bei hizo zimesababisha wakulima wengi kushindwa kumudu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu huu ukienda kwenye mikoa yetu ni mikoa ambayo wakulima wengi wanakuwa wameandaa mashamba lakini ni tofauti kabisa na miaka

yote. Sasa hivi ukienda kila mkulima amekaa kwa hali ya kujisahau maana hana tumaini lingine. Watu wanawaza watapatajaje hizo pembejeo za kilimo kutokana na hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri tu Serikali, kama tunavyoweza kuweka kipaumbele katika miradi mingine, kama tunavyoweza kuhakikisha sekta ya ujenzi inakua kwa kasi, kama tunavyoweza kutumia nguvu kubwa kukuza sekta ya nishati, nguvu hiyo hiyo tuielekeze katika sekta ya kilimo ili kukomboa uchumi wa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali siyo shwari kwa mikoa yetu. Sasa hivi hata tukienda huko kwenye mikoa yetu kuna hatari ya kupigwa mawe, maana mwananchi hana tumaini kabisa na hajui kesho yake itakuaje. Na kwa kujua kwamba mawazo huwa yanababishi vidonda vya tumbo, ni hatari zaidi huko kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe kuugua vidonda vya tumbo maana hawana tumaini, wamejawa na msongo wa mawazo, kitu ambacho kinaweza kikawasababishia matatizo ya kiafya kwenye mili yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali itumie njia ya dharura kutatua suala la pembejeo za kilimo kwenye mikoa yetu. Tuombe Serikali itoe ruzuku kwa dharura ili kupeleka katika pembejeo za kilimo na wananchi wetu waweze kupata pembejeo za kilimo kwa bei ndogo ambayo kila mkulima ataweza kumudu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikuwa tunanunua mbolea kwa shilingi 65,000 lakini bado kilikuwa ni kilio kwa wananchi. Leo ukienda Mkoa wa Songwe, mfuko wa mbolea unaupata kwa shilingi 120,000, jambo ambalo hakuna mkulima anayeweza kumudu gharama hizi. Lakini wakati huohuo ukienda sokoni mkulima anauzu gunia la mahindi kwa shilingi 30,000 na kwa kanuni, ili ulime eka moja na uweze kuvuna mahindi ya kutosha ni lazima uwe na mifuko sita ya mbolea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mkulima gani ambaye anaweza kumudu shilingi 720,000 kwa ekari moja tu; mkulima yupi wa namna hiyo? Hiki kitu hakiwezekani, hebu tuombe Serikali jambo hili mllichukue kwa udharura. Kwa wakati mwingine tunasema miyo yetu inavuja damu maana tunajua hali za wakulima wetu huko mikoani hali ni mbaya mno. Na kuna wakati sisi kama Taifa tunapaswa kujifunza hata kwa nchi jirani ambazo zimetuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda Zambia na Malawi bei za mbolea ziko chini kuliko Tanzania, lakini Malawi na Zambia wanajumua mizigo yao huko nje ambako ndiko na Watanzania tunakojumua na wanapitia katika Bandari ya Tanzania kwenda kwenye nchi zao lakini bei zao zipo chini. Hii inaonesha kwamba mrundikano wa kodi kwenye nchi yetu unawatesa na kuwaumiza wakulima wetu. Tuombe tuwanusuru wakulima wetu, lakini tunusuru uchumi wa Taifa letu; tuweke ruzuku katika pembejeo za kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninaomba kuishauri Serikali kama wengine walivyosema kwamba fedha zilitolewa zaidi ya bilioni mia moja ishirini na kwa ajili ya kununua mazao. Nataka kusema jambo hili kwa uchungu kabisa. Fedha hizi kwa asilimia kubwa hazijamgusa mkulima wa chini maana fedha hizi kwanza zimefika kwa kuchelewa lakini badala yake zimewagusa wafanyabiashara badala ya wakulima. Wakulima bado wana maumivu, bado wana kilio pamoja na Serikali kutoa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe kwa wakati mwingine fedha zitolewe kwa wakati ili ziweze kumlenga mkulima mdogo ambaye ndiye anayehangaika kule chini na anasota, fedha zitolewe kwa wakati. Na ninaamini tukifanya hivi tunaweza kumkomboa mkulima wa chini ambaye anataka kukwamuka kutoka hatua ya kwanza kwenda ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, ahsante. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Hongera!

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma ajiandae.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi jioni ya leo kuweza kuchangia mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kusimama jioni ya leo, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan; Makamu wa Rais, Dkt. Mpango; Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote, kwa kazi inayoendelea kufanywa katika kuona kwamba nchi yetu inapiga hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini kipekee pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa maandalizi ya mwongozo wa mpango huu. Na pia nampongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati pamoja na taarifa ambayo imewasilishwa na ninaendelea kuunga mkono hoja ambayo tumewasilisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mapendekezo ya mpango ambayo yamewasilishwa inaonesha Serikali imejipanga kukusanya na kutumia zaidi ya trillioni 39 kwa mwaka 2022/2023. Maoni yangu katika *item hii* ya makusanyo na matumizi kwa kuwa Serikali ina mzigo mkubwa wa miradi mbalimbali ya kimkakati, na kwa kuwa Serikali yenyewe iliahidi kwa mwaka huu wa fedha 2021/2022 kwamba itakamilisha kujifanya tathmini ya namna ambavyo inaweza kukopesheka kwenye masoko ya kimataifa (*sovereign credit rating*), naomba mpango ujao sasa itakayouandaa Serikali ije na taarifa mahususi ya kukamilisha tathmini hii ili iweze kuingia kwenye soko la fedha la kimataifa kupitia *infrastructure bond*, kupitia *Eurobond*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kupitia pia hatua ambayo hata Mheshimiwa Rais ameielekeza Wizara ya Fedha hizi *municipal bond* ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi hii ya kimkakati ambayo inachukua muda mrefu kuweza kuanza kutumika na kuweza walau kuanza kurejesha sehemu ya gherama na Serikali ijikite katika kugharamia shughuli zile za msingi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tukizingatia imeshaongeza ajira mpya, imeshapandisha madaraja watumishi, imeshaongeza kwenye masuala ya mikopo ya wanafunzi, kwa hiyo ni wazi kabisa itahitaji fedha, na ili kuwapunguzia pia Watanzania zile kodi zingine kwa mfano tozo, Serikali ijikite kwenye masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tumeona namna gani Serikali imefanikiwa kwenye huu mkopo wa masharti ya bel nafuu, uwezo wa Mheshimiwa Rais wa kushawishi, wa kujenga hoja ndani ya muda mfupi tumeweza kupata triliioni moja na bilioni 300, ni wazi hata hili pia linawezekana.

Kwa hiyo ninaomba katika mpango unaokuja Mheshimiwa Waziri wajielekeze huko ili kupunguzia gherama. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaomba katika taarifa yake Mheshimiwa Waziri ameainisha kwenye ukurasa wa 20, ametoa msisitizo kwamba bado kuna mianya ya uvujaji wa mapato, lakini bado pia kuna mianya ya kuvuja mapato kupitia risisti *EFD*. Nashauri atakapokuja na mpango kamili aeleze kinagaubaga ni namna gani Serikali itadhibiti uvujaji ambao yeye mwenyewe ameusema katika taarifa yake, kwamba hali bado haiyumkiniki, hali bado siyo shwari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze hatua ya Serikali ya kuweza kutoa kibali cha kuajiri watumishi zaidi ya 1,000 wa *TRA*. Hatua hii iendane na mkakati mahususi watakavyoweza kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nijielekeze kwenye suala zima la mwenendo wa mfumuko wa bei. Katika mapendeleko ya mpango huu yaliyowasilishwa inaonekana bado mwenendo wa mfumuko wa bei upo ndani ya viwango ambavyo vimeainishwa kwenye Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa, lakini hata hivyo mpaka sasa hivi mfumuko wa bei uko asilimia nne ukilinganisha na asilimia tatu ya kipindi kama hiki mwaka jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hali ni tete mtaani. Bei za bidhaa cementi, bei za bidhaa nondo, bei ya mafuta, kwa kweli hali bado ni tete. Lakini niishukuru Serikali kuptitia Wizara ya Nishati na nimpongeze Waziri wa Nishati, Mheshimiwa January Makamba, amekuwa akitufahamisha hatua mbalimbali na mwelekeo wa Serikali wa kuweza kuona bei ya mafuta inapungua au hata kama inaongezeka lakini si kwa kiwango kilichokusudiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kwa hizi bidhaa za nondo, cementi, mabati, tuiombe Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Fedha nao watuambie, wawaarifu Watanzania mkakati wao wa kuona namna gani bei zinapungua. Na ukizingatia kuptitia bajeti ya 2021/2022 Serikali iliweka hatua mbalimbali za kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza leo bei ya nondo ukilinganisha ya Julai kwa tani zinazozalishwa hapa nchini BS 300 ilikuwa milioni moja laki nane thelathini. Tunapozungumza leo mwezi Novemba, kwa tani moja ya nondo ya aina hiyo BS 300 inayozalishwa hapa nchini ni milioni mbili laki mbili themanini, ongezeko la laki nne na nusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuzingatia kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Rais ya hizi pesa za *1.3 trillion*, na ujenzi unaoendelea zaidi ya bilioni 500 zimepelekwa kwenye ujenzi. Na ninaomba niikumbushe Serikali ilituletea pesa kipindi cha Aprili na Juni za ujenzi wa madarasa, milioni

ileile 20, na sasa hivi kiwango cha ujenzi wa darasa moja ni milioni 20. Naiomba Serikali iliangalie hizi kupanda kwa bei ili isikwamishe utekelezaji wa hizi pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli katika suala zima la mwaka wa fedha huu unaoendelea, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Waziri, mchango wa trilioni moja na bilioni 300 kuchochea uchumi katika maeneo mbalimbali. Mkoa wetu wa Pwani umepata zaidi ya bilioni 17, haijapata kutokea. Kwa hiyo, naomba nimshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hasa sekta ambazo zimeainishwa ni zile zinazompa fursa mwanamke kupata muda wa kujishughulisha na masuala ya uchumi. Imeshughulishwa sekta ya maji, mitambo ikinunuliwa na visima vikichimbwa maana yake wanawake watapata fursa ya kujishughulisha na shughuli za uchumi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipa fursa. Lakini niseme tu kwamba...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nahsukuru sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kutoa maoni yangu katika mpango ujao. Lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu, kipenzi

chetu, kwa kazi nzuri anazozifanya, kwa dhamira yake ya dhati ya kuifungua Tanzania kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nishukuru kwa shilingi trillioni 1.3 ambayo kwa Jimbo la Meatu kwa trillioni 1.3 tumpata bilioni 2.6 ikiwepo miradi ya elimu, afya na maji. Lakini ukiongeza na fedha zingine ndani ya miezi mitatu, miradi ya barabara Jimbo la Meatu katika miezi mitatu tuna bilioni sita. Na kama watendaji wetu watakuwa na dhamira ya dhati ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, dhamira ya dhati kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Meatu, ndani ya muda mfupi Jimbo la Meatu linakwenda kubadilika kwa muda mfupi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze katika mpango wetu, nianze kwa kuunga mkono hoja ya Serikali, lakini niunge mkono hoja maoni ya Kamati ya Bajeti ambayo ni Mjumbe na nimpongeze Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Daniel Sillo, kwa namna anavyotusimamia katika Kamati yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali inatarajia kuongeza makusanyo kwa asilimia 7.4 ikilinganishwa na mwaka 2021/2022. Kazi kubwa iliyopo mbele ya Serikali ni namna gani hizi asilimia saba tunaweza kuzifikia. Na Serikali imeweka msisitizo kuhakikisha kwamba mapato yote katika Wizara na taasisi za Umma yanaendelea kukusanya kupitia mfumo wa *GEPG*, lakini katika utekelezaji wa mpango huu unaoendelea, Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 20 amesema kwamba kuna uvujaji mkubwa wa makusanyo ya maduhuli ya Serikali kwa Serikali za Mitaa na ulegevu wa matumizi ya *EFD*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ninapenda niiambie Serikali, pamoja na kuzisema Halmashauri za Serikali za Mitaa, bado kuna taasisi 72 za Serikali ambazo hazijaanza kutumia mfumo wa *EFD*. Matokeo yake taarifa zake, takwimu zake haziwezi kusomwa katika mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali itoe mkazo na msisitizo kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali

zinajiunga na mifumo iliyoidhinishwa na Serikali kwa kuwa Serikali imetumia fedha nyingi kutengeneza mifumo hiyo. Hata kama tukisema taasisi hizo zipewe mitaji na Serikali, lakini pia kunakuwa na udhibiti katika makusanyo ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeendelea kupokea fedha za mikopo ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Naunga mkono hoja ya Kamati kwamba miradi yote inayotekelawa kwa muda mrefu itumie mikopo ya muda mrefu ambayo ina masharti nafuu ambayo inaiva ndani ya miaka 10 ili iweze kuleta faida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali pia katika miradi ya aina hii, inayotekelawa kwa muda mrefu ambayo inahitaji fedha nyingi itekelezwa kwa uchache. Inavyotekelawa kwa uchache inatoa fursa ya kuweza kukamillishwa kwa wakati na kuanza kuleta faida ili iweze kusaidia kuchangia kurejesha mikopo na kuweza kusaidia deni letu liendelee kuwa himilivu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, ipo miradi mingi iliyotekelawa kwa kutumia mikopo, kwa mfano; daraja jipyia la Selander alimaarufu kama *Tanzanite Bridge*. Miradi ya aina hii na mingine inayoonesha fursa ya kuweza kukusanya ushuru, naunga mkono hoja ya Kamati kwamba Daraja la *Tanzanite* litakapokamilika liweze kutumika kutozwa fedha kwa sababu kuna njia mbadala ambayo mwananchi ambaye ataona hawesi kutoa ushuru atatumia njia nyingine, kwa sababu taarifa tulioipokea ni kwamba magari mengi yanapita takriban kwa wastani magari 5,000 yanapita kwa siku katika barabara ile ya zamani. Kwa hiyo endapo kama asilimia kidogo au 25 au 30 itatumia *Tanzanite Bridge* kwa kutumia tozo, Serikali inaweza ikaingiza fedha ambayo itasaidia pia kuongeza katika kurejesha mikopo yetu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage na Mheshimiwa Almas Athmani Maige ajiandae.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2022/2023. Kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii.

Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoendelea kuifanya kwa Nchi yetu ya Tanzania. Mwenyezi Mungu amwongezee maisha marefu. Amina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwenye vipaumbele vya Mwongozo wa Mpango huu ambao tunauongelea na sana sana nitajikita kwenye vipaumbele viwili kati ya vipaumbele vitano. Navyo ni vile vipaumbele vinavyogusa kilimo. Nitaongelea kilimo tu. Nikisema kilimo ni zile sekta ambazo ni kama hazipewi kipaumbele, kwenye kilimo naongelea kilimo, uvuvi pamoja na mifugo. Hizi sekta ni za uzalishaji, lakini ukiangalia kwa kweli hazipewi kipaumbele na ningependekeza kuwa kwenye Mpango unaokuja zipewe kipaumbele namba moja kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea kilimo, wananchi wote asilimia 100 wanategemea kilimo kwa upande wa chakula, nyote humu ndani mmekula, kama hujala utakula, hiyo yote ni kilimo. Wafanyakazi wanakula, wanunua chakula kinachotoka shambani, hiyo yote ni kilimo. Asilimia 66.3 ya Watanzania wanategemea kilimo kama ndiyo ajira yao na ndiyo uchumi wao, lakini bado hatujakipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa upande wa asilimia kwa kukua kwa kilimo ni asilimia tatu mpaka nne tu, hii kwa kweli inasikitisha kwa sababu kwa ninil kwa sababu hakuna uwekezaji, lakini tungakuwa tunawekeza kwenye kilimo kingekuwa na chenyewe kinakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo chetu kinachangia asilimia 26.9 ya pato la Taifa, lakini bado hakipewi kipaumbele. Naomba mwaka huu katika Mpango huu na kwenye bajeti inayokuja ya 2022/2023, kipaumbele namba moja kiwe kilimo. Tukiweza kuwakwamua wananchi wetu wanaoishi huko vijiji na mijini wanaotegemea kilimo, ndio tutaweza kutoa umaskini na kuleta ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi humu Bungeni wanawakilisha asilimia kubwa ya wakulima huko wanakotoka kwenye majimbo yao. Wabunge wengi humu ndani zaidi ya asilimia 60 na wenyewe ni wakulima. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuungane na Serikali, tuiambie Serikali kilimo iwe kipaumbele namba moja, ndio tutaweza kuondoa umaskini na kuweka ajira kwa Watanzania wetu na vijana wengine na akinamama ambao tunategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa nini? Maazimio ya Malabo, tuliazimia kuwa asilimia 10 ya bajeti nzima iende kwenye kilimo, lakini sasa sisi bado hatujafika popote kwenye maazimio haya ya kilimo, bado bajeti ipo chini.

Naungana na Kamati ya Bajeti kwa mambo yote waliyoyasema kuhusu kilimo. Hongera sana kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa mambo yote waliyoyaongelea. Wameongea na Kamati yangu ya Kilimo nikiwa Mwenyekiti *I declare the interest*, tumeongea kuhusu mambo ya Bajeti, kuwa bajeti ya kilimo iweze kupandishwa. Bajeti ya kilimo kwenye upande wa Kamati ya Bajeti ambayo nimeisifia na kuipongeza, wamesema Bajeti itoke kwenye bilioni 250 ya mwaka uliopita iweze kufikia angalau bilioni 450. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu na mimi mwenyewe, nasema bado na hiyo ni kidogo, iweze kupanda zaidi ya hapo, ikiwezekana iende kwenye bilioni 500 kwa kuangalia Mpango wetu ambao unategemea kuwa mazao ya kilimo ndiyo yanalisha na viwanda, malighafi za kilimo ndiyo zinazolisha viwanda yetu. Sasa tunasema twende na dhima hiyo ambayo inasema kuwa tuweze kuwa ina viwanda, lakini je, viwanda vitatoka wapi kama hatuna mazao ya kilimo? Lazima tuweke kipaumbele kwenye kilimo kwenye uzalishaji, uzalishaji ndiyo namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mambo haya ya uzalishaji kuna mambo mengi...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Sijui hiyo ni kengele ya pili au ya kwanza.

MWENYEKITI: Ya pili.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, lakini kubwa ninalosema, bajeti ya kilimo ipandishwe juu, ndiyo tutaweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Charles John Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Athmani Maige na Mheshimiwa Samwelii Hhayuma Xaday ajiandae.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia mada iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, lakini niipongeze Mamlaka, niipongeze Serikali kwa jinsi tulivyoweza kupita kwenye rejea mwaka mzima, wakati nchi nyingine zina uchumi hasi, sisi tumekuwa na uchumi chanya. Watu wanakula, kazi zinafanyika, hili ni

jambo kubwa sana, inatosha kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuchangia kwenye kuboresha vipaumbele vya Mpango na nini tufanye. Jambo moja tunapaswa kufahamu, huu ni Mpango wa Mwaka wa Pili katika miaka mitano ya Mpango wa Tatu wa miaka mitano mitano. Tatizo la miaka mitano hii, ndiyo miaka mitano inayokwenda kutupeleka kwenye kilele cha Dira ya Taifa. Sasa tatizo tulilonalo, yaani ndiyo tunafika fainali hivyo, tunafika fainali ambako tunategemea kuwa tumeondoa umaskini, ile biashara ya *income ya per capita* ya Dolla 3,000, lakini tunafika finali katika linge lengo la kujenga uchumi imara wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapozungumza kuondoza umaskini ina maana unalenga uchumi jumuishi, wengine wanaita uchumi shirikishi, hapo mimi Kiswahili kinapingana. Uchumi jumuishi, yaani tunataka tufike kwenye uchumi wa kat, Watanzania wote tusiwe tumeachana sana, siyo kushiriki. Unawenza kwenda kwenye harusi ukamwona bibi harusi kule umeshiriki, lakini kujumuika ni kumtunza na kuhanganya naye yule bibi harusi, hapo umejumuishwa. Sasa kuwajumuisha Watanzania wote, lazima Watanzania wote washirikishwe, wajumuike wapate huo uchumi, ndipo inapokuja tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia dhima ya Mpango wa Pili wa Miaka Mitano ulilenga kwenye miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi. Ndiyo hii sasa Mheshimiwa Waziri ameibeba tena ikawa vipaumbele vya Mpango wa Tatu. Vipaumbele vya Mpango wa Tatu vilipaswa kulenga zaidi shughuli za kiuzalisha (*the productive sectors*) hajazzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipotoka, huko nyuma sawa kwa sababu miradi haikukamilika, sawa aje nayo, lakini sasa anapofika hapa kuna wenye shughuli, tunajenga reli, reli inapaswa isafirishe bidhaa, isafirishe maziwa, yapo wapo? Inapaswa isafirishe

matunda, yako wapi? Kwa hiyo lazima *productive sectors* ziweze kushughulikiwa na *productive sectors* ndizo zitatengeneza ajira, ndiyo zitalisha viwanda na ndiyo zitajenga uchumi wa nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeki, unapozungumza uchumi imara, unazungumza uwezo wa nchi kuuza nje. Tanzania tuna mapungufu yetu tunapaswa tuyaangalie, kama walivyosema Wabunge wengine kwa kujilinganisha na nchi nyingine. Wamezungumza Uganda, kahawa Uganda wanauzu Dola milioni 500 kwa mwaka, sisi 135, lakini sisi tuna *potential*, tuna ardhi tunaweza kwenda juu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri katika Mpango wetu unapokuja tutengeneze jedwali la kuangalia kila sekta inaweza kutuletea nini. Hatari tulio nayo, mapato yetu ya Taifa kwa fedha za nje kwa kiasi kikubwa inategemea uziduaaji. *Two third* ya mapato yetu yanategemea dhahabu na madini ambayo ni hatari, ni kipato kwa Taifa, lakini siyo jumuishi. Kwa hiyo tunapaswa tuwekeze kwenye shughuli za ujumuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu. Jambo la kwanza kwenye Sekta ya Mifugo, lazima Serikali iwekeze zaidi katika kuhakikisha kwamba wafugaji wanaacha kuhamahama. Huwezi kujenga Sekta ya Nyama na Maziwa kwa watu wanaohamahama na ili kudhibiti hilo lazima Serikali iweke fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kwa upande wa kilimo, sisi Tanzania tuna hekta milioni 29 zinazofaa *irrigation* na tunalima *0.4 million hectares*, Serikali wawekeze, waweke fedha, kama Mwalimu Nyerere alivyojenga Mbarali, waweke fedha nyingi watu walime halafu wawaachie, halafu watengeneze Mfuko wa kuwalipisha wale watu ili tuachane na kilimo cha kutegemea kudra za Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kitu kingine, ningependa nishauri, limezungumzwa suala la mbolea litatusumbua sana. Nimewahi kulizungumza, naishauri Serikali, juhudzi za kuweza kutengeneza Kiwanda cha Mbolea lisisubiri, achana na visima vyenye *well and bottleneck*, waende

wakachimbe visima vingine. Bahati nzuri Sekta ya Nishati naona wamewarudisha wakongwe wa mafuta akina Mzee Halfani wanarudi, wanajua gesi ilipo, waende kuchimba visima tutengeneze gesi, hii bei itapanda na kushuka na kupanda na kushuka ndiyo historia ya gesi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nalifurahia, Serikali wameanza kuzungumza suala la Bagamoyo, wamefanya kazi ya Bagamoyo, waizungumze, siyo siri, tuzungumze Bagamoyo kama *Industrial City*, tuzungumze Bagamoyo kama Bandari, tuzungumze Bagamoyo kama *Logistic Centre*. Wamezungumza suala la *DRC Congo kwamba Tanzania mnataka kuwa njia, unapotaka kuwa njia lazima uwe na uwezo wa kupokea Panama Versal*, uwe na uwezo wa kupokea meli kubwa ziweze kuja hapa. Nalipendekeza hilo waliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni mradi wa ajira. Ziko nchi duniani zimeendelea kwa kukopa na kuwaajiri watu. Hizi Sekta za Uzalisha, *Productive Sectors* hazina wafanyakazi, tusione aibu kwenda kukopa. Jambo moja la faida, *Productive Sectors* ukikopa ni malipo ambayo utayaona katika kipindi kifupi. Ukichukua *model/ya Swaziland ambaowana ng'ombe laki sita, sisi tuna ng'ombe milioni 33.9, wao wanapata Dola milioni mbili Dola export kwa extrapolation* sisi tunaweza kupata Dola karibu milioni 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiwekeza kwenye sekta hizi unakopa na katika kipindi kifupi unaweza kupata mapato. Kwa hiyo, pamoja na hii miundombinu wezeshi na saidizi, sasa tunapaswa kutupa kwenda kwenye *Productive Sectors*. Hata hivyo, jambo la muhimu twende tukope, tuajiri watu, watu wafanye kazi. Kwa sababu watakapofanya kazi utaweza kupokea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine nitawasilisha kwa maandishi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Athuman Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer*

Samweli Hhayuma Xaday na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu ajiandae.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie Mapendekezo hayo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa ajili ya Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Kwanza nitoe shukrani, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupa fedha nyingi sana jimboni kwetu za madarasa, barabara lakini pia za hospitali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango sasa, ndugu yangu Mheshimiwa Mwijage amesema vizuri na Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kilimo, sisi tunachangia kilimo. Sekta ya Kilimo ndiyo inayofanya tuseme, tuongee hapa. Kilimo kimekuwa na kauli nyingi sana; Kilimo cha Kufa na Kupona, Siasa ni Kilimo na Kilimo ni Utii wa Mgongo, lakini leo naona uti wa mgongo hauna mfupa, huu kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisemee mambo machache ambayo ni muhimu sana. Kilimo cha kwetu kinadumaa na kama kilimo kinadumaa na kinaajiri zaidi ya watu asilimia 75. Kwa hiyo watu wote huko vijijini hali siyo nzuri. Sababu kubwa ni uhaba wa mbegu, ukosefu wa mbolea, lakini vile vile bei kubwa ya mbolea na bajeti ndogo ya Serikali kwenye kilimo. Niwakumbushe tu kwamba bajeti ya mwaka jana ilikuwa asilimia 0.8 ya bejeti ndiyo kilimo, lakini pia tumetekeleza skimu zote za umwagiliaji lakini pia ukosefu wa watalaan wa kilimo, Maafisa Ugani Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kina mchango mkubwa sana kitaifa. Moja, kilimo kinatoa ajira kwa wananchi zaidi ya asilimia 75, lakini kinachangia bajeti asilimia karibu 27, lakini pia malighafi viwandani na chakula kwa Watanzania wote, kilimo ni kitu muhimu sana. Ili niweze kuchangia na niwe mkweli ningependa kupendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Fedha na Mipango ije na Mpango mzuri wa kujenga Viwanda vya

Mbolea. Ili tuweze kupunguza bei kubwa ya mbolea lazima tuwe na Viwanda vya Mbolea hapa nchini, tulikuwa nacho kimoja huko Tanga kimekufa, Kampuni ile *TFC* haina kazi yoyote. Kwa hiyo, tunahitaji viwanda vya mbolea nchini, sisi tuna malighafi zote za kujenga viwanda vya mbolea hapa, gesi tunayo, lakini pia malighafi nyingine zinapatikana. Ndiyo maana watu kutoka Burundi wanakuja kujenga Kiwanda cha Mbolea hapa na hawaleti malighafi kutoka nje. Malighafi ipo hapa, tujenge Kiwanda cha Mbolea ambacho kitafanya mbolea ipatikane. Kwa wale ambao hawafahamu mbolea iliyopo nchini sasa ni asilimia 35 haizidi 40, lakini pia bei zake wananchi hawawezi kununua mbolea kwa bei ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, umefika wakati ni lazima tupange ardhi ya kilimo. Sasa hivi ardhi haijulikani ipi ni ya kilimo, tumepanga ardhi ya wanyama, *National Games*, maeneo oevu, lakini kwa kilimo, haiwezekani akaja mkulima mkubwa sana anataka Tanzania tumpe ardhi iko wapi? Haijawa *demarcated*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda basi, kama inashindwa kuwa *demarcated*, Serikali irasimishe mashamba ya wakulima wadogo wadogo kama ardhi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni kilimo cha umwagiliaji. Hatuwezi kutoka kwenye kilimo cha kutegemea mvua? Sasa hivi tunaambiwa mvua haitoshi, lakini mabwawa yapo yamejaa maji. Tungekuwa na skimu za kumwagilia zinazojulikana, siyo kumwagilia kwa mitaro, mashine kubwa zimwagilie mashamba ya kisasa. Tunaweza tukapanga kiasi gani tutavuna kwa mwaka kwa kutumia umwagiliaji. Siyo mvua hainyeshi, mwaka huu hatupati. Nashauri kilimo cha umwagiliaji ni jambo muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni kuongeza bajeti. Bajeti ya Serikali ya 0.8 kwa mwaka kusaidia sekta ya kilimo haitoshi kabisa. Napendekeza na watu wote duniani wanasema lile Azimio la Maputo, lilisema Serikali iweke asilimia 10, iwe ndiyo kwa ajili ya kilimo. Sasa mimi napendekeza hata twende 5% siyo 0.8%, hatuwezi kuwa na kilimo bora.

La mwisho ni Benki ya Kilimo. Tunayo Benki ya Kilimo hapa nchini. Hii benki haifanyi kazi yoyote kusaidia kilimo, haionekani popote katika ushiriki wake wa kujenga au kuongeza tija ya kilimo. Inakopesha watu na imekuwa tu ni wakala wa mabenki ya biashara na ili wananchi wachache wajanja wajanja waweze kukopa, lakini wakulima wadogo wadogo ambao benki hii ilikuwa imekusudiwa kwenda kuwasaidia, haionekani kabisa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nchi nzima hii ina ofisi moja tu kwenye hii benki ya kilimo. Haionekani mikoani kote wala kwa wakulima. Imekuwa tu Wakala kwamba unataka kwenda kukopa *CRDB*, unataka kwenda kukopa benki yoyote ile, sijui *NMB*, wao ndio wanakuwa *brokers*, wanasema wanaweka dhamana. Benki ya Kilimo ichukue jukumu lake na Serikali isaidie kuipa fedha nydingi Benki ya Kilimo ili iwakopeshe wakulima wadogo wadogo kuongeza tija. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo suala lingine dogo nje ya kilimo ambalo ni *REA*. Mradi wa *REA* ni muhimu sana, unaleta maendeleo makubwa vijiji, lakini utekelezaji wake umeanza kuwa na matatizo. Wanajenga halafu vijiji vingine wanaruka. Wale wananchi ambao wanarukwa vijiji vyao wanakuwa wanyonge sana. Wanakosa raha, wanakuwa kama siyo Watanzania. Tumefanya mikutano na watu wa *REA*, wale Wakandarasi wanasema wao wamepewa *BOQ* ya nguzo 20 kwa kijiji kimoja. Sasa kuna kijiji cha pili yake labda nusu kilomita wanakiruka, waya za umeme zinapita kwenda kuweka umeme kijiji kingine kinachofuatia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa kasoro kubwa sana ambayo inaleta chuki kwa wananchi wetu na viongozi. Vile vile, suala hili linafanya wananchi wengine wawe na matabaka kati ya wananchi wengine; hapa pana umeme, umeme huo unaruka mahali fulani. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Nishati... (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kengele ya pili imeshagonga.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Eng. Samweli Xaday Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, ajiandae.

MHE. SAMWELI X. HHAYUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia, kwenye mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Awali ya yote niungane na wenzangu ambao wametangulia kwenye kumshukuru na kumpongeza sana Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa fedha ambazo ametupatia kwenye maeneo yetu hasa kwenye eneo la elimu, afya, maji, umeme na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha vizuri Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2022/2023. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nakupongeza wewe na Mheshimiwa Spika kwa jinsi ambavyo mnatuongoza vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wenzangu ambao nafanya nao kazi kwenye Wilaya yangu ya Hanang kwa ushirikiano ambao wanani patia. Ushirikiano wao ndiyo uliowezesha Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kuongoza Kitaifa kwenye makusanyo ya mapato. Hii imewezekana tu kwa sababu viongozi tumeshirikiana kuanzia Mkuu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi, Waheshimiwa Madiwani na viongozi wengine, pamoja na watendaji wa Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza Wana-Hanang kwa jinsi ambavyo wanatuwezesha sisi kutekeleza majukumu yetu vizuri, sana sana wanaotuunga mkono kwenye ukarabati wa Hospitali ya Wilaya Tumaini, ambako tuna bajeti ya zaidi ya shilingi milioni 200 na mpaka sasa karibu bajeti yote imepatikana ya kukarabati Hospitali ya Wilaya. Ninawashukuru sana kwa jinsi ambavyo wamejitoa, ninaamini Serikali itatuunga mkono; kuna upungufu wa majengo pale, tutapata yale majengo ambayo yanapungua ili angalau, huduma za afya ziweze kutolewa vizuri kwenye Hospitali yetu ya Wilaya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie kwenye Mpango huu. Tumesema mara nyingi kwamba kilimo ni uti wa mgongo na tunesema na hata kwenye Mpango imeandikwa kwamba, asilimia zaidi ya 66 ya wananchi, wanategemea ajira zao kwenye kilimo, lakini ukienda kwenye maeneo ya vijiji ni zaidi ya asilimia 90 watu wanategemea kilimo na ndio wengi wapo huko. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, bila kuwekeza kwenye kilimo hatutapiga hatua. Tumekuwa na dhana na matamko mbalimbali kwenye eneo la kilimo. Tumekuwa na Kilimo Kwanza na matamko mengine kama hayo. Sekta hiyo inaaajiri watu wengi. Ukiangalia wananchi au vijana wengi, wanaokimbia vijiji ni kwenda mijini, ni kwa sababu kilimo hakina tija. Ili tupate tija kwenye kilimo, ni lazima tuweke fedha za kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tupate wataalam watakaosaidia wakulima wetu kulima kisasa ili tupate tija kwenye kilimo. Tupate wataalam wa mifugo ambao watasaidia wafugaji ili angalau ufugaji upate tija. Bila kuwekeza kwenye kilimo kimkakati, bila kukiangalia kilimo na tukawa tunaweka fedha kidogo kidogo, hatutakwenda kokote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mambo mengi tunayoyafanya, tutakuwa tunaangalia sehemu ambazo zinaajiri chini ya asilimia 30 ya Watanzania. Kilimo chetu kina

changamoto nyingi; kilimo kinategemea mvua. Ni lazima tuwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tumeongea na tumeahidi kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwamba tutatafuta mbegu, pembejeo, viuatilifu vya bei nafuu, lakini hali kwa sasa ni mbaya kwa wakulima wetu, lazima tuangalie eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunayo mashamba makubwa kwenye nchi yetu ambayo mengine tumeyabinafsisha. Tunayo sababu ya kuangalia ufanisi wa hayo mashamba ili hatimaye pia hayo mashamba ambayo tumewapa wawekezaji ambao inawezekana hawana nia au hawana uwezo wa kuwekeza; tufanye tathmini ya kina, mashamba yale ambayo tunaona hayana tija kabisa, tuyatwae ili kuyapangia matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima tuwekeze kwenye suala la kufanya uchakataji wa mazao yanayozalishwa na wakulima wetu, ikiwepo kwenye upande wa kilimo na upande wa ufugaji ambako ndiko kuna wananchi wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu Mpango ambao tunaenda nao, lazima tuangalie sana eneo la miundombinu ya barabara za vijijini, kwani kule wakulima wakilima, mazao yale lazima yasafirishwe na kuwe na usafiri wa uhakika. Kuna maeneo mengine kwenye nchi yetu na hasa Jimbo langu la Hanang, mvua zikinyesha safari ndiyo imeishia hapo. Hakuna kwenda kupata huduma za kiafya, hakuna shughuli za kimaendeleo inayoendelea, mazao ya kilimo hayasafirishwi na tunatakiwa lazima tuwekeze kwenye eneo hilo. Tuwekeze kwenye uchakataji ambao hatimaye pia tutaleta ajira za kutosha kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiboresha kilimo bila kuboresha miundombinu hakuna kitu chochote cha maana ambacho tutakifanya. Lazima tuhakikishe kwamba tunaboresha upande wa bandari, tuboreshe viwanja vyetu vya ndege. Kwa mfano, Mkoa mzima wa Manyara pamoja na ukubwa wake wote, hauna hata kiwanja kimoja cha

ndege. Ipo kwenye Mpango muda mrefu; Kiwanja cha Ndege cha Mkoa wa Manyara. Itakuwa rahisi watu kufanya shughuli zao kama kweli kuna usafiri wa ndege unaoflikka kwa urahisi Mkoani Manyara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna barabara yetu ambayo inaenda kwenye mashamba yenyе uzalishaji mkubwa wa ngano. Barabara ya kutoka Mogitu kwenda Haydom, kule tunazalisha ngano ya kutosha; shayiri pamoja na ngano ya chakula. Ile barabara ikitengenezwa itawafungulia wananchi fursa kubwa sana ya kusafirisha mazao yao na kupata tija kwenye eneo la kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020 wakati tukiwa kwenye Mpango na kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Rais, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, alisema yale ambayo tunaweza kuzalisha ndani ya nchi, tuzalishe na tuondoe nakisi hasa kwenye ngano ya chakula lakini na mazao mengine ambayo tunaweza kuyazalisha nchini kwa wingi, tusiagize nje ya nchi. Kwa mantiki hiyo, uwekezaji ule ambao ulifanywa kwenye ngano ya chakula, shayiri mwaka 2020, bei ilikuwa ya uhakika na wananchi waliingia mikataba ya Kilimo cha Shayiri. Mwaka huu kidogo inasuasua. Wizara ya Kilimo iangalie eneo hili ili angalau wananchi wapate mikataba ya kulima shayiri na ngano ya chakula na uzalishaji uwe wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mpango huu wa mwaka 2022/2023. Pia nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wengine kuendelea kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan

kwa namna ambavyo anajali sana hali za wananchi wetu, hasa kwa kuangalia kuwekeza kwenye elimu, afya, maji na miundombinu ya barabara. Tunamshukuru sana na tunamwombea Mungu aendelee kumpa afya na hekima katika kuliongoza Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomshukuru Mheshimiwa Rais naomba pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha anapoandaa hii Mpango, kwa kuwa Mama sasa ameshafanya lile jukumu lingine ambalo lilikuwa ni madarasa na sehemu nyingine, kwenye afya na vituo vya afya, basi awe anatuletea pia na taarifa ya yale mengine tuliyoyapanga sisi wenyewe humu ndani, yanakwenda vipi? Zile chenji za fedha ambazo zingebaki au zilitakiwa zitumike, hazijatumika, zimeendaje? Tunaomba hilo tuwe tunaambwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha awe anatuambia pia, katika Mpango huu aliousoma na Kamati ya Bajeti imeelezea kwamba, kuna wakati fedha hazikupelekwa *MSD* kwa sababu ya wizi uliokuwa unatokea pale *MSD*. Basi tuwe tunapewa pia mrejesho, chenji, wakati ule walipozuia zisiende; zile ambazo zilizuiwa ziko wapi? Au zimefanya nini? Itakuwa ni vizuri sana tukijua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia Mpango huu, moja kwa moja kwanza, nichukue fursa hii kuuelezea Mpango wenyewe na kuangalia kwamba Mpango huu ndiyo mwanzo, ukiwa ni mwendelezo wa Mpango wa Miaka Mitano ulioanza mwaka 2016/2017, ambao unaisha mwaka 2021 na sasa tunaingia Mpango mwingine wa Miaka Mitano. Katika vipaumbele vya ule Mpango wa nyuma, mojawapo ilikuwa ni kukuza uchumi na kuendelea kujenga msingi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoongelea msingi wa uchumi wa viwanda, huwezi kuacha miundombinu ya barabara, miundombinu ya umeme, vile vitu ambavyo vitachochea kukua kwa uchumi. Sasa nimepita katika Mpango na tuna miradi yetu ya kimkakati na tuliposema ni miradi ya kimkakati, maana yake ni miradi ile ambayo

inajenga msingi ambao utakuza uchumi wa viwanda.
(Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunasema miundombinu ya barabara, miundombinu ya reli na mambo ya umeme. Sasa tuna barabara na tuna miradi ya kimkakati ambayo sehemu nyingine ilikuwa inatupelekea kuingiza mapato zaidi au kuongeza pato zaidi la Taifa ambalo lingeweza kufufua sekta nyingine za viwanda. Kwa hiyo, tuna barabara kwa mfano, tuna miradi ya utalii kama ambavyo katika Mpango wake anasema; kukuza utalii ili kuongeza pato la Taifa na tunajua llani ya CCM inatutaka tuongeze pato la Taifa kufikia dola bilioni sita ifikapo mwaka 2025. Pia tuongeze watalii wafike milioni tano ifikapo mwaka 2025 na tunategemea sana kutanua uwanda wetu wa utalii ikiwepo utalii Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mbuga kubwa ambayo ni ya pili Afrika ambayo ni Ruaha *National Park*. Tunaposema utalii wa kusini, unachukua Mikoa yote ya Kusini. Tunaiona Katavi, tunaangalia Kimondo cha Songwe, tunaangalia Njombe Kitulo, tunaangalia *Selous*, tunaangalia ule utalii wote wa kusini pamoja na Ruaha yenyewe. Sijaona kama Serikali imeweka kwenye Mpango suala la kutengeneza barabara zinazoingia kwenye ile Mbuga. Zaidi sana naona shilingi bilioni 90.2 ambayo itashughulika na miundombinu kufidia hasara zilizotokana na Uviko kwenye Mashirika yale yale ya Utalii kama *TANAPA* na wengine, lakini hatuoni Mpango ukituambia kuna kutengeneza zile barabara zinazoingia kwenye ile Mbuga ili watalii wanapofika waweeze kuingia kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ile kuanzia Iringa, kilomita 104 kuelekea Ruaha. Tuna barabara nyingine ambayo inaanzia Iringa pia inaingilia Idodi Jimbo la Isimani huko. Hatuoni kama Serikali ina Mpango, zaidi sana waliweka Mpango wa kutengeneza madaraja. Sasa tunatengeneza madaraja wakati sehemu nyingine za barabara ni mbovu. Hii ni miradi ya maendeleo ambayo ingechochea uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine, tunaishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo inaonyesha uchumi wetu wa Tanzania, pamoja na athari za Uviko bado uchumi wetu umekua chanya. Tusipojiangalia, sisi ni nchi mojawapo katika nchi 11 zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo uchumi wake unakua kwa chanya. Nchi nyingine zote 33 zinakua hasi, ukiondoa Gabon na ile Afrika ya Kati ambayo uchumi wake ni zero. Sasa tusipojiangalia tulikuwa tunakua uchumi chanya, lakini tutakuja kupitwa na wale waliokuwa na uchumi hasi, kwa sababu ya (nitumie neno lile lile) utelezi ambao tunauweka wenyewe kwenye mipango yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kurudia hapa ni hiki hapa; moja ya sababu kubwa ya kufanya uchumi ukue hasi au kushuka kwa uchumi imeonekana ni Uviko na sababu zilizosababisha ni kufungwa kwa uzalishaji kwenye nchi nyingi kwa jina la kuaminika ambalo lilikuwa ni *lockdown*. Sisi Tanzania Mwenyezi Mungu alitusaidia tukiwa na Serikali yetu mahiri na shupavu, hatukuwa na *lockdown*, lakini viongozi wetu walifuatilia ile misingi ya afya tukaweza kuwa salama, tukaendelea na uzalishaji na uchumi wetu ukaendelea kukua katika hali ya kuwa chanya, siyo hasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kilichoathiri; kwa nini sisi tulikuwa tunaendelea na shughuli za uzalishaji? Kwa sababu, kwa kawaida pia linapotokea tatizo ni fursa, ni mwanya pia wa kuendelea kiuchumi. Kama ninyi ambao mtakuwa mmejipanga vizuri mnaendelea kuzalisha, mngeweza *kuwa-serve* wenzeni wengine ambao walikuwa wamejifunga.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru sana. Basi naomba kuunga mkono hoja. Mengine nitachangia kwa maandishi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, tutamalizia na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. SILLO D. BARAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo kwenye mapendekezo ya Mpango huu wa Taifa wa mwaka 2022/2023. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu, Mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya Taifa letu ikiwa ni pamoja na mapambano dhidi ya ugonjwa huu wa Uviko ambao tumepata mkopo wa masharti nafuu wa shilingi trillioni 1.3 ambao umesaidia sana katika maendeleo yetu mbalimbali katika nchi yetu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na timu nzima ya Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri na ushauri ambao imetoa katika Mapendekezo ya Mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nakupongeze wewe Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Spika kwa kutuongoza vizuri sana katika Bunge letu Tukufu. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano mkubwa sana kwenye Kamati ya Bajeti pamoja na kuleta mapendekezo ya mwongozo huu wa Mpango wa Taifa wa mwaka 2022/2023. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia maeneo machache, moja ni upande wa kilimo. Amesema Mheshimiwa Ali King kwamba ukitemewa mate na wengi, utalowa. Kilimo chetu kinachangia asilimia 26.9 katika pato la Taifa. Pia kilimo kinaajiri Watanzania zaidi ya asilimia 66. Vile vile malighafi za viwandani zaidi ya asilimia 60 zinatoka kwenye sekta ya kilimo. Kama tunasema kilimo kinachangia asilimia 26.9 ya pato la Taifa, maana yake Watanzania zaidi

ya asilimia 66 wanachangia asilimia 26 tu kwenye pato la Taifa. Kwa hiyo, maana yake, kwa kuwa kilimo kinaajiri Watanzania wengi zaidi, tulitarajia basi na mchango wa kwenye pato la Taifa ungekuwa mkubwa, siyo asilimia hii ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja kubwa sana ya Serikali kuwekeza kwenye sekta ya kilimo ili kuhakikisha kwamba inachangia vizuri kwenye pato la Taifa ambako pia itakuza uchumi, itakuza ajira na itaongeza wigo wa walipa kodi katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mapendekezo haya, namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika Mapendekezo haya ya Mpango huu tunaouandaa, Serikali iwekeze vyema kabisa kwenye sekta ya kilimo. Ninaamini kabisa tutakwenda kuondoa Watanzania kwenye umasikini na pia na kufikia dira ya nchi yetu ya mwaka 2025. Kwa hiyo, naomba sana kwenye Mpango wazingatie sana sekta hii ya kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni sekta ya afya. Naipongeza sana Serikali imewekeza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, tumejenga vituo vya kutosha, kuna hospitali za Halmashauri pamoja na zahanati katika maeneo yetu, lakini kuna upungufu wa rasilimali watu watumishi wa afya zaidi ya asilimia 53. Tumejenga majengo najua Serikali italeta dawa lakini hatuna wataalam wa kutosha, upungufu wa asilimia zaidi 53 ni kubwa sana. Kwa hiyo niombe kwenye mpango huu tunaouandaa sasa Serikali iwekeze vizuri kwenye kuajiri wataalam wa afya katika maeneo haya ambayo tumejenga vituo vya afya pamoja na zahanati na hospitali za Halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya maeneo ukienda unakuta zahanati ina nesi mmoja tu akiugua na huduma haitoki, kwa hiyo niiombe sana Serikali kwenye mapendekezo ya mpango huu sasa, iweke mkakati kabisa wa kuchambua na kuajiri hawa watoa huduma za afya katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ni sekta ndogo ya fedha. Unakumbuka mwaka 2018 Bunge lako Tukufu ililipitisha sheria pamoja na kanuni zake mwaka 2018 kuhusu sekta ndogo ya fedha, Kifungu cha 14 cha sheria hiyo killiipa mamlaka Benki Kuu kukaimisha usimamzi wa mikopo kwenye maeneo yetu kwa Serikali za Mitaa na Kifungu cha 54 cha Sheria hiyo kinamlinda mkopaji, waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakuwa mashahidi watu huko vijiji wanakopeshana, wafanyabiashara walio rasmi na wasio rasmi wanawakopesha walimu na wananchi wetu na kuwatoza riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu haijafanya vizuri kwenye eneo hili, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha isimamieni Benki Kuu sheria hii isimamiwe, sheria zinazotungwa na Bunge lako Tukufu zisimamiwe kama tunaona sheria haina manufaa kwa wakati huu tuifute, wananchi wanateseka hasa walimu na wakulima wetu kule vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuserma hayo nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha wazingatie maoni na ushauri wa Kamati, jana nilisema humu ndani kuna madini ya kutosha wasome wazingatie naamini kwamba watakuja na mpango mzuri sana na bajeti inayokuja ya mwaka 2022/2023 itakuwa nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Raisi kwa kazi nzuri anayoifanya, na mim ni mmojawapo wa watu ambao kwa kipindi chake tumeshanufaika na mabilioni ya Mheshimiwa Rais Samia. Nimepata madarasa siyo chini ya

sabini, lakini kwenye barabara nina zaidi ya Billioni Nne ni kazi kubwa sana, tunampongeza sana na tunamuombea aendelee kufanya kazi na kusaka pesa Watanzania waweze kufaidi Urais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba katika mpango unaoandaa hebu angalia ukamilishaji wa miradi. Tunakuwa na miradi mingi ambayo haifiki mwisho, ukiangalia kuna baadhi ya Halmashauri mpya zilipewa Billioni Moja za kujenga majengo na ramani ikaletwa ya ghorofa, leo tunamaliza mwaka hamna hela wala sioni kama kuna dalili ya kupewa tena hela ya kumalizia kwa kipindi kifupi, watu wameshamaliza majengo utakuta wengine wameweka na kenchi mbao zinaoza mirunda imeoza, ikija tena Bilioni Moja mnakuwa tena kama mnaaza kukarabati majengo upya. Kwa hiyo ninaomba katika mpango wako upange kukamilisha ile miradi ambayo Serikali ilikuwa imeianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo Mheshimiwa Waziri hata kwenye hivi vituo vya afya ulivyotoa pesa milioni 250 tutajenga majengo mengine yatafika renta na ramani mmeleta, mengine yatakamilika tutabakiza ukamilishaji, tena tunasubiri miaka miwili mitatu ndiyo unafikiria kutuletea, kwa hiyo ni vizuri ukatoa kama ni hizi chache mlizotoa zikamilishwe ziishe ili mwakani muanzishe nytingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza hapa kuna watu wengine humu ndani wana Hospitali za Wilaya bado hazijakamilika mpaka leo, kuna wengine pesa zao zilichukuliwa na mfumo wa Serikali ule wa mwezi wa sita mpaka leo Halmashauri yangu inadai milioni 290 mpaka leo, sasa tunaenda kuanzisha zingine. Kwa hiyo, ni vizuri mpango mzuri ni ule unaokamilisha na watu wanaanza kukitumia, tunaanzisha vitu tunasema vizuri majukwaani halafu kitu kinakuwa ni jengo halina huduma, haliwasaidi Watanzania na sidhani kama wanafaidika sana na hiyo mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine tunazungumza kukuza Shirika latu la Ndege, nimeona kwenye

mpango unataka tukushauri unajenga viwanja, Mheshimiwa Waziri, ninashauri tu naona hapa Dodoma hatujakaa vizuri, uwanja wa Dodoma unatumika mwisho saa 12. Ninyi wenyewe ni mashahidi ukiwa na kazi Dar es Salaam umeitwa Dodoma tunakimbizana kweli kuvizia ndege kila siku imejaa. Uwanja ule uliwekwa taa za kutua usiku lakini feki, kwanini msiweke taa ndege ikatua mpaka Saa Mbili, Saa Tatu, Saa Nne tukawa na *route* za usiku, tumefungiwa taa mpya mpaka leo zinamaliza mwaka hazifanyi kazi, bora kama tulipigwa famba na Mheshimiwa Waziri agiza taa tumalize uwanja huu uwanja wa kiuchumi, watu wanataka kuja kufanya kazi Dodoma wamalize mikutano Saa Mbili wakalale Dar es Salaam, haya ndiyo maisha Mheshimiwa Rais anasema nchi imefunguka kwa hiyo tufunguke vitu vyote siyo kufungua vitu nusu nusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumza kwa upole sana suala la wamachinga maana nikizungumza kwa ukali nitasemwa mimi siyo Mtanzania, lakini niliviyolisema mwanzo nadhani watu hamkunielewa. Nikishukuru sana Chama cha Mapinduzi kupitia Mwenezi wake alinisaidia, niposema niliambiwa mimi ni Mrundi siyo Mtanzania lakini Mheshimiwa Mwenezi wangu kwa sababu yeye ni mweupe nilitegemea alivyosema wangesema yeye ni Mwarabu, sasa kwa vile imekuwa ngoma *draw* nitalizungumza kwa upole sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka vijiji nami ni mkulima wa mpunga, tunavyozungumza leo gunia la mpunga ndani ya mwezi mmoja limeshafika Shilingi 90,000, mimi nimeuza jana shilingi 90,000 na wiki mbili tatu tulikuwa tunauza shilingi 40,000 hadi shilingi 50,000 nikawa najiuliza huu mpunga tunauza nchi gani ambako kumefumka njaa, hakuna! yaani mchele umepanda hapa hapa ndani kwetu nikajiuliza swali ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya *research* kulingana na akili yangu kidogo tu, kwamba walaji wa mchele sasa hivi wameongezeka, ukienda huko Njombe, Lushoto na sehemu zingine wauza viazi via chipsi wanalia

vinaoza hamna walaji! Kwangu nauza mananasi tulikuwa tumezoea ukipeleka mananasi Mjini wanunuwa machinga hawa wanakatakata wanawauzia watu Shilingi Mia Mbili, Mia Mbili, Mia Moja linanunulika, hakuna Watanzania wengi wanaoweza kununua nanasi la Shilingi Elfu Tatu au tikiti maji ambalo lilikuwa linauzwa kwenye kapu shilingi 500 sasa hivi hayanunuliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge niwaambie ukiondoa kama hatuna maisha ya Kibunge hata mimi naamini humu ndani Wabunge wenzangu kwamba kama Wasukuma wenzangu tunazaa watoto 10 - 15 bado Shangazi na nani wamekuja kukusalimia, unaweza kweli ukakaanga chipsi mkala mlo wa usiku, utaweza hiyo gharama za kuandaa chipsi? kwa hiyo watu wote wamerudi kwenye wali, tunakula tunabakiza na kiporo cha chai! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanasomesha wana watoto labda 15, wana Watoto watatu hata Dar es Salaam, mtoto anatoka Mbagala anasoma shule ya Uhuru, ulikuwa unampa elfu moja, maisha ni magumu elfu moja anakula chipsi kavu kwenye nailoni, sasa hivi machinga wote wamefurumshwa mnataka watu wakale kwenye *restaurant*. Kwa hiyo, ni vizuri mimi nililewa kabisa Mheshimiwa Rais alivyosema tukawaandalie mazingira mazuri, mazingira mazuri ni yapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo yameandikwa *public interest* labda mimi kwa sababu sijui kizungu yana kazi gani? Kwa mfano Mnazi Mmoja ile ipo wazi, *public interest* sasa hivi wamebaki kukaa mateja tu wavuta unga kwanini msiwaweke pale wamachinga, unamtoa mtu unampeleka Mbagala kwa hiyo ni vizuri Mheshimiwa Waziri tuchunguze vizuri kwamba tunawatoa watu tunawapeleka kule tunapobaki hapa tunaanzisha vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mimi nina duka Kariakoo nijitolee mfano nina siku ya Saba sijauza kila siku ninatuma nauli hapa, hebu jifikirie mfanyakazi wangu ambaye nilikuwa nampa elfu tatu posho ya chakula leo anatakiwa akale

restaurant chai Shilingi Elfu Mbili, mchana Shilingi Elfu Tano inakuwa Shilingi Elfu Nane nitaitoa wapi? Kama mnabisha Waheshimiwa Wabunge wewe nenda tu pale Kariakoo sasa hivi pale Congo, utaona kila anaefungua duka ana mfuko una *hotpot*, watu wanakuja na makande, watu wanakuja na wali wa kiporo, haiwezekani kuhudumia kwa sababu hatuuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakushauri sana Mheshimiwa Mwigulu, jaribu kuliangalia na bahati nzuri umenitaja nakushukuru maana wewe ni Waziri wa Fedha inawezekana una takwimu vizuri kwamba mimi ni tajiri, mimi ni zao la machinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinga wapo wa aina tofauti, kuna machinga mwingine anashinda tu mlangoni kupiga debe anakaribisha watu anapata elfu mbili, usiflikri watu wote wana mitaji na hao wenye mitaji ndiyo wanaowawezesa machinga huwezi kuwatenganisha, ukiwatoa machinga mtaa wa Congo biashara imekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaofanya *research* ni machinga, unataka unitoe Mwenge nikanunue Congo halafu nije nimepanda daladala, machinga akinunua Congo anakuja kwa miguu anauza barabarani, kwa hiyo ni vizuri hili zoezi tulichukue kwa uzuri. Hata ukiangalia nilikuwa napata takwimu za Mkao wangu wa Geita, vijijini tunataka kwenda kupiga watu Katoro kuwatoa machinga, hatuna mtaro wa maji, hatuna waenda kwa miguu, hatua yaani '*bagosha*'. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahala kwa kweli kwenye mpango naijiliza vizuri, mlitengeneza maandiko mazuri sana mkajenga stendi mkajenga masoko, chukua mfano soko la Kisutu, soko la kuku bahati nzuri kuku zinatoka kwa Waziri wa Fedha kwa Mwigulu, kuku ya Singida huko Kinampanda unaipeleka kwenye soko ya kioo na kigae, ikidonoa hivi inaumia mdomo, ikiangalia juu kuna taa hee! Zimeshindikana, ndiyo maana Rais anawaambia jamani haya masoko mengine tuyageuze yawe ukumbi wa starehe

hamumuelewi! Kwa nini msifanye hizi gharama za kuandaa stendi na masoko ya ajabu ajabu mkawekeza kwa wamachinga kuliko kuwatesa watu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli najiuliza mpaka kuna masoko mengine ambayo machinga tumeanzisha wenyewe, tunaenda kupigwa. Mfano Mwanza Nyamagana, kuna soko linaitwa Buhongwa kule barabarani watu wameenda wameanzisha miaka na miaka, leo eti unatengeza mazingira bora, unaenda unawatoa barabarani unawapeleka dampo wanapotupa vinyesi....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Musukuma muda wako umekwisha.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha umenipata vizuri kuhusu kuku.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya mimi kuwa mmoja wa wachangiaji lakini mimi leo nitachangia tofauti na watu wengi kidogo. Mimi nataka nizungumzie habari ya watumishi wa nchi hii hata sisi Wabunge ni watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ukweli tuzungumze ukweli bila ya kupepesa pepesa, hii ndiyo tutakuwa tunaisadia hii nchi, lakini kama kwenye ukweli tunaweka woga au kutozungumza ukweli wakati ukweli tunauona haifai. Sawa sawa na mtu unakaa na Rais hapa na Waziri Mkuu na Naibu Spika na Spika wanakuambia angalia yule farasi anapendeza kweli wakati wewe machoni kwako unaona yule ni punda, unatakiwa umwambie hapana huyu siyo farasi Mheshimiwa umekosea ni punda, lakini kwa ajili ya woga unasema aah! farasi mzuri kweli kwa ajili woga wako, hii hapana! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alishawahi kusema maendeleo ya nchi yaendane na maendeleo ya watu, huwezi kufanya maendeleo ya nchi bila ya maendeleo ya watu. Leo tupo kwenye mpango wa bajeti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha fanya maarifa yako ya aina yoyote 2022, ujue vyanzo utapata wapi sijui wapi lakini hakikisha mishahara ya watumishi inapanda wala tusidanganyane. Nchi hii imekuwa na hali mbaya watu wamezungumza maneno mengi sana, hela zimebanwa, hela hazipo, lakini mimi katika utafiti wangu nilichokuja kugundua bila ya watumishi kupandishiwa mishahara hali itazidi kuwa mbaya kwa watu wote, kuanzia hao machinga, makulima na watu wengine wote watakuwa na hali mbaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi ambao wakipewa pesa na inaweza ikasambaa kwa wananchi ni watumishi peke yake, huo ni ukweli wala tusidanganyane! Leo watumishi miaka sita, saba hawaajaongezewa mishahara mnategemea hela hiyo itakuwepo mtaani wakati vitu vimepanfa bei lakini mishahara ipo pale pale? Haiwezekani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo mnaongeza vi-percent viwili, vitatu, hakikisheni Serikali mnakuja na mpango muangalie mapato mtapata wapi, tumewaambia mapema mhakikishe watumishi wanaongezewa asilimia kubwa ya kutosha ili waweze kukidhi, watumishi ndiyo watumiaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi akitoka hapa anaenda Dar es Salaam njia nzima atanunua, akitoka hapa atanunua karanga, akifika Gairo atanunua viazi, akifika Dumila atanunua mahindi, akifika Mikese mpaka aje afike nyumbani laki moja kishapoteza, hawa ndiyo wanaosambaza pesa, ukienda hata sehemu za starehe ni watumishi ndiyo wanaosambaza pesa! Watumishi wakiongezewa pesa mjue kila kitu kwenye hii nchi kitakaa vizuri na pesa itaonekana, hii lawama ya kwamba pesa haipo mifukoni mwa watu, tusidanganyane eti Wakandarasi hawajalipwa, Mkandarasi nikiwa mimi Shabiby ukinilipa hiyo

hela yangu ya kuchezea nitagawagawa kwa kila mtu, nina wafanyakazi kumi hadi kumi na tano, watumishi wapo wangapi? Halafu tuangalie kodi ya nchi hii asilimia kubwa inalipwa na nani katika ya wafanyabiashara na watumishi, wanaolipa asilimia kubwa ni watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii naomba sana kwenye bajeti yako, Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunajua Mama yetu aliahidi lakini tumekupa mapema ili uangalie na vyanzo vyako utakavyovipata mishahara ipande asilimia ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Machinga alichozungumzia Ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma, naungana na Serikali katika mipango ya kuweka mji vizuri sana, kweli mji unapendeza vizuri lakini tukumbuke hawa machinga nao wakiwekewa mazingira mazuri wanaweza wakaleta mapato makubwa sana kwenye hii nchi, ni mazingira tu! Hivi leo mimi najiuliza hii Serikali hawa watu wataalam wetu wa Serikali wanapokwenda Vyuo Vikuu huwa wanaenda kule kujifundisha kumwagilia maua kwenye bustani au utaalam? Maana yake hata huelewi mtu ana akili timamu unaenda kupeleka majengo ya machinga kule llala ndani Shaurimoyo, kuna kibarabara kimoja hata mahali pa kufika hakieleweki, hamna stendi ya daladala unampeleka mtu kule, nani anaweza kufanya biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuiga nchi nydingine zilizoendelea? Dunia nzima tuangalie hata tuende pale Nairobi, majengo yote yaliyopo mijini ni ya Serikali, tukitoka hapo majengo yote ya *National Housing* yalikuwa ya Msajili wa Majumba haya yote ya kwetu, ukiangalia yale majengo makubwa ukichukua kodi wanayochukua Serikali lile jengo zima labda utachukua milioni Mbili au Milioni Tatu, lakini ukiyavunja yale majengo ya mijini hapa kama pale mtaa wa Congo, Msimbazi mpaka kule anakozungumza ndugu yangu hapa Musukuma, ukivunja yale majengo yale ya Serikali ujenge *Mallstena Shopping Malls* za ghorofa hazina gharama kwa sababu *Malls* zipo waziwazi halafu waingize watu.

MBUNGE FULANI: Au jangwani.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, au jangwani kokote pale, ndani lakini katikati ya Miji siyo ukampangie mtu huko katikati ya miji, hivyo mtaingiza machinga wangapi? kwa hiyo ni lazima kuwe na mipango tuchukue haya majengo ya Serikali tufanye kama Guangzhou - China, tufanye kama Dubai, tufanye kama nchi zingine, tuvunje yale majengo ya Serikali. Serikali ni yetu, Serikali ndiyo yenye machinga, Serikali ndiyo yenye watu wake, tuwajengee kwenye Miji katikati siyo kuziba barabara hapa, eti umchukue machinga ukamuweke sijui wapi huko hakuna hata stendi ya daladala nani atakaekwenda kununua? Unajua kuna vitu vingine tuzungumze ukweli siyo Mkurugenzi anapanga tu hapa ndiyo penyewe nimewajengea choo, sasa mtu anataka choo ataenda kuomba tu akibanwa huko hata porini ataenda, watu wanataka kupata huduma na wanaotaka kutoa huduma nao wanataka nao kufata watoa huduma na wapate faida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ushauri wangu ni kuhakikisha pale Msimbazi hebu angalieni majengo yale yote ni ya Serikali *National Housing*, ukienda kule mjini kote ni majengo ya Serikali, hivyo kweli wanaambulia tu kupata milioni mbili, tatu watu wamekaa kule majumba menyewe kupiga rangi wanashindwa, vunja yale weka *Malls*, weka ghorofa mbili, tatu, nne tena haina gharama kabisa, halafu machinga wakae mle, hapa msimbazi watakuwepo machinga, hapa sijui Lumumba watakuwepo machinga, hata katikati ya mjini kule karibu na hii *station* yetu ya *railway* tunayoijenga watakuwepo wamachinga, watu wata-enjoy, lakini hii kufukuzana halafu mpango hamna! Mimi nimeamua kutoa mpango kabisa ili kuelekeza mpango uweje sitaki kulalamika. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Na mishahara ya Wabunge!

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwingine hapa anasema mishahara ya Wabunge, hiyo utasema kesho hamna wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli ndiyo huo. Lingine, kabla dakika zangu hazijaisha, kweli watu wanajitangaza tu tunatoa mikopo kwa wakulima, kuna Mheshimiwa alizungumza hapa nafikiri, Mheshimiwa Almasi alizungumza kwamba zinajitoa benki na Mheshimiwa Waziri unaangalia na wewe tunakuamini sana na tunajua utalifanya kazi. Hizi zote zinakopesha matajiri...

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha Mheshimiwa Shabiby...

MHE. AHMED M. SHABIBY: Ah?

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipe dakika moja tu nimalizie.

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha!

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa Kamati imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa namna mlivyoshiriki kujadili andiko ambalo amelileta Mheshimiwa Waziri ambalo linatupa mwelekeo wa mawazo ya Serikali na tumeletewa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Katiba inataka tushiriki

kwenye jambo hili. Kwa hivyo, Serikali imeleta mapendekezo yake na sisi tunapata fursa ya kutoa mawazo yetu kwenye mapendekezo ya Serikali kwamba wakaboreshe kile ambacho wamekiletu.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao mmepata fursa ya kuchangia leo ninawashukuru sana kwa sababu mmeisaidia Serikali na wengine wataendelea kupata hizo fursa huko baadaye.

Mambo mawili, kwa sababu mambo yakishasemwa humu ndani yanaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. La kwanza ni hili alilolisema Mheshimiwa Shabiby hapo wakati tukimalizia na kwa mujibu wa Kanuni nisingeweza kusema tukiwa kwenye Kamati ya Bunge. Masuala la mishahara ya Wabunge hayajadiliwi hapa ndani, kwa hiyo, unaweza ukaliseema kwa masihara lakini hakuna masihara kuhusu jambo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, alishalitolea maelekezo. Kwa hiyo, tujadili mambo mengine, haya mengine nayo tufuate mipaka ile iliyowekwa.

Jambo la pili nimeletewa malalamiko hapa kuhusu muda unaotolewa wa Waheshimiwa Wabunge kuchangia. Nimeshawahi kutoa maelezo marefu kabisa namna ambavyo muda unatolewa hapa mbele. Lakini bahati mbaya sio Wabunge wote tunakuwepo hapa ndani kusikia nini kinazungumzwa na Kiti wakati wote.

Kwa hiyo, nirejee leo kwa kifupi, hapa mbele huwa kuna maombi ya Wabunge mbalimbali ambayo huwa yanaletwa na kanuni zetu mnafahamu zinavyotoa mamlaka kwa Mheshimiwa Spika na watu wote wanaomsaidia kuongoza na ndiyo maana Kanuni hizo hizo zinatambua kwamba kwa kuwa anayeongoza ni mwanadamu anaweza akafanya makosa. Akifanya makosa unatumia Kanuni ya 5 kupeleka malalamiko yako kwenye Kamati ya Kanuni. Huyo unayemlalamikia hatakuwa sehemu ya kikao hicho.

Kwa hiyo, kwa sababu sisi wote ni watu wazima ndiyo maana huwa tunakumbushwa. Yanapokuja maombi ya Waheshimiwa Wabunge na mnafahamu muda wetu ni finyu kuliko idadi ya Wabunge na kila Mbunge humu ndani ana haki sawa na mwingine kwa hiyo, hakuna namna Kiti au Makatibu watafanya kusudi ili wewe Mbunge fulani uonewe, hapana.

Kwa hiyo, yakinoteka makosa basi ni ya kibinadamu. Lakini, nieleze kwa siku ya leo, wako Wabunge ambao hawakuwepo kwenye orodha lakini kwa ajili ya majukumu waliyonayo wameomba kuchangia leo. Kwa sababu, na wao wana haki ya kuchangia na kama muongoza kikao inhabidi niwape pia fursa. (*Makofi*)

Sasa katika kuwapa fursa hiyo, siwezi kutoa tena sawasawa kwa kila mtu. Laini tukitaka kuliweka Bunge kwa mazingira hayo, maisha yanaweza yakawa magumu sana hapa ndani kwa sababu yapo mazingira ambayo hata maswali Waheshimiwa Mawaziri huwa tunawapa mengi na ziko nyakati pia ambazo hata muda wa maswali kwa mujibu wa Kanuni zetu tunapoongoza hapa mbele huwa tunaongeza kidogo ili Wabunge mpate fursa ya kusema mambo yanayotoka huko kwa wananchi wenu.

Kwa hiyo, tunaongoza hapa mbele msituwekee wakati mgumu sana kwa sababu, nilikuwa nawasikiliza hapo Mheshimiwa Juma wakati akichangia, akasema tena katika kufuata Kanuni, mimi hapa ndani katika eneo nililobobea ni hilo. Tunaweza kuamua hapa kwamba saa moja, maswali saa moja hakuna mtu mwingine kunyanyuka kufanya nini. Hilo nalo tunaweza, lakini twende kistaarabu sisi kama wamoja, Wabunge, Waheshimiwa. Nimeona nilieleze hili ili Mbunge yejote asijione yeye ni myonye, asijione yeye anaonewa, hapana. Kiti kinapofanya maamuzi iko sababu ya msingi ya kufanya hivyo. Na kwa sababu sisi kama viongozi mliotutanguliza mbele na si kwamba sisi ni bora sana kuliko ninyi, basi tuaminini kwa namna tunavyoongoza. Nafikiri hilo limeeleweka.

Sasa nililetewa pia jambo lingine nikikumbushwa hapa, wakati unatolewa mchango wa Mheshimiwa Tabasam alieleza jambo hapo kwa namna fulani hivi sasa nikawa nimeitisha Taarifa Rasmi za Bunge, maelezo yaliyoletwa hata nikaitisha hizi Taarifa Rasmi za Bunge yalielezwa kwa namna ambavyo kwamba vitisho vinavyotolewa kuhusu fedha zilizotolewa zinazoenda kwenye Halmashauri mbalimbali ni kama vile vitisho havina meno, nadhani kulikuwa na kuashiria hilo. Baadaye akachangia kuhusu *CAG* na mambo kama hayo, sasa nitasoma hiyo sehemu inayohusika ili twende vizuri.

Katika mchango wake kuna maneno ambayo nitasoma sehemu hiyo tu inayohusika na hilo jambo ambalo nimeletewa nikiwa hapo mezani na Kikanuni ninatakiwa nieleze Bunge likiwa limerejea.

Anasema; Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sasa hivi imekuwa ni wizi, tunakwenda kuziimarisha ofisi zetu kule, watu wanakwenda kuiba hizi pesa zinapelekwa hazina ukaguzi. Kwenye mpango wako hatujaona hapa sisi suala la *CAG* unakwenda kumuimarishaje *CAG*? Hatujaona kwenye mpango wako na ndiye anayekwenda kukagua hizi pesa hizi trillioni 1.3 subiri balaa lake utakuja kuliona. Pamoja na vitisho mnayovitoa sasa hivi ambavyo havina meno wataendelea kuiba hizi pesa kwa sababu, walioiba hawajapelekwa kortini mpaka sasa hivi.

Sasa yako maelezo mengine yaliyokuja baada ya hapo na mengine yalikuwa kabla ya hapo.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka wakati zikitolewa hizi fedha Mheshimiwa Rais siku ya tarehe 10 Oktoba, 2021 wakati anaeleza kuhusu fedha hizi, alisema kwamba kama yuko mtu anayetaka kufahamu rangi yake halisi basi adokoe fedha hizi. Nafikiri mlimsikia vizuri. (*Makofii*)

Baada ya yale maelekezo, wasaidizi wake, Waheshimiwa Mawaziri kwa Kadri zile fedha zilivyogawiwa kwenye sekta zao kila Waziri amekuwa akitoa sasa maelekezo kwa wale wanaotekeleza sasa yale majukumu yao. Kwa hiyo,

wamekuwa wakitoa kwa kufuata yale aliyosema Mheshimiwa Rais na wao wanafuata muelekeo huo.

Sasa sehemu hii ya mchango wa Mheshimiwa Tabasam kwa kuwa nimeletewa hayo malalamiko yanayoashiria kwamba Mheshimiwa Tabasam na kama nilivyowasomea hapa yapo dhahiri kwamba vitisho hivyo havina meno sasa ni kama yanakosa kidogo heshima kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu ndiye aliyeanza kwa kusema fedha hizi zisidokolewe na alisema mtu akitaka kufahamu rangi zake halisi basi ataziona akidokoa fedha hizi. Si kwamba ni vitisho ambavyo havina meno, meno vinayo.

Kwa kuwa meno vinayo, mchango huu wa Mheshimiwa Tabasam na kwa kutunza heshima ya Mheshimiwa Rais kama Katiba yetu inavyotutaka lakini pia kama Kanuni zetu zinavyotutaka, sehemu hii ya mchango wa Mheshimiwa Tabasam itaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, nadhani nilishawakumbusha pale mwanzo kuhusu kujizuia. Unajua lugha ya mazungumzo si sawa na lugha ya maandishi, kwa hiyo, tutaendelea kukumbushana. Unapozungumza jitahidi kujizuia ili usikosee namna ambavyo Bunge tunaendesha shughuli zetu.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 1.15 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 5 Novemba, 2021 Saa Nane Mchana)*